# MWINGILIANOTANZU NA UCHIMUZI WA MAUDHUI KATIKA FASIHI BUNILIZI ZA WATOTO

NA

CHERONO C. KIRUI

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA JAMII**

**CHUO KIKUU CHA MOI**

**2022**

# IKIRARI

**MTAHINIWA**

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya utahini katika chuo kikuu chochote. Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili sehemu yoyote ya tasnifu hii bila idhini yangu au Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi …………………………… Tarehe: …………………………………

**CHERONO C. KIRUI**
**SASS/PGK/03/19**

**WASIMAMIZI**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa ridhaa yetu kama washauri walioteuliwa na Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi …………………………… Tarehe: …………………………………

**DKT. WAFULA MAGDALINE**
Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika
Chuo Kikuu cha Moi
Eldoret

Sahihi …………………………… Tarehe: …………………………………

**DKT. MUGE TECLA**
Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika
Chuo Kikuu cha Moi
Eldoret

# TABARUKU

Kwa marehemu babangu Reuben Bii na mama Liza kwa kunihimiza niendeleze masomo yangu. Kwa mume wangu mpendwa Philip Kirui kwa kukubali kubeba majukumu ya baba na mama kwa wanangu. Wanangu Brenda, Brian, Duncan na Allan kwa kukubali kuishi bila kuwepo kwangu kwa safari hii ngumu. Kwa ndugu zangu Edward, Eric, Edmon na dadangu Chebet kwa kuniinua katika safari hii.

# SHUKURANI

Kazi hii ilihitaji jitihada nyingi ili kukamilika. Kwanza ninatoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu aliyenipa nguvu na uwezo wa kufanya utafiti na kunipa afya na uzima. Pia, ninawashukuru wote waliofanikisha uandalizi wa kazi hii kwa njia moja au nyingine. Ninashukuru Chuo Kikuu cha Moi pamoja na uongozi wake kwa kunipa nafasi niendeleze masomo yangu ya Uzamili. Hapa, niliweza kupata maarifa mbalimbali kuhusiana na taaluma ya Kiswahili, utafiti na uandishi wa utafiti kwa ujumla.

Ninatambua uelekezi wa Dkt. Wafula Magdaline na Dkt. Muge Tecla kwa ushirikiano wao wa dhati. Ninawashukuru kwa dhati kwa kukubali kunisimamia, kuniongoza na kunitia moyo pale nilipokabiliana na mambo mengi ya kukatisha tamaa. Mwenyezi Mungu awalinde, awape afya njema na kuwaongezea ufanisi katika kazi zenu. Ninawashukuru pia wahadhiri wengine kwa kunihimiza nijitahidi pamoja na kunipa mawazo na mawaidha.

Ninatoa shukrani kwa mume wangu mpendwa Philip Kirui kwa kukubali kubeba majukumu ya baba na mama kwa wanangu. Asante kwa kunivumilia na kuniwezesha pale nilipokwama nikiwa masomoni. Nashukuru kwa kuitunza familia yetu kwa muda wote niliokuwa masomoni. Mungu akubariki na uishi maisha marefu ili ushuhudie matunda ya masomo yangu. Wanangu Brenda, Brian, Duncan na Allan, mlikubali kuishi bila kuwepo kwangu kwa safari hii ngumu. Mlinivumilia sana kipindi chote nilichokuwa masomoni na mkakosa haki ya mama kama watoto na niliwaacha peke yenu mkiwa wadogo sana. Nawapenda sana watoto wangu. Mungu azidi kuwalinda na kuwapa maisha marefu yenye baraka tele. Ndugu zangu Edward, Eric, Edmon na dadangu Chebet kwa kuniinua katika safari hii. Mliniimiza nifuate maagizo ya marehemu baba, nitie bidii masomoni. Mungu awabariki sana. Babangu mdogo, Gilbert, ulisimama nami wakati nguvu zangu zilipolegea katika safari hii. Mungu akulinde na abariki familia yako.

Pia ninatoa shukurani kwa wazamili wenzangu; Agume, Adzo, Achieng' na Sera kwa mchango wao mkubwa katika uandalizi wa tasnifu hii.

# IKISIRI

Japo bunilizi nyingi za watoto katika fasihi ya Kiswahili zinabainisha sifa za mwingilianotanzu kiumbo, hakuna utafiti ambao umeangazia suala hili. Utafiti huu unachunguza namna mwingilianotanzu unachimuza maudhui katika fasihi bunilizi za watoto. Malengo ya utafiti huu ni mosi; kupambanua namna tanzu mahsusi zinajenga bunilizi teule za watoto. Pili, kuchanganua namna tanzu mahususi zinachimuza maudhui katika bunilizi teule za watoto na tatu ni kuhakiki uamilifu wa maudhui kwenye tanzu husika kwa mtoto Mwafrika katika mazingira yake. Ili kutimiza malengo haya, utafiti uliongozwa na maswali yafuatayo: Kwanza, ni tanzu zipi zinazojenga fasihi bunilizi za watoto wa daraja la tatu? Pili, ni kwa namna gani vipengele vya mwingilianotanzu vinachimuza maudhui katika fasihi bunilizi teule za watoto? Mwisho, tanzu na maudhui yanayowasilishwa kwa bunilizi teule yana uamilifu upi kwa mtoto Mwafrika? Utafiti huu umejikita katika vitabu teule vya watoto; *Mchezo wa Mtelezo na Hadithi Nyingine* (Nandwa, 2016), *Kade na Katana* (Syokau, 2018), *Mchezo wa Kobole* (Momanyi, 2019), *Kito Apepeta* (Nandwa, 2013), *Sitaki Iwe Siri* (Matundura, 2008), *Hidaya* (Namlola, 2019), na *Msiba wa Kujitakia* (Kea, 2013). Nadharia ya Mwingilianomatini yake Kristeva (1960) na Nadharia ya Uoniafrika ya Asante (1980) ndizo kiunzi cha utafiti huu. Kristeva (1960) anadai kuwa matini siku zote huingiliana na kutegemeana. Ni kwa msingi huu ndipo utafiti huu unachunguza namna tanzu anuwai zinaingiliana na kuchimuza maudhui katika bunilizi teule za watoto. Kwa upande mwingine, Uoniafrika unasisitiza kuwa maisha ya Mwafrika lazima yatathminiwe kwa kuzingatia mwonoulimwengu wake. Nadharia hii ilituongoza kuhakiki namna tanzu zinazoingiliana katika bunilizi teule zinamwangazia mtoto Mwafrika katika mazingira yake. Ukusanyaji wa data ya kimsingi ulitokana na bunilizi saba za watoto. Sampuli ya kimakusudi ilitumiwa kuteua bunilizi hizo. Data ilichanganuliwa kiufafanuzi kulingana na maswali ya utafiti na mihimili ya nadharia za utafiti. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kuwa mwingilianotanzu ni mojawapo ya mbinu ya kisanaa inayochimuza maudhui kama vile umaskini, dini, uzalendo, utangamano na mengine katika bunilizi teule. Utafiti huu ni kichocheo kwa wahakiki wa fasihi ya Kiswahili kuchunguza namna mwingilianotanzu unachimuza maudhui katika tanzu nyinginezo za fasihi andishi na simulizi. Aidha, utafiti huu unachangia pakubwa katika kubainisha vigezo vya utunzi hasa wa fasihi ya watoto katika Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika.

.

## ABSTRACT

Although most of the Kiswahili children's fiction literature are intergenrical in nature, no study has examined intergenral as a literal strategy. This research focuses on how the intergenral aspect in children's fiction foregrounds specific themes. The research was guided by the following objectives; First and foremost, to expound different genres that constitute the selected children's fiction. Secondly, to examine how various genres foreground specific themes in the selected texts. Thirdly, to analyse the relevance of the genres and the captured themes to the African child.To realize the specific objectives, the study set out to answer the following questions: What are the specific genres that constitute the selected children's fiction for level 3 children? How do the specific genres foreground specific themes in the selected children's fiction? How relevant are the genres and themes in the selected texts to the African child? This research was based on selected texts; *Mchezo wa Mtelezo na Hadithi Nyingine* (Nandwa, 2016), *Kade na Katana* (Syokau, 2018), *Mchezo wa Kobole* (Momanyi, 2019), *Kito Apepeta* (Nandwa, 2013), *Sitaki Iwe Siri* (Matundura, 2008), *Hidaya* (Namlola, 2019) and *Msiba wa Kujitakia* (Kea, 2013). Intertextuality and Afrocentric theories propagated by Kristeva (1960) and Asante (1980) respectively guided this research. Kristeva argues that every text is related to another text in one way or another. This theory was used to analyse the different genres and themes depicted in children's texts. Afrocentric Theory of Asante emphasizes the central position of the African subject within the context of African history. Therefore, Afrocentric Theory guided our quest to establish how various genres deployed in the selected children's fiction are relevant to the African child. This is a library research involving seven children's fiction sampled purposefully. Primary data from the seven texts was analysed using explanatory method based on the research questions and the theories guiding this study. The study findings reveal that the intergenrical feature in the seven texts is a literary strategy that foregrounds specific themes such as religion, poverty, culture among others in children's fiction. This study is important in that it is a motivation to Kiswahili literary critiques to investigate the function of the intergenrical style in other literary texts. Moreover, this study will offer useful guidelines on the composition and analysis of children's fiction in Kiswahili and in other African languages.

.

# YALIYOMO

IKIRARI ............ ii
TABARUKU ............ iii
SHUKURANI ............ iv
IKISIRI ............ v
ABSTRACT ............ vi
YALIYOMO ............ vii
ORODHA YA MICHORO ............ xii
UFAFANUZI WA ISTILAHI ............ xiii
TAFSIRI YA MANENO ............ xiv
MAELEZO YA VIFUPISHO ............ xv
**SURA YA KWANZA ............ 1**
**MISINGI YA UTAFITI ............ 1**
1.0 Utangulizi ............ 1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti ............ 1
1.1.1 Dhana ya Mtoto ............ 2
1.1.2 Dhana ya Fasihi ya Watoto ............ 4
1.1.3 Dhana ya Mwingilianotanzu ............ 6
1.2 Suala la Utafiti ............ 7
1.3 Malengo ya Utafiti ............ 8
1.4 Maswali ya Utafiti ............ 8
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ............ 8
1.6 Umuhimu wa Utafiti ............ 9
1.7 Upeo wa Utafiti ............ 10
**SURA YA PILI ............ 12**
**MBINU ZA UTAFITI ............ 12**
2.0 Utangulizi ............ 12
2.1 Eneo la Utafiti ............ 12
2.2 Uteuzi wa Sampuli ............ 12
2.3 Vifaa vya Kukusanya Data ............ 13
2.3.1 Tarakilishi ............ 13
2.3.2 Kalamu, Karatasi na Shajara ............ 13
2.4 Ukusanyaji wa Data ............ 13

2.5 Uwasilishaji na Uchanganuzi wa Data ..... 14
2.6 Hitimisho ..... 14
**SURA YA TATU ..... 15**
**MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA ..... 15**
3.0 Utangulizi ..... 15
3.1 Dhana ya Mwingilianomatini ..... 15
3.2 Dhana ya Mwingilianotanzu ..... 19
3.3 Msingi wa Kinadharia ..... 25
3.3.1 Nadharia ya Mwingilianomatini ..... 25
3.3.2 Nadharia ya Uoniafrika ..... 27
3.4 Hitimisho ..... 30
**SURA YA NNE ..... 31**
**TANZU MAHUSUSI ZINAZOJENGA BUNILIZI TEULE ZA WATOTO ..... 31**
4.0 Utangulizi ..... 31
4.1 Muhtasari wa Bunilizi Husika ..... 31
4.1.1 *Sitaki iwe Siri* (Bitugi Matundura, 2008) ..... 32
4.1.2 *Kito Apepeta* (Rebeca Nandwa, 2013) ..... 32
4.1.3 *Kade na Katana* (Caroline Syokau, 2018) ..... 33
4.1.4 *Mchezo wa Kobole* (Clara Momanyi, 2009) ..... 33
4.1.5 *Hidaya* ( Juma Namlola, 2019) ..... 34
4.1.6 *Mchezo wa Mtelezo* (Rebeca Nandwa, 2016) ..... 35
4.1.7 *Msiba wa Kujitakia* (Pauline Kea, 2013) ..... 35
4.2 Wimbo ..... 36
4.2.1 Wimbo ndani ya simulizi ..... 38
4.2.2 Matumizi ya wimbo katika Bunilizi ya Kitamthilia ..... 41
4.2.3 Wajibu wa nyimbo katika fasihi ya watoto ..... 43
4.2.3.1 Kukuza watoto kiakili /kifikra ..... 44
4.3 Utanzu wa Mashairi ..... 46
4.3.1 Ushairi ..... 46
4.3.2 Mashairi katika bunilizi za watoto ..... 48
4.3.3 Umuhimu wa mashairi kwa watoto ..... 52
4.4 Utanzu wa Barua ..... 53
4.4.1 Utanzu wa barua ndani ya bunilizi ..... 54
4.4.2 Barua ndani ya hekaya kwenye bunilizi ..... 56

4.5 Mazungumzo Ndani ya Hadithi kwenye Simulizi ................................................59
4.6 Utanzu wa Ndoto ndani ya Hadithi........................................................................60
4.7 Hekaya/Hadithi Ndani ya Usimulizi ......................................................................61
4.8 Utanzu wa Sala .......................................................................................................62
4.9 Utanzu wa Insha katika Bunilizi ............................................................................63
4.10 Utanzu wa Picha au Michoro Mbalimbali ...........................................................65
4.11 Michezo ya Watoto ...............................................................................................66
4.12 Dhima ya Mwingilianotanzu katika Bunilizi za Watoto......................................67
4.13 Hitimisho..............................................................................................................68
**SURA YA TANO .......................................................................................................69**
**NAMNA MWINGILIANOTANZU UNACHIMUZA MAUDHUI KATIKA BUNILIZI ZA WATOTO ...........................................................................................69**
5.0 Utangulizi...............................................................................................................69
5.1 Maudhui .................................................................................................................69
5.1.1 Dini.....................................................................................................................71
5.1.2 Maadili, bidii na utiifu........................................................................................74
5.1.3 Umaskini ............................................................................................................80
5.1.3.1 Umaskini Utokanao na Kifo ...........................................................................80
5.1.3.2 Umaskini Utokanao na Changamoto za Maisha.............................................81
5.1.4 Magonjwa...........................................................................................................84
5.1.4.1 Ugonjwa utokanao na ushirikina ....................................................................85
5.1.4.2 Ugonjwa utokanao na kutotii..........................................................................86
5.1.4.3 Ugonjwa wa Ukimwi.......................................................................................87
5.1.5 Ushiriakiano na Utangamano katika jamii .........................................................88
5.1.6 Haki za Watoto...................................................................................................97
5.1.6.1 Haki ya kukua ..................................................................................................98
5.1.6.2 Haki ya ushiriki wa mtoto ..............................................................................101
5.1.6.3 Haki ya Kutofanya kazi za Sulubu .................................................................102
5.1.7 Ushujaa.............................................................................................................103
5.1.8 Malezi...............................................................................................................108
5.1.8.1 Malezi ya mtoto nyumbani ............................................................................109
5.1.8.2 Malezi ya mtoto shuleni ................................................................................110
5.1.9 Utamaduni ........................................................................................................111
5.1.9.1 Uraia na Amani..............................................................................................118

5.1.9.2 Umoja na Bidii ..... 118
5.1.9.3 Upendo ..... 118
5.1.10 Uwajibikaji ..... 119
5.2 Hitimisho ..... 120
**SURA YA SITA ..... 122**
**UAMILIFU WA MAUDHUI NA VIPENGELE VYA MWINGILIANOTANZU KATIKA BUNILIZI TEULE KWA MTOTO MWAFRIKA ..... 122**
6.0 Utangulizi ..... 122
6.1 Uamilifu wa Maudhui na Tanzu mbalimbali katika bunilizi teule ..... 122
6.1.1 Dini ..... 123
6.1.2 Umaskini ..... 126
6.1.3 Ushujaa ..... 130
6.1.4 Utamaduni ..... 131
6.1.5 Ushirikiano na Utangamano ..... 135
6.1.6 Magonjwa ..... 136
6.1.7 Malezi ..... 139
6.1.8 Haki za Watoto ..... 140
6.1.9 Maadili na Adabu ..... 141
6.1.10 Uzalendo ..... 142
6.1.11 Bidii na uvivu ..... 143
6.2 Uamilifu wa Tanzu mbalimbali katika Bunilizi za Watoto ..... 143
6.2.1 Barua ..... 143
6.2.2 Picha na Michoro ..... 144
6.2.3 Hekaya ndani ya bunilizi ..... 144
6.2.4 Maigizo ..... 144
6.2.5 utanzu wa sala ndani ya bunilizi ..... 145
6.2.6 Utanzu wa ndoto ndani ya simulizi ..... 145
6.2.7 Insha ndani ya bunilizi ..... 146
6.2.8 Mazungumzo ndani ya hadithi ..... 146
6.2.9 Utanzu wa nyimbo ndani ya bunilizi ..... 147
6.2.10 Mashairi katika bunilizi ..... 147
6.3 Hitimisho ..... 148

**SURA YA SABA ........................................................................................ 149**
**MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO ............................................ 149**
7.0 Utangulizi ................................................................................................ 149
7.1 Muhtasari wa Tasnifu ............................................................................... 149
7.2 Matokeo na Mahitimisho ya Utafiti ........................................................... 152
7.2.1 Mwingilianotanzu katika Bunilizi za Watoto ............................................ 152
7.2.2 Uchimuzi wa Maudhui ........................................................................... 153
7.2.3 Uamilifu wa Maudhui na vipengele vya Mwingilianotanzu ........................ 154
7.3 Mchango wa Utafiti ................................................................................. 155
7.4 Mahitimisho ............................................................................................. 155
7.5 Mapendekezo .......................................................................................... 156
MAREJELEO ............................................................................................... 158

# ORODHA YA MICHORO


Mchoro 1: Katana akiwa na ajuza....83

Mchoro 2: Katana akielekea uvuvini....84

Mchoro 3: Watoto wakitangamana na kushirikiana katika kuchagua wimbo....91

Mchoro 4: Watoto wakicheza mchezo wa mchongoma....93

Mchoro 5: Nyanya Mwalongo na wajukuu wake....95

Mchoro 6: Mchoro unaoonyesha utangamano wa watoto wanapocheza na kuimba pamoja....96

Mchoro 7: Mchoro unoonyesha watoto wakifanyizwa kazi za sulubu....103

Mchoro 8: Nyumba ya kiasili....113

Mchoro 9: Taswira ya maandalizi ya uwasilishwaji wa hadithi katika baadhi ya jamii za Kiafrika....114

Mchoro 10: Mavazi zenye dhihirisho la utamaduni wa jamii....116

Mchoro 11: Hali ya Katana akiwa amevalia nguo kuukuu iliyojaa viraka....128

Mchoro 12: Matumizi ya ala za muziki katika utendaji....132

Mchoro 13: Taswira ya maandalizi ya uwasilishwaji wa hadithi katika jamii ya Kiafrika....134

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

Istilahi hizi zimetumika kwa mujibu wa utafiti huu;

**Bunilizi za watoto:** Hizi zinahusu fasihi za watoto zilizoandikwa kwa mtindo wa kiutondoti. Katika utafiti huu, ni tungo za kifasihi zinazomlenga mtoto wa daraja la tatu.

**Bunilizi:** Ni fasihi za kubuni zilizoandikwa kwa mtindo wa kiutondoti

**Mwingilianomatini:** Dhana hii imetumika kurejelea uhusiano wa matini mbalimbali na mbinu zingine za kisanaa katika kuboresha bunilizi za watoto.

**Mwingilianotanzu:** Hii imetumika kurejelea uhusiano wa tanzu mbalimbali zinavyoingiliana na kuhusiana pamoja na mbinu zingine za kisanaa katika kuboresha bunilizi za watoto.

**Senta au Kati:** Dhana hii imetumika kwa maana ya kuhusishwa kwa mambo ya kimsingi yanayohusiana na masuala ya kijamii.

**Uchimuzi:** Kufanya sifa fulani ijitokeze mbele au kubainika waziwazi.

**Uoniafrika:** Nadharia inayomthamini Mwafrika kwa kuzingatia historia yake akiwa kwenye kiini cha utamaduni wake.

# TAFSIRI YA MANENO

| **Kiswahili** | **Kiingereza** |
|---|---|
| Daraja la tatu | *Class* 4-8 |
| Mwingilianomatini | *Intertextuality* |
| Mwingilianotanzu | *Intergenre* |
| Senta au Kati | *Centrality* |
| Uoniafrika | *Afrocentricity* |

# MAELEZO YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **ILO** | - | International Labour Organization |
| **KICD** | - | Kenya Institute of Curriculum Development |
| **MM** | - | Mwingilianomatini |
| **MT** | - | Mwingilianotanzu |
| **UA** | - | Uoniafrika |
| **UNICEF** | - | United Nations Children’s Fund |

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii imeweka wazi misingi ya utafiti huu. Hapa usuli wa suala la utafiti umebainishwa ambapo dhana ya mtoto na fasihi ya watoto imefafanuliwa kwa kina. Aidha, suala la utafiti, malengo na maswali ya utafiti yamefafanuliwa. Hali kadhalika, sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti, upeo na mbinu za utafiti zimeelezwa.

## 1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Sehemu hii ni msingi wa masuala yanayoshughulikiwa katika usuli wa suala la utafiti. Kwa ujumla, utafiti huu ni wa kifasihi hususan fasihi ya watoto. Fasihi hii ya watoto ni fasihi changa na utafiti mwingi haujafanywa hususan kuhusiana na mada. Fasihi ya watoto ni fasihi iliyoandikwa kwa ajili ya kusomwa na kumfaa mhusika ambaye ni mtoto. Ikumbukwe kwamba fasihi ya watoto inajumlisha mashairi, michezo ya kuigiza (tamthilia fupi ya watoto), bunilizi za watoto( riwaya fupi au fasihi ya kinathari), hadithi fupi za watoto na hata fasihi simulizi ya watoto. Hivyo basi, utafiti huu umeegemea bunilizi au fasihi ya kinathari ambapo tuliangazia mwingiliano wa tanzu na uchimuzi wa maudhui kutoka tanzu hizo katika bunilizi teule. Hali kadhalika, utafiti ulitathmini ikiwa tanzu (nyimbo, maigizo, barua, mashairi, insha n.k) na maudhui (magonjwa, dini, utamaduni, uzalendo) yaliyochimuzwa yalimfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake asilia. Hata hivyo, katika kuujenga utafiti huu, ufafanuzi wa istilahi za kimsingi ulitolewa. Hapa, ufafanuzi wa dhana ya mtoto umetolewa kwa kina. Vile vile maelezo kuhusu fasihi ya watoto ikiwemo bunilizi za watoto na mwingilianotanzu umefafanuliwa.

### 1.1.1 Dhana ya Mtoto

Dhana ya mtoto ni pana na ina utata kwa kiasi fulani kutegemea mwega wa mtoa maana hiyo. Watu wa dini mbalimbali hasa za Kikristo, watu wazima, wazee kwa vijana hudai kuwa wao ni watoto wa Mungu (Bakize, 2014). Kwa mtazamo huo wa Bakize, mtoto hakui, anabaki kuwa hivyo mpaka kufa. Mungu anabaki kuwa baba. Mbali na imani za kidini, mtu anapozaliwa wazazi wanamwita mtoto, hata akue, awe na mvi, iwapo wazazi wake wangali hai, anabaki mtoto mbele yao.

Ibala (2018) anasema kila jamii ina njia zake za kutofautisha watoto na watu wazima. Jamii za kiasili hapa nchini Kenya hutumia njia anuwai za kitamaduni zinazotumiwa kutambua mtu mzima. Njia hizi ni kama vile matumizi ya jando, ambapo baada ya kupitia shughuli hizi za kiutamaduni, mtoto huchukuliwa kuwa amekuwa mtu mzima. Katika baadhi ya jamii, kutolewa kwa meno sita ya chini au kutahiri kwa wavulana ndicho kigezo kinachotumiwa kutofautisha watoto na watu wazima (Agalo, 2012).

Shirika la Kazi Duniani (International Labour Organization) linatambua kuwa mtoto ni mtu yeyote mwenye umri wa chini ya miaka 18. Wafula (2011) katika kufafanua dhana hii, amegawanya watu katika makundi makuu manne. Anadai kuwa rika la utoto ni miaka 0-17, rika la ujana ni miaka kati ya 18-34, rika la wazazi (utu uzima) ni miaka kati ya 35-52, rika la wazee ni miaka 53 na kuendelea. Kwa mgawanyo huo, mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18. Mtazamo huu ni sawa na ule wa Shirika la Kazi Duniani. Nchini Kenya, katiba iliyoidhinishwa mwaka wa 2010 vilevile inasema kwamba mtoto ni mtu aliye na miaka chini ya 18. Hata hivyo, Kahigi (1995) akifafanua vitabu vya kundi la watoto anasema kuwa, mradi wa Vitabu vya Watoto Tanzania unatambua ngazi tatu za vitabu hivyo; ngazi I: Awali hadi darasa la 2, ngazi II: darasa la 3 hadi 4 na ngazi III: darasa la 5 hadi 7.

Erastus (2017) anasema kwamba, watoto wale walio katika darasa la kwanza na wana bunilizi zao, wa darasa la pili wana bunilizi zao, wa tatu na la nne wanazo zao pia, hali kadhalika wale wa darasa la tano hadi saba. Lengo la mgawanyo huu ni kuwawezesha watoto kumudu kuzisoma na kuzielewa bunilizi hizo kulingana na upeo wao wa kiakili. Erastus anaendelea kusema kwamba, mtoto anayejua mambo mengi, huwa pia jasiri wa kusimama mbele ya wenzake darasani na kueleza visa na matukio aliyoyasoma. Ujasiri huo hauishii pale, bali mtoto huyo huendelea hivyo maishani.

Maelezo hayo yamejikita katika viwango vya madarasa ya watoto. Hata hivyo, tunaweza kutambua kwamba ngazi hizi zote ni za watoto wenye umri chini ya miaka 18. Wao wana fikra changa kutokana na umri wao mdogo na walio chini ya uangalizi wa watu wazima kimalezi na kimahitaji. Ni kikundi cha jamii wasio na uhuru wa kujitawala au kujifanyia maamuzi.

Tucker (1981) anasema kwamba, mtoto ni binadamu ambaye ana umri wa miaka kumi na mitano kurudi chini. Hawa ni watoto ambao ni wa umri wa kuanza shule na kabla ya kubaleghe. Hali kadhalika, shirika la UNICEF linatambua kwamba, mtoto ni binadamu yeyote aliye chini ya miaka kumi na mitano kurudi chini. Ingawa wataalam hawa wote wana maoni yao tofauti kuhusu dhana ya mtoto, wote wanaafikiana kwamba mtoto ni binadamu yeyote mwenye umri wa miaka kumi na minane kurudi chini na walio chini ya uangalizi wa wazazi na walimu. Katika utafiti wetu, mtoto anayezungumziwa ni yule wa daraja la tatu. Mtoto huyu anashughulikiwa kupitia kwa fasihi inayomlenga. Daraja la tatu hapa kulingana na uratibu wa 8: 4: 4 ni kiwango cha darasa la nne hadi nane wenye umri wa miaka 9 hadi 13 hivi. Kikundi hiki ni cha watoto ambao wana uwezo wa kusoma na kuelewa mtiririko wa bunilizi ambazo wanazisoma.

### 1.1.2 Dhana ya Fasihi ya Watoto

Fasihi ya watoto ni fasihi inayoandikwa kwa ajili ya watoto (Wamitila, 2003). Upekee wa fasihi hii ni kuwa inabeba ujumbe mwepesi kwa ajili ya watoto. Wamitila (2010) anasema kuwa, fasihi ya watoto inaweza kueleweka kwa kukitwa katika mitazamo mikuu miwili: Mosi, fasihi ya watoto ni ile ambayo imetungwa na kuandikwa au kusimuliwa na mtoto. Pili, ni ile fasihi ambayo imetungwa na kusimuliwa na mtu mzima. Kwa kuongezea mawazo ya Wamitila, ni muhimu kusisitiza kuwa mtu mzima anayesimulia kisa husika anamlenga mtoto. Kwa hivyo mitazamo yote miwili inalenga watoto kama hadhira. Mawazo hayo yanaungwa mkono na Ismael (2015) na Ibala (2018) wanaokiri kuwa fasihi ya watoto ni kazi zozote zilizoandikwa aidha na watoto wenyewe au na watu wazima kwa ajili ya watoto.

Muge (2018), anapambanua vigezo vikuu vitatu vinavyotambulisha fasihi ya watoto ambavyo ni; kwanza, mhusika mkuu lazima awe mtoto. Pili, dhamira iwahusu watoto na tatu, lugha sahili itumiwe kuendeleza msuko. Mawazo ya Muge ni muhimu kwa sababu yanadokeza sifa za umbo na muundo wa fasihi ya watoto ambazo ni muhimu katika utafiti wetu. Utafiti wetu unalenga kuangazia mwingilianotanzu katika bunilizi teule za watoto. Kwa hivyo, tulichunguza namna bunilizi hizi zinajipambanua kuhusiana na lugha sahili ilivyotumika kuzisuka bunilizi hizo.

Ngugi (2012) anaeleza kuwa, fasihi ya watoto ni fasihi iliyoandikwa kwa minajili ya kusomwa na watoto. Kwa upande wake, Bakize (2014) anabainisha kuwa fasihi ya watoto inalenga hadhira ya watoto wa umri wa chini ya miaka kumi na minane na inayohusu watoto pekee. Fasili ya Bakize na ile ya Ngugi ina uhusiano wa karibu kwa sababu Ngugi (2012) alirejelea fasihi iliyoandikwa ilhali Bakize (2014) anaeleza kuwa fasihi ya watoto ni ile iliyoandikwa au kusimuliwa kwa mdomo. Fasihi simulizi

za watoto ni kama nathari nyepesi, mashairi mepesi yanayoweza kuimbwa na watoto, nyimbo za watoto, hadithi simulizi za watoto na maigizo mepesi ya watoto. Nayo fasihi andishi ya watoto inajumuisha hadithi zilizoandikwa za watoto, vitabu vya watoto, vitabu vya vibonzo, mashairi mepesi yaliyoandikwa na tamthilia nyepesi zilizoandikwa (Njeri, 2019). Maelezo ya Njeri yanafaa utafiti huu maana baadhi ya tanzu katika vipera vyote vya fasihi ya watoto vitashughulikiwa. Utafiti huu unalenga watoto wa daraja la tatu wenye umri wa miaka 9 hadi 13. Kikundi hiki ni cha watoto ambao wana uwezo wa kusoma na kuelewa yale ambayo wanayasoma katika bunilizi zao.

Kutokana na mawazo ya wataalam tuliowarejelea, ni wazi kuwa, fasihi ya watoto zikiwemo bunilizi za watoto hujipambanua kwa umbo na maudhui mahususi. Watunzi hutumia mbinu mahususi za kisanaa ili kuunda tungo za watoto kwa lengo la kuwasilisha maudhui ama masuala maalum kwa hadhira ya watoto. Ni bayana kuwa tungo mbalimbali katika fasihi ya watoto katika Kiswahili zinadhihirisha upekee fulani kiumbo. Mojawapo ya upekee huu ni mwingilianotanzu. Mathalan bunilizi nyingi za watoto katika fasihi ya Kiswahili zimejengwa kwa tanzu mbalimbali kama, hadithi (simulizi), semi, maigizo, mashairi na hata picha. Tunadhukuru kuwa, upekee huu wa umbo wa bunilizi za watoto katika fasihi ya Kiswahili umekusudiwa kutekeleza majukumu maalum na watunzi wa bunilizi hizi. Kwa mfano katika *Kito Apepeta* (Nandwa, 2013), tunaona simulizi, picha, shairi, na hata nyimbo zikijitokeza katika bunilizi hii. Nayo bunilizi ya *Mchezo wa Kobole* (Momanyi, 2009), imejengwa kwa picha, nyimbo, na hata mazungumzo.

Osazee (1991) katika Ngugi (2012) anasema kwamba fasihi ya watoto ni ule ubunifu wa kifasihi unaoibua dhana ya Uafrika na inayoandikwa kwa lugha na mbinu zinazofaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake. Ni fasihi inayoendeleza tamaduni

za Kiafrika na kumwezesha mtu mzima kufahamu na kuyapenda mazingira yake ipasavyo (Tafsiri yetu). Maelezo ya Osazee ni muhimu hapa maana kazi yetu inaangalia ikiwa maudhui yanayowasilishwa na hali kadhalika vipengele vya mwingilianotanzu vinamfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake au la?

### 1.1.3 Dhana ya Mwingilianotanzu

Mwingilianotanzu hurejelea mtagusano wa tanzu mbalimbali katika matini na namna utanzu unavyotagusana na tanzu zingine zote kwa ujumla ili kuboresha uwasilishaji wa ujumbe (Mulokozi, 1989). Maoni haya yanaafikiana na maoni ya Murimi, Obuchi na Kandagor (2016) ambao wanadai kuwa, tanzu mbalimbali katika kazi za fasihi huingiliana kimaudhui na kifani ili kuboresha uwasilishaji wa ujumbe kwa hadhira. Kimsingi, wataalam hawa wanabainisha kuwa mwingilianotanzu ni mbinu ya kisanaa inayojumuisha tanzu mbalimbali za fasihi katika utanzu mkuu maalum. Mathalan, utanzu wa riwaya unaweza kujumuisha tanzu za ushairi, maigizo, picha, hekaya na hata mazungumzo. Tanzu hizi huingiliana ili kusuka utanzu wa riwaya kiumbo na pia kuwasilisha maudhui maalum kwa hadhira lengwa.

Kwa vile kuna uhusiano kati ya mbinu za kisanaa na yaliyomo, inawezekana kuwa, watunzi wa bunilizi za watoto hutumia mbinu mahususi ya kisanaa ikiwemo mwingilianotanzu kuchimuza maudhui maalum kuhusiana na mtoto Mwafrika. Huu ndio msingi wa utafiti huu kuchunguza matumizi ya mwingilianotanzu katika bunilizi teule katika fasihi ya Kiswahili.

Katika fasihi za watoto, bunilizi zikiwemo, kuna uhusiano mkubwa kati ya mbinu za kiutunzi na yaliyomo au maudhui. Mbinu za kisanaa hujenga muundo wa kazi kwa jumla. Mbinu hizi huingiliana na kutegemeana katika ujenzi wa yaliyomo. Kwa hivyo lengo la kuwepo kwa mbinu hizi katika kazi za kifasihi ni kuchimuza maudhui fulani

yanayolengwa na mwandishi. Mbinu hizi za kiutunzi lazima ziwe wazi na zinazosisimua kwa mtoto. Mbinu hizi huingiliana katika bunilizi za watoto kwa lengo la kupitisha ujumbe fulani kwa mtoto. Ujumbe huu unaweza kuwa unaelekeza kuhusu masuala ya malezi, maadili, magonjwa, haki za watoto, utamaduni, elimu kati ya mengine yanayomhusu mtoto anayelengwa.

Katika kuangalia uhusiano huu, basi utafiti wetu uliangalia jinsi mwingiliano wa tanzu mbalimbali katika bunilizi teule za watoto unachimuza maudhui yanayomfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake asilia.

**1.2 Suala la Utafiti**

Utafiti huu ni uchunguzi wa namna mwingilianotanzu unachimuza maudhui katika bunilizi za watoto wa daraja la tatu. Bunilizi za watoto: *Mchezo wa Mtelezo na Hadithi Nyingine* (Nandwa, 2016), *Kade na Katana* (Syokau, 2018) *Mchezo wa Kobole* (Momanyi, 2019), *Kito Apepeta* (Nandwa, 2013), *Sitaki Iwe Siri* (Matundura, 2008) *Hidaya* (Namlola, 2019), *Msiba wa Kujitakia* (Kea, 2013) zinasheheni mwingiliano wa tanzu anuai kiumbo. Kwa vile fani na maudhui katika kazi za fasihi huenda sambamba, utafiti huu ulilenga kufafanua usambamba huu kwa kutathmini namna mwingilianotanzu unajitokeza kama mbinu ya kisanaa inayochimuza maudhui kwa ajili ya mtoto Mwafrika.

Mwingilianotanzu ni mojawapo ya sifa za bunilizi za watoto katika fasihi ya Kiswahili katika kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa na waandishi kwa hadhira lengwa ambayo ni mtoto Mwafrika. Wataalam wengine wameshughulikia mwingilianotanzu katika fasihi ya watoto, lakini hakuna aliyejikita katika uchimuzi wa maudhui kwenye bunilizi za watoto na hasa kuonyesha nafasi ya mtoto Mwafrika. Kupitia uchunguzi wa namna mwingilianotanzu unajengwa katika fasihi bunilizi za watoto, pana haja ya

kuangalia iwapo mtoto Mwafrika amezingatiwa katika mazingira yake. Ni kwa msingi huo ndipo utafiti huu unachunguza iwapo mwingilianotanzu unaweza kuchimuza maudhui katika fasihi bunilizi za watoto wa Kiafrika.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo yafuatayo:

i. Kupambanua namna tanzu mahsusi zinajenga bunilizi teule za watoto.
ii. Kuchanganua namna vipengele vya mwingilianotanzu vinachimuza maudhui katika fasihi bunilizi teule za watoto.
iii. Kuhakiki uamilifu wa maudhui na tanzu kwenye bunilizi teule kwa mtoto Mwafrika.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:

i. Je, ni tanzu zipi zinajenga bunilizi teule za watoto?
ii. Je, tanzu zinazoingiliana zinachimuza maudhui yepi katika bunilizi teule?
iii. Je, tanzu na maudhui yanayowasilishwa katika bunilizi husika yana uamilifu upi kwa mtoto Mwafrika?

### 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Utafiti huu unaangazia umuhimu wa maudhui na fani kama vipengele vinavyojengana katika kazi yoyote ya fasihi. Kwa hivyo kuna haja ya kuchunguza namna mwingilianotanzu kama sehemu ya fani (muundo) na maudhui yanahusiana katika bunilizi za watoto. Aidha, bunilizi za watoto zina upekee kimuundo kwa sababu ya hadhira inayojengwa. Kwa hivyo matumizi ya mwingilianotanzu yanachunguzwa kwa mujibu wa dhima zake katika kuwasilisha ujumbe mahsusi kwa mtoto Mwafrika.

**1.6 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu utakuwa marejeleo muhimu katika kufanya uchunguzi wa namna tanzu mahususi zinajenga bunilizi teule za watoto. Aidha, kupitia ujenzi huo, maudhui mbalimbali yanayochimuzwa na tanzu hizo zitawasaidia wahakiki wa fasihi kutambua uamilifu wa tanzu hizo kwa mtoto Mwafrika katika mazingira yake asilia. Aidha, watafiti wengi watapata nafasi na sababu ya kumshirikisha mtoto Mwafrika katika mazingira yake. Vipengele mahususi vya kimwingilianotanzu vimetumika hasa katika kile kiwango cha watoto wa daraja la tatu kwa sababu ya ule mvuto unaoambatana na vipengele hivyo.

Mtoto Mwafrika asilia anapaswa kuyafahamu mazingira yake kupitia kwa maudhui yanayochimuzwa na vipengele vinavyojenga bunilizi zao kupitia usomaji. Kwa mfano, mwandishi anapozungumzia kuhusu Bahari ya Pwani ya Afrika Mashariki, mtoto anayetoka bara huenda akatatizika kuelewa kuhusu kinachozungumziwa.

Utafiti huu utatoa mwanga kwa waandishi wa kisasa hasa wanaochangamkia bunilizi za watoto kwamba katika uandishi wao wa kubuni, lazima wamhusishe mtoto Mwafrika katika mazingira yake asilia.

Aidha, utafiti huu unanuiwa kuwahamasisha waandishi wa Kiswahili walioko Afrika 1kwamba, wanapaswa kuzingatia historia na tamaduni za mtoto Mwafrika katika uandishi wao hasa kuhusiana na muainisho wa vipengele vya kimwingilianotanzu. Vilevile, utafiti huu utakuwa nguzo kuu katika fasihi bunilizi za Kiswahili pamoja na kurutubisha maandishi katika bunilizi za watoto.

Hali kadhalika, tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu suala la mwingilianotanzu, zimefanywa katika fasihi Simulizi ila hakuna tafiti zilizofanywa kuhusu namna mwingilianotanzu unachimuza maudhui katika fasihi bunilizi za watoto. Hivyo, kwa

kutafitia mwingilianotanzu katika fasihi bunilizi za watoto, maarifa zaidi yatakuwepo kwa watafiti wa siku za baadaye.

Utafiti huu ni muhimu kinadharia kwa sababu unapambanua ufaafu wa nadharia ya mwingilianomatini katika kuonyesha vile vipengele vinavyoingiliana katika bunilizi za watoto. Hali kadhalika, unapambanua nadharia ya Uoniafrika katika kuonyesha kuwa mtoto Mwafrika amehusishwa katika mazingira yake asilia ama anasingiziwa tu matini asiyoielewa. Muhimu ni uzingatifu wa mtoto Mwafrika katika mazingira yake asilia. Hata hivyo, ni wazi kuwa Uoniafrika umethibitika katika bunilizi teule. Kulingana na utafiti wetu, inabainika kwamba, vipengele vinavyoingiliana vinachimuza maudhui kama dini, utamaduni, ushirikiano na utangamano, magonjwa, uwajibikaji na mengine katika kazi husika. Hali kadhalika, kutokana na utafiti wetu, imebainika kwamba, waandishi wa bunilizi za watoto wamezingatia mhimili wa nadharia ya Uoniafrika.

### 1.7 Upeo wa Utafiti

Ili kufanikisha malengo yake, utafiti huu unajikita kwenye bunilizi saba tu. Bunilizi hizo ni: *Mchezo wa Mtelezo na Hadithi Nyingine* (Nandwa, 2016), *Kade na Katana* (Syokau, 2018), *Mchezo wa Kobole* (Momanyi, 2009), *Kito Apepeta* (Nandwa, 2013), *Sitaki Iwe Siri* (Matundura), *Hidaya* (Namlola, 2019), *Msiba wa Kujitakia* (Kea, 2013). Vitabu hivi vimeteuliwa kimakusudi kwa sababu vina data zinazofaa uchanganuzi ili kufikia malengo ya utafiti. Data hizo ni vipengele vya mwingilianotanzu kama vile matumizi ya nyimbo, ushairi, hadithi ndani ya hadithi, maigizo, insha, barua na mengine. Hali kadhalika kutathmini ikiwa vipengele hivyo vinachimuza maudhui yanayomfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake.

Fasihi bunilizi za watoto na kazi nyingine za fasihi zilirejelewa mara kwa mara kwa lengo la ufafanuzi zaidi au kuwianisha mawazo yanayohusika. Sehemu inayofuata imeshughulikia mbinu zilizotumika katika utafiti.

# SURA YA PILI

# MBINU ZA UTAFITI

## 2.0 Utangulizi

Kothari (2008) anasema kwamba, mbinu za utafiti ni muhimu sana katika kufanya uchunguzi wa kitaaluma, kutokana na mbinu hizo ndipo utafiti unaweza kufanyika kisayansi. Katika sehemu hii tumeelezea kuhusu, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data na hali kadhalika vifaa vya kukusanya data, uwasilishaji na uchanganuzi wa data.

## 2.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanywa maktabani ambapo bunilizi teule zimechunguzwa. Tulisoma makala mbalimbali yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti kwenye mtandao na pia maktabani.

## 2.2 Uteuzi wa Sampuli

Borg na Gall (1996) wanasema kwamba, usampulishaji ni njia au utaratibu wa kuteua washiriki wachache kutoka katika kundi kubwa la jumla la watafitiwa wote. Katika utafiti huu, sampuli ilikuwa ya kimakusudi. Tuliteua vitabu vya watoto katika viwango vya daraja la tatu. Sampuli ya makusudi kwa mujibu wa Scott na Deirdre (2009) ni uteuzi wa sampuli kwa sababu ina vipengele vinavyoafiki malengo ya utafiti. Katika utafiti huu, tumeteua kimakusudi vitabu: *Mchezo wa Mtelezo na hadithi Nyingine* (Nandwa, 2016), *Kade na Katana* (Syokau, 2018), *Mchezo wa Kobole* (Momanyi, 2009), *Kito Apepeta* (Nandwa, 2013), *Sitaki Iwe Siri* (Matundura), *Hidaya* (Namlola), *Msiba wa Kujitakia* (Kea 2013). Nia kuu ya uteuzi huu ni kuwa vina data mahususi iliyounda kiunzi cha uchanganuzi wetu ili kutimiza malengo ya utafiti.

## 2.3 Vifaa vya Kukusanya Data

Vifaa vilivyotumika katika utafiti huu ni;

### 2.3.1 Tarakilishi

Tarakilishi pakatwa ilitumiwa na mtafiti kutafuta matini katika tovuti na kuhifhadi data mbalimbali.

### 2.3.2 Kalamu, Karatasi na Shajara

Hivi vifaa vilimsaidia mtafiti kunukuu data alizokusanya kwa kusoma machapisho na vitabu teule. Kadhalika, vilimwezesha kuhifadhi baadhi ya data za kimsingi kama vipengele vya mwingilianotanzu; nyimbo, barua, insha, maigizo na mengine ambayo yamejadiliwa katika tasnifu. Wakati mwingine, daftari lilitumika kama kifaa cha kuhifadhi na kuchambua data.

## 2.4 Ukusanyaji wa Data

Walliman (2005) anaeleza kuwa ziko mbinu mbili ambazo mtafiti anaweza kuzitumia kwa kukusanya data, nazo ni: Mbinu za kukusanya data nyanjani na mbinu za kukusanya data maktabani. Katika utafiti huu mtafiti alisoma kazi teule maktabani kwa lengo la kuchanganua namna vipengele vya mwingilianotanzu vinaweza kuchimuza maudhui tukiongozwa na nadharia za utafiti. Vitabu teule vilivyosomwa ni: *Mchezo wa Mtelezo na Hadithi Nyingine* (Nandwa, 2016), *Kade na Katana* (Syokau, 2018), *Mchezo wa Kobole* (Momanyi, 2009), *Kito Apepeta* (Nandwa, 2013), *Sitaki Iwe Siri* (Matundura), *Hidaya* (Namlola, 2019), *Msiba wa Kujitakia* (Kea, 2013). Kisha, kilichofuata ni usomaji wa kina maktabani kuhususiana na nadharia za utafiti kutoka vitabu, majarida na machapisho kadha wa kadha katika maktaba na kwa mtandao ili kupata misingi thabiti kuhusu mada ya utafiti. Akiongozwa na malengo na maswali ya utafiti, mtafiti alisoma na kunakili tanzu mahsusi zilizojitokeza katika kila bunilizi na namna tanzu hizo ziliingiliana na kuchimuza maudhui maalum. Baada ya

kusoma bunilizi teule, tanzu mbalimbali za fasihi zinazodhihirika katika vitabu hivi teule zilinakiliwa kwenye tarakilishi. Data iliyonakiliwa ni ile inayohusiana na utafiti wetu. Tanzu zilizonakiliwa ni kama vile, nyimbo ndani ya hadithi, mashairi ndani ya barua, matumizi ya barua ndani ya hadithi na hata maigizo.

### 2.5 Uwasilishaji na Uchanganuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kitendo cha kusimba na kupanga vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti (Bogdan na Biklen, 1992; Taylor na Bogdan, 1984). Uchambuzi wa data ulifanyika kwa kuzingatia maswali ya utafiti na kuwasilishwa kimaelezo. Data iliyokusanywa ili kuunda kiunzi cha uchanganuzi ni tanzu mbalimbali za fasihi simulizi na andishi zinazojitokeza katika vitabu teule, Baadhi ya tanzu ni matumizi ya picha, nyimbo, mashairi, barua na maigizo. Maelezo yakinifu yametolewa kila baada ya nukuu ya data kutokana na vitabu teule kutegemea malengo na nadharia ya utafiti.

### 2.6 Hitimisho

Sura hii imeangazia usuli wa suala la utafiti ambapo dhana mbalimbali imefafanuiwa kwa kina ili kutusaidia kuelewa kinachozungumziwa katika utafiti huu. Aidha, tumeelezea suala la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti yaliyotokana na malengo hayo. Hali kadhalika, sababu za kuchagua mada, upeo na njia za kukusanya data zimeelezwa. Hatimaye, mbinu za utafiti ambapo ukusanyaji wa data, uteuzi wa sampuli, vifaa na uwasilishaji na uchanganuzi wa data za utafiti huu zimefafanuliwa. Sura inayofuata inaangazia mapitio ya maandishi na mkabala wa kinadharia.

# SURA YA TATU

# MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inaangazia baadhi ya maandishi yanayohusiana na mada na suala la utafiti. Kwa ujumla, maandishi ya wataalamu waliotafiti kuhusu mwingilianotanzu kutoka kwa mwingilianomatini yameonyeshwa. Maandishi haya yalituwezesha kujadili na kufafanua jinsi kauli zao zilijenga utafiti wetu. Kwa kuongozwa na kiunzi cha kinadharia, tumechunguza jinsi mawazo yao yanaweza kuoana na mawazo yetu.

Sehemu hii pia inaangazia nadharia zilizotumika katika utafiti wetu. Waasisi wa nadharia hizo na mitazamo yao kuhusiana na suala letu la utafiti imefafanuliwa. Nadharia hizo mbili zilitumika kimwingilianomatini kuyafikia malengo ya utafiti.

## 3.1 Dhana ya Mwingilianomatini

Dhana ya mwingilianomatini (MM) imefasiliwa na wataalamu kadha wa kadha, akiwemo Kristeva (1960), Allen (2000) na Lemaster (2012). Katika ufafanuzi wao, kuna uhusiano wa karibu sana na dhana ya mwingilianotanzu (MT). Kristeva (1960) anaeleza kuwa MM ni kuathiriana, kuhusiana na kutegemeana kwa kazi za fasihi, ambapo matini za kifasihi huingiliana na kuchangizana ili kukamilishana. Anachomaanisha Kristeva ni kwamba kila matini ni matokeo ya mwingiliano wa matini nyingine ambapo matini inaundwa kwa mkusanyiko wa matini nyingine mbalimbali. Anadai kuwa, si rahisi kuzungumzia uasili au upekee wa kazi ya fasihi, kwani kazi yoyote ile ya kifasihi inatokana na kazi zilizotangulia. Hivyo, kuamini kuwa matini ya kifasihi inajitegemea ni kupotoka. Nikojeleva (1996) anakubaliana na kauli hii ya Kristeva (1960) katika uchunguzi wake wa MM katika fasihi ya watoto. Nikojeleva anabaini kuwa maana ya matini humbainikia mtafiti au msomaji kutokana na mwingiliano uliopo kati ya matini zilizotangulia na za kisasa. Dhana hii

ilithibitishwa kwa kulinganisha vitabu kadhaa vya fasihi ya watoto: *Mchezo wa Mtelezo na hadithi Nyingine* (Nandwa, 2016), *Kade na Katana* (Syokau, 2018), *Mchezo wa Kobole* (Momanyi, 2009), *Kito Apepeta* (Nandwa, 2013), *Sitaki Iwe Siri* (Matundura, 2008), *Hidaya* (Namlola, 2019), *Msiba wa Kujitakia* (Kea, 2013).

Allen (2000) anafasili MM kuwa ni kuhusiana na kutegemeana kwa kazi za fasihi. Kutokana na maoni ya Allen, ni wazi kuwa hakuna kazi ya kifasihi ambayo inakamilika bila kutegemea kazi nyingine ya fasihi. Anatoa mfano kuwa, katika utambaji wa hadithi, msimulizi huweza kuingiza nyimbo na hata mafumbo. Fasili ya Allen (keshatajwa) inatufaa kwa vile kuna kuhusiana na kutegemeana kwa tanzu za fasihi katika bunilizi za watoto. Utanzu mmoja hutegemea utanzu mwingine ili kuibua ujumbe uliokusudiwa. Fasili ya dhana ya MM inayotolewa na Allen (keshatajwa) inadhihirisha kuwa dhana ya MM na MT ina uhusiano wa karibu.

Lemaster (2012) anaeleza kuwa, mwingilianomatini katika fasihi, ni pale ambapo kitabu kimoja kinarejelea kitabu kingine katika jina la kitabu, visa na matukio, wahusika na usimuliaji. Vilevile, mwingilianomatini ni pale ambapo matini mbalimbali zinatumiwa ndani ya matini ya kifasihi kama vile, matumizi ya matini za kijamii, wimbo, hadithi za kitamaduni, filamu, maonyesho ya televisheni, na matini za vyombo vya habari. Huu ndio mwelekeo tunaochukua katika utafiti wetu kwamba matini moja hupatikana katika matini nyingine ili kukamilishana.

Kwa upande wa wanafasihi wa Kiswahili, dhana ya MM inajadiliwa na wataalam mbalimbali, kama vile Wamitila (2003, 2008), Senkoro (2011), Herman (2011) na Macha (2013). Wamitila (2008) anaeleza kuwa MM ni kule kuhusiana kwa kazi moja ya fasihi na nyingine zilizotangulia. Anabainisha kuwa, MM huo huweza kuwa katika

dhamira, wahusika au mtindo. Katika utafiti wetu, tunaangalia namna uhusiano huu wa kimtindo unachimuza maudhui katika kazi husika.

Senkoro (2011), anasema kuwa, MM ni kule kutumiwa kwa utanzu mmoja wa fasihi katika kutolea au kuwasilishia utanzu mwingine, mfano wimbo ndani ya ngano au hadithi. Hali kadhalika, MM hurejelea uwepo wa sifa mbalimbali za matini moja au zaidi katika kazi fulani ya fasihi, mfano matumizi ya nyimbo, barua, ngoma, masimulizi ya hadithi, misemo na nahau. Senkoro (2011) anaielezea mbinu ya mwingilianomatini kuwa, ni kule kutumiwa kwa utanzu mmoja wa fasihi katika kutolea au kuwasilisha utanzu mwingine, mfano kuwepo kwa wimbo ndani ya ngano au hadithi.

Utafiti wetu umeegemea sana ufafanuzi wa Senkoro (2011) kwa vile anachokizungumzia ni mwingilianotanzu na wala si mwingilianomatini kwani mwingilianotanzu ni kule kuingiliana kwa vipera vya fasihi. Ufafanuzi huu wa Senkoro una uhusiano mkubwa na utafiti huu kwani tunachunguza namna tanzu katika bunilizi za watoto zinaingiliana. Hakuna utanzu unaosimama kipweke bila kuingiliana na mwingine. Mawazo ya Senkoro (2011) yalitufaa katika kutambua tanzu ambazo zinaingiliana katika bunilizi za watoto pamoja na kuchunguza umuhimu wa mwingiliano huu wa tanzu kwa mtoto Mwafrika.

Macha (2013), anaunga mkono Senkoro kwa kusema kuwa, mwingilianomatini ni ule uwepo wa sifa mbalimbali za matini moja katika kazi fulani ya fasihi, kama vile matumizi ya nyimbo ndani ya hadithi, barua ndani ya hadithi, ngoma ndani ya wimbo, maigizo ndani ya hadithi, mashairi ndani ya barua, nahau, majibizano, vichekesho ndani ya masimulizi, picha na vielelezo vinavyoambatisha masimulizi katika bunilizi

za watoto. Huu ndio mwelekeo wa mwingilianotanzu unaosisitizwa katika utafiti wetu.

Nduye (2015) amejadili dhima za mwingilianomatini katika hadithi za watoto za kabila la Wabena. Baadhi ya dhima hizo ni kuvuta makini za watoto, kuipumzisha au kuiburudisha hadhira, kutambulisha utamaduni, kuliwaza watoto, kuleta uhai wakati wa utendaji, kupitisha taarifa ya jambo fulani na hali kadhalika kupitisha maudhui mbalimbali za hadithi husika. Nduye ameweka bayana maana ya hadithi na kubainisha kuwa ni mojawapo ya dhana au utanzu wa fasihi simulizi ya Kiswahili. Hata hivyo, Nduye amejikita katika kipengele cha hadithi ambapo hadithi ni masimulizi ya kimfululizo. Nduye anasema kwamba hadithi ni mojawapo ya vipera vya fasihi simulizi ambapo wahusika wake huweza kuwa binadamu au viumbe vyovyote vinavyopewa sifa za kibinadamu.

Kuhusiana na dhima ya kubeba maudhui, Nduye (2015) alitaja tu kwamba, hadithi huibua maudhui mbalimbali kama dhamira, ujumbe na mafunzo mbalimbali. Kwamba madhumuni makuu yalikuwa kuwafundisha, kuwaonya na kuwasaidia kupata njia mbalimbali za namna ya kuishi na watu. Utafiti wake ulitufaa kwa kuwa baadhi ya vipera vya fasihi simulizi vinavyodhihirika katika masimulizi ya hadithi pia vilishughulikiwa katika utafiti huu. Licha ya kuwa Nduye (keshatajwa) hakuweza kubainisha maudhui hayo katika fasihi simulizi, utafiti wake ulichangia kazi yetu katika kuangazia uchimuzi wa maudhui katika fasihi bunilizi za watoto. Tofauti kuu iliyopo baina ya kazi ya Nduye na yetu ni kuwa, Nduye (2015) alichunguza hadithi za kabila la Wabena ilhali uchunguzi wetu ulilenga bunilizi za Kiswahili.

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996), fasihi andishi huchota baadhi ya vipengele vyake kutoka kwa fasihi simulizi. Kwa mujibu wa Wananadharia wa Mwingilianomatini,

kuingiliana kwa tanzu au matini ni mbinu inayotumika katika kazi za kifasihi. Akitoa mfano wa kuingiliana kwa kazi za fasihi andishi, hususan hadithi fupi, novela na riwaya, Wamitila (2002) anasema kuwa mwingiliano huo ni wa kawaida kwa sababu kazi hizi hutumia stadi za utunzi zinazofanana.

Erastus (2017) anasema kwamba bunilizi za watoto hujengwa kwa namna ya kumvutia mtoto kwa mtindo wa taharuki. Wahusika wake huwa ni watoto. Katika harakati za kuibua maudhui, matumizi ya wahusika wanyama, mazimwi na majitu hutumika ili kumvutia mtoto. Mawazo ya Erastus yana uhusiano na utafiti huu maana katika kujenga namna ya kumvutia mtoto kiakili, tanzu mbalimbali zilitumika kwa mfano nyimbo ndani ya hadithi, utendaji kwenye michezo ya watoto, hadithi fupi kwenye bunilizi na kadhalika. Tanzu hizo zote huleta uhai katika usimulizi huo wa bunilizi na huteka akili ya mtoto kuzingatia yanayosimuliwa.

Kwa mantiki hii, mwingiliano wa tanzu katika kazi za kifasihi ni nyenzo muhimu sana ya utunzi ila haijachunguzwa kuonyesha namna inachimuza maudhui. Kutokana na mawazo ya wataalam hawa inabainika kwamba bunilizi za watoto kama utanzu mkuu hutumia vipengele mbalimbali vya fasihi simulizi kama nguzo kuu ya utunzi.

### 3.2 Dhana ya Mwingilianotanzu

Mwingilianotanzu kwa upande mwingine hurejelea namna utanzu unavyotagusana na tanzu zingine zote kwa ujumla ili kuboresha uwasilishaji wa ujumbe. Kama anavyosema Mulokozi (1989), hakuna utanzu wowote ule uliojitosheleza ila tanzu huingiliana na matumizi ya tanzu zingine ili kufaulisha uwasilishaji wa ujumbe. Maelezo haya yanaoana na dhana zinazotolewa na wahakiki kama vile, Senkoro (2011), Lemaster (2012) na Macha (2013) wanapojadili dhana ya Mwingilianomatini. Licha ya kuwa mwingilianomatini kama ilivyojadiliwa na Kristeva (1980) huhusisha

kuathiriana kwa kazi za kifasihi zilizotangulia, Mwingilianomatini pia huhusisha kuchopeka kwa tanzu zingine za fasihi kama vile wimbo katika utanzu mwingine tofauti.

Murimi, Obuchi na Kandagor (2016) wanahoji kuwa, mwingilianotanzu katika kazi yoyote ya fasihi husababishwa na mwingilianomatini ambao huiwezesha kazi husika kukopa, kubashiri, kunukuu, kuiga na hata kurejelea tanzu zingine ama katika fani au maudhui bila kuzingatia mipaka dhahania ya utanzu husika. Pia, wanaeleza kuwa, tanzu mbalimbali katika kazi moja ya fasihi huingiliana, huumbana, huchangiana na kisha kujibadilisha na kujigeuza kimaudhui na kifani katika mchakato wa unyambuaji ili kuboresha uwasilishaji wa ujumbe kwa hadhira.

Hoja muhimu inayotokea hapa ni kuwa, mwingilianotanzu ni sehemu ya mwingilianomatini ambayo ni mbinu mojawapo ya kisanaa ya kuwasilisha maudhui katika kazi za kifasihi. Utafiti huu unasaili namna mwingilianotanzu unachimuza maudhui katika bunilizi za watoto zilizoteuliwa. Mwingilianotanzu umewavutia wanafasihi wengi kwa muda mrefu.

Mwingilianotanzu hujengwa kwa kuhusisha mbinu mbalimbali za fasihi ama andishi au simulizi. Mbinu hizi huingiliana na kuhusiana kwa lengo mahsusi. Matumizi ya mbinu kama vile barua ndani ya bunilizi, ushairi ndani ya barua, nyimbo ndani ya maigizo katika hadithi, maigizo katika wimbo kwenye bunilizi, na mashairi ndani ya masimulizi hutumika katika fasihi bunilizi za watoto. Utafiti huu ulichanganua mtindo huu wa uandishi katika kuchimuza maudhui kwenye fasihi bunilizi za watoto.

Tafiti za awali zimedhihirisha mwingilianotanzu katika fasihi simulizi za watoto. Bakize (2014) wakati wa kubainisha dhima ya mwingilianomatini katika hadithi, alitaja tu kwamba, mwingilianotanzu hudokeza maudhui. Utafiti wetu unapiga hatua

zaidi ya Bakize kwa vile maudhui yaliyodokezwa yamechanganuliwa kwa kina kwa kuonyesha namna maudhui hayo huchimuzwa na vipengele vya mwingilianotanzu katika bunilizi teule. Muhimu ni ufaafu wa maudhui hayo kwa mtoto Mwafrika katika mazingira yake asilia.

Wamitila (2008) anajadili kuwa mwingilianotanzu katika kazi moja hutoa nafasi kubwa ya msanii kujieleza barabara. Mwandishi hufanya hivi kwa kujua au kwa kutojua. Dhana ya mwingilianotanzu inaondoa mipaka ya utanzu husika na kuiweka wazi kutazamwa kwa kuzingatia jinsi ilivyojumuisha mitindo na mbinu mbalimbali kwa mfumo uliosukwa taratibu ili kuwasilisha ujumbe wake.

Mwingilianotanzu katika fasihi ni suala linaloonekana la kawaida kwa baadhi ya wataalam. Kwa mfano, Mulokozi (1989) anasema kwamba, mojawapo ya sifa ya fasihi simulizi ni vipera vyake kuingiliana katika utendaji. Mwingilianotanzu huwa na dhima mbalimbali kama anavyobainisha Bakize (2014). Bakize anaeleza kuwa mwingilianotanzu huleta uhai katika utendaji wa fasihi, huchangamsha hadhira, hudokeza maudhui, huvuta usikivu wa hadhira, huwaaminisha watoto kuhusu yanayosimuliwa, hutambulisha utamaduni miongoni mwa mambo mengine. Dhima hizi anazozitaja Bakize (2014) zina umuhimu katika kazi yetu maana tunaangalia jinsi vipengele vya mwingilianotanzu vinachimuza maudhui katika bunilizi za watoto zilizoandikwa.

Katika uwasilishaji wa fasihi simulizi, fanani na hadhira huhitajika kuwepo ndipo kipera husika kiwasilishwe. Hadhira mara nyingi huhusika kikamilifu katika utambaji wa kipera kile. Ili kuweza kuihusisha hadhira kikamilifu, mtambaji huhitajika kutumia mbinu na mitindo kadhaa ili kuiteka hadhira na kukamilisha malengo yake. Katika kutumia mitindo na mbinu tofauti katika kazi ile moja, mwingilianotanzu huibuka.

Mtambaji hujikuta anatumia vipengele kama vile maigizo, nyimbo, semi miongoni mwa tanzu zingine ili kuleta uhai katika masimulizi ya kazi husika. Mwingiliano huu wa tanzu mbalimbali katika bunilizi za watoto ndio uliojadiliwa katika fasihi bunilizi hizo na kuangalia ikiwa mwingiliano huo unamfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake ya kiasili.

Aidha, Maitaria (2003) alifanya utafiti kuhusu matumizi ya methali katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti wa Maitaria ulilenga kuonyesha kuwa, methali kama utanzu wa fasihi simulizi hutumiwa katika mashairi ambao ni utanzu wa fasihi andishi kwa madhumuni ya kusisitiza ujumbe fulani. Aidha, Maitaria anadai kuwa, methali zinaweza kutumiwa kama kigezo mbadala cha kuainisha mashairi andishi ya Kiswahili. Utafiti huo ni mfano wa mwingilianotanzu katika fasihi andishi; ambapo kipengele cha fasihi simulizi kinaibuka katika fasihi andishi ili kukamilisha maudhui na kuufanya utanzu huu kutekeleza wajibu wake barabara. Alivyojadili Maitaria kuhusu matumizi ya methali katika mashairi, ndivyo tumeweza kutambua kwamba mashairi pia hupatikana ndani ya bunilizi za watoto katika lengo la kuibua maudhui. Maudhui hayo kama vile uwajibikaji, dini, magonjwa, maadili na malezi, sala, utamaduni, haki za watoto, bidii na uvivu yanamfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake. Maoni ya Maitaria (2003) yalichochea sana utafiti wetu kwa kutuelekeza katika kuangalia namna tanzu zinaweza kuingiliana ili kuchimuza maudhui katika bunilizi za watoto.

Vievile, Kenguru (2013) alifanya utafiti kuhusu athari za fasihi simulizi katika riwaya akiangazia riwaya ya *Utubora Mkulima.* Katika utafiti wake anahitimisha kuwa fasihi andishi haipo bila fasihi simulizi. Anabainisha kuwa waandishi wengi huchota wahusika, mbinu na maudhui kutokana na fasihi simulizi. Kenguru (2013) alifanya utafiti wake kwa kuegemea uhusiano kati ya fani na maudhui katika vipera hivi vya

fasihi. Matokeo ni kwamba, fasihi andishi huathiriwa sana na tanzu za fasihi simulizi. Maoni ya Kengeru (2013) yanajenga utafiti wetu kwa sababu bunilizi za watoto huathiriwa sana na tanzu zingine za kisanaa ambazo husaidia kuleta uhalisia katika bunilizi za watoto. Tanzu hizo huingiliana kwa lengo la kuchimuza maudhui fulani katika kazi husika.

Kwa upande mwingine, Kobia (2008) alijishughulisha na suala la utendaji katika nyimbo za tohara miongoni mwa Waigembe. Anaendelea kudai kuwa, utendaji ndio uti wa mgongo wa fasihi simulizi. Anadai kuwa, bila utendaji, nyiso haziwezi kutekeleza majukumu yake vizuri. Utafiti huu wa Kobia unakubali kwamba nyiso pia huhitaji utendaji kama mwingilianotanzu ndipo wazo lililolengwa liwasilishwe kwa uwazi zaidi. Hali hii inabaini kwamba nyiso kama kipera cha nyimbo hutekeleza majukumu vyema zikihusishwa na utendaji ambapo utendaji ni kipera cha drama kama inavyoelezwa na Mulokozi (1989). Utafiti wa Kobia (2008) unaafikiana na utafiti wetu kwamba tanzu za fasihi simulizi huingiliana na kutegemea tanzu zingine kama ilivyo katika bunilizi za watoto kwa lengo la kuibua ujumbe unaokusudiwa na mwandishi. Katika kuangalia ujumbe unaoibuliwa basi uamilifu wa maudhui hayo unachunguzwa ili kubaini iwapo yanafaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake asilia.

Wanjala (2015) anahusisha dhana ya mwingilianotanzu na mchakato wa uumbaji na uumbuaji upya wa utanzu. Anasema hii ni hali ambayo huruhusu tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kuvunja mipaka ya kiutanzu na kuchanganyana wakati wa utendaji. Uumbuaji na uumbaji huu wa tanzu hujenga maana kamili ya utanzu mkuu kutokana na tanzu zingine, hivyo kuusaidia utanzu husika kutekeleza wajibu wake. Katika utafiti wetu, wajibu unaotekelezwa unachukuliwa kuwa uchimuzi wa maudhui katika bunilizi za watoto.

Macha (2013) ameshughulikia matumizi ya mtindo wa mwingilianomatini kwenye tendi. Alikusudia kutambua iwapo tendi za Kiswahili huwa na Mwingilianomatini na kubainisha vipengele vinavyoingiliana katika utanzu wa tendi na dhima yake. Mfano, matumizi ya picha na michoro kwenye tendi husaidia kufanya matukio yaweze kueleweka kwa urahisi pale ambapo hayakueleweka vizuri. Aidha, yamepelekea kuleta uhalisia wa matukio na visa hivyo kwa hadhira na jamii nzima. Tofauti na utafiti wetu, Macha alishughulikia utanzu wa tendi katika utafiti wake ilhali utafiti huu umejikita katika kushughulikia mwingilianotanzu katika fasihi bunilizi za watoto.

Mawazo ya Macha yana uhusiano mkubwa na utafiti wetu kwa sababu kipengele cha picha ni mojawapo ya vipengele vya kimwingilianotanzu katika bunilizi za watoto. Picha na michoro katika bunilizi za watoto huonyesha uhalisia wa jambo linalosimuliwa na linaloendelea. Pia husaidia kueleza zaidi kile kinachozungumziwa katika kazi husika kwani huwa na mahusiano ya moja kwa moja na kile anachoeleza mwandishi au mtunzi kupitia wahusika mbalimbali. Matumizi ya picha katika bunilizi za watoto zilizochunguzwa yamechangia kuchimuza maudhui na uhalisia wa mazingira ya mtoto Mwafrika.

Kutokana na utafiti wa wataalamu hawa waliotajwa hapo juu, inabainika kuwa, dhana ya mwingilianotanzu haiwezi kuelezeka kivyake bila ya kuhusisha dhana ya mwingilianomatini. Maelezo haya vilevile, yanatoa mwanga wa utafiti huu kuwa, fasihi ya watoto kama ilivyo fasihi nyingineyo, haiwezi kujikamilisha ikiwa pweke. Inahitaji kuingiliana na vipera vingine vya fasihi ili kuweza kuwasilisha ujumbe wake kikamilifu.

### 3.3 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; Nadharia ya Mwingilianomatini na Nadharia ya Uoniafrika. Nadharia ya Mwingilianomatini ilitufaa katika uchanganuzi wa mwingilianotanzu katika bunilizi za watoto. Nadharia ya Uoniafrika ulifaa katika kutathmini vipengele vinavyoingiliana na kuchimuza maudhui yanayomfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake ya asili au la. Katika sehemu ifuatayo, nafasi ya Nadharia ya mwingilianomatini katika utafiti huu imeshughulikiwa.

#### 3.3.1 Nadharia ya Mwingilianomatini

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya MM na Nadharia ya UA. Nadharia ya MM iliasisiwa na Mwanasemiotiki wa Kifaransa, Kristeva (1960) na kuendelezwa na wataalam wa baadaye kama Senkoro (2011) na Macha (2013). Kristeva (1960) aliizua nadharia hii ya MM kutokana na mawazo ya Mrusi Mikhail Bakhtin (1975) katika Nadharia ya Usemezano. Bakhtin katika nadharia hiyo ya Usemezano, anaamini kuwa kazi ya fasihi ina sauti mbalimbali zinazoingiliana na kupiga mwangwi katika kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo au zitakazokuja baadaye. Hii ina maana kuwa, athari ya kazi moja huweza kuonekana katika kazi nyingine zilizotangulia, zilizopo na hata zijazo.

Kristeva (1960) aliyaendeleza na kuyapanua mawazo ya Bakhtin na kuibua nadharia yake ya MM. Kwa mujibu wa Kristeva, hakuna matini yoyote inayoweza kuangaliwa peke yake, kwa upekee wake na kwa kujitegemea, bali ni lazima kutakuwa na matini nyingine iliyotangulia ambayo inahusiana na matini hiyo mpya.

Hii ina maana kuwa, kuna uhusiano na kutegemeana kwa kazi za fasihi, na kwa maana hiyo, si rahisi kuzungumzia uasilia au upekee wa kazi ya fasihi, kwani kwa

vyovyote vile itakuwa inatokana na kazi za fasihi zilizotangulia au zilizopo na zitakazokuja kwa mitindo ya kiuashiriaji.

Kristeva (1960) anaitazama dhana ya MM kama jumla ya maarifa na mbinu inayofanya matini kuwa na maana. Maana ya matini huangaliwa kama inayotegemea matini nyingine katika kile Macha, (2013) anakiita mwanda wa kimwingilianomatini. Kwa mujibu wa Kristeva (1960), matini yoyote ile huchukua au hufaidi kutokana na matini nyingine pamoja na kuziumbua katika mwanda huo wa kimwingilianomatini. Mawazo haya pia yameshikiliwa na Senkoro (2011), ambaye anaeleza kuwa MM ni kule kutumiwa kwa utanzu mmoja wa fasihi katika kutolea au kuwasilishia utanzu mwingine, mfano wimbo ndani ya ngano au hadithi. Hali kadhalika, kuna uwezekano wa kuwepo sifa mbalimbali za utanzu mmoja au zaidi katika kazi fulani ya fasihi: Mfano mzuri ni katika matumizi ya nyimbo ndani ya hadithi, mashairi ndani ya barua, ngoma ndani ya maigizo, maigizo ndani ya hadithi, na hata michoro au vielelezo katika kazi bunilizi.

Kwa hivyo, kutokana na mawazo ya Kristeva (1960), wamitila (2008), Lemaster (2012), Allen (2000), Nikojeleva (1996), Macha, (2013) na senkoro (2011), tunapata mihimili ifuatayo:

1. Matini zote zilizoandikwa hurejelea matini zilizotangulia.
2. Kazi yoyote ya fasihi husheheni sifa mbalimbali za matini zilizotangulia.
3. Katika uandishi wa kazi za kifasihi, mwandishi huathiriwa sana na kazi tangulizi maana uandishi wowote ni kioo cha kazi tangulizi.
4. Mbinu ya mwingilianomatini ni kule kutumiwa kwa utanzu mmoja wa fasihi katika kutolea au kuwasilisha utanzu mwingine.

Utafiti huu umeegemea sana mhimili wa nne kwamba katika kazi za fasihi ikiwemo bunilizi za watoto, utanzu mmoja hutumika katika kuwasilisha utanzu mwingine. Yaani, kazi za kifasihi husheheni tanzu zingine ambazo huzifanya zikamilike kifani na kimaudhui (Senkoro, 2011 na Macha, 2013)

### 3.3.2 Nadharia ya Uoniafrika

Nadharia ya Uoniafrika iliibuka baada ya nchi nyingi za Afrika kupata uhuru. Nadharia hii ilikita mzizi mwaka wa 1960 kutokana na Waafrika wengi, katika sehemu mbalimbali za dunia kuona kwamba, Mwafrika alikuwa anarejelewa kutoka pembeni. Mwafrika alikuwa anabezwa na mara nyingi akitathminiwa kwa kutumia vigezo vya wazungu. Ndiyo maana mambo mengi ya Waafrika yalikuwa yanabezwa. Mwasisi wa Nadharia hii ni  Asante (1960). Mtaalam huyu anasema kwamba UA ni wazo ambalo matarajio, matamanio na mwelekeo wa Mwafrika huwekwa katikati kuhusiana na masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hoja kubwa ya Nadharia ya Uoniafrika ni kumtazama na kumtathmini Mwafrika kwa kuzingatia historia yake na akiwa kwenye kiini cha utamaduni wake.

Dhana ya UA ni kule kuhamisha fikra iliyopendekezwa kama urekebishaji wa uumbaji wa mawazo au fikra kuhusu mtazamo wa mtu Mwafrika (mweusi) kutohusishwa na kutowekwa katikati. Hapa Asante (1960) anajaribu kuleta mtazamo mpya kwa Waafrika kuhusiana na mazingira, ruwaza za kikoo au ujamaa, mahusiano kati yao, aina zao za dini na marejeleo ya kihistoria. Uchambuzi wowote unaojikita katika utamaduni wa Kiafrika, uwe ni wa kifasihi au kiuchumi, uwe ni wa kisiasa au kiutamaduni, lazima ujali mtazamo unaojikita katika historia na utamaduni wa Mwafrika mwenyewe (Asante, 1998; 2003; Okafor, 2010).

Uoniafrika kimsingi hurejelea hali ya Waafrika asilia pamoja na matamanio yake kulingana na tamaduni za Kiafrika kutabuliwa na kuwekwa katikati. Achebe (1976) na Chinweizu (1987) wanafafanua kwamba mwandishi wa Kiafrika anatakiwa kuwa kama mwalimu wa jamii ambaye anapaswa kuifundisha jamii kuhusu historia na utamaduni wake ili kuimarisha utamaduni wa jamii husika. Jukumu muhimu la mwandishi ni kuikosoa jamii hata kama jamii hiyo itamgeuka. Hivyo basi, kazi kubwa ya mwandishi ni kusimamia ukweli wa mambo ili kuibadilisha jamii (Achebe, 1976, 1990). Hata hivyo, jamii hii itabadilishwa tu ikiwa mambo yanayozungumziwa katika kazi husika yanahusu mazingira anayoelewa msomaji.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Uoniafrika, tunachunguza ikiwa fasihi bunilizi za watoto zinamfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake asilia. Je, mwingiliano wa tanzu mbalimbali zinamfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake? Hali kadhalika, maudhui yanayoendelezwa na mwingiliano huo umemweka katikati mtoto Mwafrika kimaslahi? Kulingana na Chawane (1954), mtazamo wa Asante (1960) kuhusu UA unapendekeza kwamba mtu mweusi lazima aangalie maarifa au mawazo kwa mtazamo wa Mwafrika. Masuala yote yasipoangaliwa kwa mtazamo huo wa Kiafrika itakuwa ni kukosea ama kutohusishwa kwa  Mwafrika kwa masuala yanayomhusu. Kwa hivyo, katika kuchunguza fasihi bunilizi za watoto, tulizingatia watunzi ambao wamejikita katika mazingira ya Waafrika wakiwalenga watoto Waafrika.

Chike (2015) anasema kwamba, tangu kuanzishwa kwa Nadharia hii ya UA mwaka wa 1960, imekuwa ni nadharia inayokataa aina yoyote ya ubaguzi wa watu Waafrika. Imeweka kati tamaduni za Waafrika na kukuza Waafrika kama watu wenye thamani. Robert (1994) anasema kwamba, lengo kuu la UA ni kuhimiza mataifa ya watu weusi yasiwe na kiburi cha kikabila ili kuondoa madhara ya tamaduni za ubaguzi wa rangi.

Hata hivyo, kwa kufuata mkondo wa nadharia hii, fasihi ya Kiafrika ina jukumu kubwa la kubadilisha bunilizi za watoto zimfae mtoto Mwafrika katika mazingira yake. Mwandishi anapaswa kujikita katika uandishi unaolenga mtoto Mwafrika. Mtoto Mwafrika asilia hapa kulingana na Disasa (1988), ana baadhi ya sifa hizi; ukuaji wa mapema wa nidhamu, tamaa ya kupata masomo, heshima ya zana za utamaduni, hali ya kutaka kujijua mapema, uhusiano na utegemezi wa pamoja. Sifa hizi zinamzunguka mtoto Mwafrika. Kwa hivyo, waandishi wa fasihi bunilizi za watoto hawana budi kuhusisha mtoto huyu katika kazi zao ili mtoto aweze kufaidika kutokana na kazi hizo.

Nadharia hii ina mikondo mingi ya mitazamo. Hata hivyo, kwa kujikita kwa mtazamo wa Asante (1980) utafiti wetu uliegemea kwenye mhimili mkuu ambao ni kumweka katikati Mwafrika kiutamaduni na kimazingira. Basi uandishi na uchambuzi wowote wa bunilizi za watoto lazima ujikite katika utamaduni wa Kiafrika na lazima ujali mtazamo unaojikita katika historia na utamaduni wa mtoto Mwafrika. Nadharia hii ilifaa utafiti huu katika kuchunguza ikiwa tanzu zinazoingiliana na maudhui yanayochimuzwa na mwingiliano huo katika bunilizi za watoto zinamfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake.

Nadharia mbili zimetumika kwa sababu nadharia ya MM inaangalia tu tanzu zinazoingiliana. Hivyo basi, nadharia ya pili ambayo ni ya Uoniafrika imetumika ili kutathmini ikiwa tanzu zinazoingiliana kwenye bunilizi zinamfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake na iwapo maudhui yanayochimuzwa na mwingiliano wa tanzu mbalimbali zinamlenga mtoto Mwafrika. Nadharia hii imetumika ili kutiiza lengo la tatu katika utafiti wetu,

### 3.4 Hitimisho

Sura hii imepitia na kujadili machapishso yanayohusu mada ya utafiti na misingi ya nadharia ya utafiti. Tumerejelea maandishi yaliyohusiana na mwingilianomatini na vilevile mwigilianotanzu hasa katika kuonyesha jinsi tanzu katika bunilizi za watoto zilivyoingiliana na kutegemeana. Hali kadhalika, nadharia zilizotumika zimeelezwa kwa kina namna nadharia hizo zina uhusiano mkubwa katika utafiti huu. Nadharia ya Mwingilianomatini imefafanuliwa kwa kurejelea mawazo ya wataalamu mbalimbali kuhusu nadharia hiyo na mihimili ya wataalam wa baadaye walioendeleza nadharia hiyo kama akina senkoro (2011) na Macha (2013). Mawazo ya Senkoro (keshatajwa) ndiyo nguzo na mwongozo katika utafiti huu na iliyotuongoza kutimiza lengo na kujibu swali la kwanza katika utafiti huu. Nadharia ya Uoniafrika pia imefafanuliwa kwa kurejelea mawazo ya wataalamu mbalimbali. Nadharia hiyo ilituongoza katika kushughulikia lengo la pili na la tatu mtawalia. Sura inayofuata ni upambanuzi wa vipengele vya mwingilianotanzu katika bunilizi za watoto.

# SURA YA NNE

# TANZU MAHUSUSI ZINAZOJENGA BUNILIZI TEULE ZA WATOTO

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inachambua data zilizokusanywa kutoka bunilizi teule; *Sitaki Iwe Siri* (Matundura, 2008), *Mchezo wa Kobole* (Momanyi, 2009), *Kito Apepeta* (Nandwa, 2013), *Mchezo wa Mtelezo* (Nandwa, 2016), *Hidaya* (Namlola, 2019), *Msiba wa kujitakia* (Kea), *Kade na Katana*, (Syokau, 2018). Bunilizi hizi teule za watoto zinajipambanua kama tungo za kinathari. Hii ni kwa sababu zinasheheni maelezo ya kiutondoti juu ya matukio yanayosimuliwa. Wamitila (2004:188) anabainisha tungo za kinathari katika fasihi andishi kama; Hadithi fupi, tamthilia, riwaya, wasifu, tawasifu na insha. Bunilizi teule ni tungo za riwaya inayojitokeza kama hadithi za kiutondoti za watoto. Bunilizi hizi ni masimulizi ya kinathari ambayo tanzu mbalimbali hujitokeza ndani mwake katika kujenga ujumbe uliomo. Data zinazowasilishwa hapa zinahusiana na lengo la kwanza: lengo ambalo ni kupambanua namna tanzu mahsusi zinajenga bunilizi teule za watoto. Katika sura hii, tunapambanua tanzu mahsusi zinazojitokeza kama vile nyimbo, maigizo, mashairi, ndoto, matumizi ya hekaya, barua, sala, insha, maigizo na michezo ya watoto na matumizi ya picha. Upambanuzi huu ni katika bunilizi za watoto wa daraja la tatu yaani darasa la nne hadi nane katika mfumo wa 8-4-4 wa elimu nchini Kenya. Kila kitanzu kimejadiliwa kiufafanuzi huku mifano halisi ikitolewa kutokana na bunilizi husika. Hata hivyo, kabla ya upambanuzi huo, muhtasari wa bunilizi husika umetolewa.

## 4.1 Muhtasari wa Bunilizi Husika

Katika sehemu hii, tumeangalia muhtasari wa kila bunilizi pamoja na kuonyesha baadhi ya vipengele vya kimwingilianotanzu na baadhi ya maudhui yanayochimuzwa

na vipengele hivyo. Bunilizi hizo ni *Sitaki iwe Siri* (Matundura, 2008), *Mchezo wa Mtelezo* (Nandwa 2013), *Hidaya* (Namlola 2019), *Kito Apepeta* (Nandwa 2013), *Mchezo wa Kobole* (Momanyi 2009), *Kade na Katana* (Syokau 2018) na *Msiba wa kujitakia* (Kea 2013).

### 4.1.1 *Sitaki iwe Siri* (Bitugi Matundura, 2008)

Bunilizi hii ni hadithi ya kinathari inayosimulia hadithi kuhusu Musa, mvulana wa darasa la sita aliyeshangazwa kuwa yeye pamoja na dada zake wawili, Haki na Ukwa ni mayatima. Chanzo cha uyatima ni siri kubwa na nyanya Mwalongo hataki kuwafichulia wajukuu zake kiini cha vifo vya wazazi wao.

Musa anapopata fursa ya kuandika insha kuhusu UKIMWI, anaamua kuumwaga mtama. Janga la Ukimwi linakuwa si siri tena; japo liliwatia uyatimani. Musa, Haki na Ukwa wanakuwa mifano bora ya kueneza ukweli kuhusu UKIMWI. Kitabu hiki ni bunilizi ya kinathari kilichojaa vipengele vya kimwingilianotanzu. Vipengele hivyo ni barua, matumizi ya sala, insha na picha. Vipengele hivi vimetumiwa ili kuibua maudhui ya dini, umaskini, bidii kazini na hata magonjwa.

### 4.1.2 *Kito Apepeta* (Rebeca Nandwa, 2013)

*Kito Apepeta* ni bunilizi ya kinathari inayosimulia kuhusu Kito, msichana mdogo wa shule ya msingi aliyekuwa na kipawa cha kuimba. Kila alipopata nafasi, alikuza kipawa hicho cha uimbaji. Mwalimu alipomtafuta mwanafunzi ambaye angemtumbuiza mgeni mkuu, wanafunzi wangemchagua Kito.

Vipengele vya mwingilianotanzu katika bunilizi hii ni matumizi ya wimbo na picha. Maudhui makuu yaliyochimuzwa na vipengele hivyo ni dini, utamaduni, ushirikiano na uzalendo.

### 4.1.3 *Kade na Katana* (Caroline Syokau, 2018)

Bunilizi ya *Kade na Katana* ni hadithi ndani ya hadithi. Nyanya anawahadithia wajukuu wake kuhusu ndugu wawili, Kade na Katana ambao ni vijana walioishi katika kijiji cha Wema. Kade na Katana walikuwa maskini hohe hahe kutokana na wazazi wao wakongwe ambao hawakuwa na riziki. Vijana hao walikuwa wanafanana kama shilingi kwa ya pili ingawa walikuwa tofauti kitabia na mienendo. Katana alikuwa maskini wa mali lakini tajiri wa maadili mema na mpenda watu. Kade naye alikuwa mtundu na mzembe. Katana alipendwa na kuheshimiwa na wanakijiji kutokana na bidii yake ilhali Kade aliishia kuhangaika kutokana na kujiinua na kumsaliti nduguye.

Katika bunilizi hii, tumepata mwingiliano wa tanzu kama vile; barua, mazungumzo, ndoto na matumizi ya hekaya ndani ya hadithi. Vipengele hivi vimechimuza maudhui ya umaskini, ushujaa, utamaduni, ushirikiano, malezi, haki za watoto na pia bidii kazini.

### 4.1.4 *Mchezo wa Kobole* (Clara Momanyi, 2009)

*Mchezo wa Kobole* ni bunilizi ya kinathari inayohusu mchezo uliochezwa na wanafunzi wa shule ya Vikwatani. Mchezo huu haukufahamika hata na walimu kwa sababu wanafunzi walipoulizwa kuhusu mchezo wenyewe, walitoa maelezo tofauti tofauti kwa sababu waliuweka kuwa siri kwa walimu. Shule hii ilijulikana sana kwa matokeo mazuri ya mitihani ya kitaifa. Kila mwaka wanafunzi wa darasa la nane waliwafurahisha wanakijiji wa Vikwatani kutokana na matokeo hayo mazuri. Muda haukuwa mrefu, matokeo ya wanafunzi yakaanza kudidimia. Hii ni baada ya tajiri mmoja, Bw. Manoti kunyakua uwanja wa watoto wa kuchezea na kuanza ujenzi wa kiwanda cha matunda. Waliofanya kazi katika kiwanda kile hawakujulikana na wenyeji, ila walisafirishwa tu kazini asubuhi na kurudishwa jioni.

Wafanyakazi wale hawakunena na mtu na lango la kiwanda kile lililindwa na bawabu kwa ukali sana. Baadaye, mwalimu mkuu aligundua kwamba chanzo cha kufeli kwa wanafunzi katika mitihani ni Bw Manoti kuajiri watoto wa shule kwa malipo ya kobole. Watoto wa shule hiyo walifanyishwa kazi ya sulubu. Bw Manoti alimwajiri mwanafunzi mmoja aliyewauzia wanafunzi matunda na peremende katika kibanda cha pekee kilichojengwa karibu na shule. Hiki ndicho kiini cha anwani ya kitabu hiki kuitwa Mchezo wa Kobole. Hii ni bunilizi ya kinathari iliyojengwa na tanzu kadhaa zinazoingiliana kwa lengo la kuchimuza maudhui. Bunilizi hii inajumuisha tanzu kama wimbo, michezo ya watoto na matumizi ya picha. Maudhui yanayochimuzwa ni ufisadi, haki za watoto na ushirikiano.

### 4.1.5 *Hidaya* (Juma Namlola, 2019)

Bunilizi ya Hidaya inasimulia kisa kinachohusu msichana kwa jina Hidaya. Msichana huyu alikuwa mwerevu darasani, mpole, mwenye bidii na aliyetilia maanani masomo yake kuliko kitu chochote. Wanafunzi wenzake katika shule ya msingi ya Tumaini walimpenda sana na mara nyingi walimzunguka wakitaka rai zake kuhusiana na mambo waliyokuwa wamesomeshwa darasani. Hidaya ni msichana aliyekuwa na ndoto ya kuwa daktari pindi akikamilisha masomo yake. Hata hivyo, ndoto zake zilielekea kuvurugwa na babake \Bwana Matata alipotaka kumwoza binti huyu kwa rafiki yake kwa jina Bwana Mapesa.

Kesi yake ilipofikia mwalimu mkuu Bwana Maarifa, mwalimu huyo pamoja na mwalimu wa darasa alichukua hatua za kisheria na wakaweza kumwepusha Hidaya na ndoa ya mapema. Hapo ndipo Hidaya akaweza kuendeleza masomo yake na kutimiza ndoto zake. Kitabu hiki cha *Hidaya* ni bunilizi ya kinathari kama tanzu kuu na inajumuisha vipengele vya mwingilianotanzu kama vile shairi, wimbo na matumizi ya

picha. Vipengele hivi vimeibua maudhui kama ushujaa, umaskini, malezi, haki za watoto na suala la bidii na uvivu kazini.

### 4.1.6 *Mchezo wa Mtelezo* (Rebeca Nandwa, 2016)

Mchezo wa Mtelezo ni bunilizi inayosimulia kisa kimoja kinachohusu vijana wawili (Brayo na Lulu) waliokataa kutii maagizo ya mwalimu mkuu kuhusu kutoshiriki mchezo wa mtelezo katika bonde la mauti. Vijana hawa wanapotumwa na mwalimu mkuu waende nyumbani wawaite wazazi wao kwa shughuli rasmi ya shuleni, wanaamua kwenda kushiriki mchezo ule wa mtelezo katika bonde la mauti ambako wanaishia kuumia. Mwalimu mkuu anatumia fursa hii kuwajuza na kuelezea kiini cha yeye kutembea akichechemea iliyotokana na kutotii wazazi wake alipokuwa mdogo. Maudhui makuu katika bunilizi hii ni utiifu. Mengine ni uzalendo na sala. Kitabu hiki ni bunilizi ya kinathari na inajumuisha tanzu kama vile wimbo, matumizi ya picha, hadithi ndani ya hadithi na barua.

### 4.1.7 *Msiba wa Kujitakia* (Pauline Kea, 2013)

Bunilizi hii inasimulia kisa cha mzee Katana aliyejawa na wivu dhidi ya jirani yake. Alitaka kulipiza kisasi kwa zingizio la kumwua babake. Anamtuma mtoto wake kutia sumu katika mtungi wa maji na kwa bahati mbaya, mkewe Katana anaishia kunywa sumu hiyo alipopitia kwa jirani huyo kutoka kliniki. Hatimaye, mkewe Katana alishikwa na ugonjwa wa 'Kuruka'

Bunilizi hii inajumuisha mashairi, hadithi ndani ya hadithi, matumizi ya picha na hali kadhalika matumizi ya nyimbo. Maudhui yanayochimuzwa na tanzu hizi ni magonjwa, ushirikina, malezi na haki za watoto pamoja na ujirani mwema.

## 4.2 Wimbo

Wimbo ni utanzu unaowasilishwa kwa kutumia sauti na mahadhi ya kimelodia yenye mapigo ya kimuziki (Method, 2015). Mbali na sauti ya kuimbika, nyimbo huweza pia kuwasilishwa kwa kutumia sauti ya kughani. Sauti ya kughani kwa kawaida huwa kati ya sauti ya kuimba na kuongea. Nyimbo ni za aina mbalimbali kutegemea kigezo cha uainishaji kilichotumika. Uainishaji huweza kufanywa kidhima, kimaudhui, kifanani au kihadhira, kimuktadha na kadhalika.

Mulokozi (1996) anasema kuwa, wimbo ni kile kinachoimbwa. Anaendelea kufafanua kwamba mambo muhimu katika wimbo ni muziki wa sauti ya mwimbaji au waimbaji, muziki wa ala kama zipo, matini au maneno yanayoimbwa, muktadha unaofungamana na wimbo huo kama vile sherehe, ibada, mazishi, vita na kadhalika. Kamusi ya Karne ya 21 (Longhorn na BAKITA, 2019) inaeleza kuwa wimbo ni maneno na sauti zilizopangwa kama vile ngoma ambazo huwa ni muziki.

Uchunguzi uliofanywa juu ya nyimbo umeonyesha kuwa nyimbo ni kipengele muhimu sana katika jamii zote ulimwenguni. Nyimbo ni tanzu zilizothaminiwa sana na zilitawala katika mifumo yote ya kijamii (Brandel, 1959). Akuno (1999) anasema kuwa muziki ni zaidi ya sauti tu ambazo huimbwa na kuchezwa. Muziki sio wazo la dhana fulani bali ni tajriba; ni tukio ambalo huwasilisha mambo mbalimbali yenye umuhimu katika jamii husika. Akuno anaona nyimbo/muziki ukiwa na uamali wa kiunjozi: Kwanza ni kama kiburudisho, huendeleza uhusiano wa mtu binafsi, humstarehesha na kumwezesha mtu huyu kuwasilisha hisia zake. Nyimbo katika bunilizi za watoto vilevile, huainishwa kidhima, kimaudhui na kadhalika ingawa mara nyingi, nyimbo za watoto ni za burudani tu.

Nyimbo za watoto ni utanzu wa fasihi simulizi ambao unapendwa sana na watoto na hata jamii nzima. Mrikaria (2015) anasema kwamba kipengele hiki cha nyimbo za watoto kina majukumu yenye mielekeo muhimu ya kujenga mahusiano miongoni mwa watoto na kwa jamii nzima. Watoto huhusiana kwa njia mbalimbali na kinachowaunganisha zaidi ni nyimbo zao hasa za kitoto zinazoimbwa wanapocheza katika ulimwengu wao.

Nyimbo zote zinazopatikana katika bunilizi za watoto ni nyimbo za watoto. Hii ni kwa sababu bunilizi za watoto zinadhamiriwa kusomwa na watoto au kuandikwa kwa ajili ya kusomwa na watoto.Nyimbo hizi zimekuwepo tangu jadi katika jamii za Kiafrika hasa nchini Kenya, ingawa zingine zimesahaulika, zinakufa na nyingine zinaibuka (Mrikaria, 2015). Jamii nyingi za Kiafrika zina nyimbo zao za watoto. Hata hivyo, baadhi ya nyimbo hizi huibuliwa katika ule utangamano wa watoto kwa watoto pamoja na baadhi ya wanajamii katika sherehe mbalimbali au shughuli zao za kila siku.

Kinoti (2008) anaeleza kuwa nyimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya kuvutia kwa mahadhi ya kupendeza. Anaendelea kufafanua kuwa kuna aina za nyimbo kama vile za kuzaliwa kwa mtoto, kuongoa, watoto wachezapo, tohara, mapenzi, harusi, kazi, matanga na nyinginezo. Wamitila (2003) anafafanua kwamba wimbo ni tungo zenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Tungo hizi huundwa kwa njia ya mkato, picha na mapigo ya silabi. Hata hivyo, nyimbo za watoto ni nyimbo zinazoimbwa na watoto katika ulimwengu wao wa michezo katika mazingira wanayofahamu wao wenyewe. Umuhimu wa utanzu huu ni kwamba, unasheheni maudhui mbalimbali na hivyo utafiti huu unajadili maudhui yanayochimuzwa na utanzu huu katika bunilizi teule za watoto.

### 4.2.1 Wimbo ndani ya simulizi

Waandishi wa bunilizi za watoto wanatumia mbinu hii ya nyimbo wakiwa na lengo sawa; kuvuta makini ya mtoto, kufurahisha na kuweka mtoto katika ulimwengu wake halisi ( Bakize, 2014) Wimbo huangazia maisha halisi ya mtoto katika jamii husika, fikra na shughuli zao. Wimbo huundwa kutokana na mazingira halisi ya jamii husika na hata shughuli zao (Simala, 2006). Hii inamaanisha ya kwamba nyimbo hizi za watoto hutokana na mazingira maalum wanamokulia watoto. Hata hivyo, nyimbo za watoto hazina mipaka kwa sababu nyimbo hizo pindi tu zinapobuniwa, watoto huzisambaza kwa njia moja au nyingine katika ile michezo yao.

Adwar (2009) anasisitiza kwamba kazi ya sanaa, iwe hadithi au wimbo, lazima iwe na thamani kuu ya kutumbuiza hadhira. Anadai kuwa nyimbo hizi humsaidia msomaji au msikilizaji kusikiliza au kusoma simulizi bila kuchoka. Jambo linalodhihirika hapa ni kuwa nyimbo hizi huburudisha, hufurahisha na kumchangamsha mwanafunzi na kupunguza uchovu wa kiakili (Wamalwa na mwenzake, 2018). Adwar (keshatajwa) anasisitiza kuwa nyimbo hujihusisha zaidi na vionjo vya kimwili na kiakili. Kwa hivyo, matumizi ya nyimbo katika bunilizi za watoto yanarahisisha kazi ya kuelimisha kwani kwa njia hii, mtoto anaweza kubwia anayofunzwa bila kulemewa kwa sababu anaburudika.

Asilimia kubwa ya nyimbo za watoto huambatana na vitendo. Vitendo ndivyo hufanya nyimbo hizo kupata uhai na utamu unaotarajiwa na mtoto. Waandishi wa bunilizi za watoto huweza kutumia nyimbo kidhima. Kulingana na Method (2015), wimbo huweza kuwa na dhima ya kutumbuiza. Tumbuizo ni nyimbo ambazo lengo lake ni kuleta burudani au kutumbuiza na kuondoa au kupoza madhila yaliyopo. Kwa mfano, katika bunilizi ya Rebecca Nandwa (2016) *Mchezo wa Mtelezo na Hadithi Nyingine*, msimulizi anatueleza jinsi mchezo wa mtelezo ulivyoandaliwa kwa minajili

ya kutumbuiza maafisa wa afya na wageni waliokuwa shuleni mwao. Mchezo huu ni wa timu mbili ambapo "kila timu ilikuwa na wasichana watano na wavulana watano" (uk. 22). Viongozi wa timu hizo wakawa Mato na Lulu waliosimamia mbele. Mashabiki walisimama pande za timu zao. Nyimbo zilisikika kutoka kwa mashabiki wa upande wa Lulu;

**1.** Lulu eee! Lulu aaa! Kina Lulu huree!
Kwa nguvu wavuteni, mbiombio wateleze
Waangukiane, wabingirike, ushindi tuutwae
wa mtelezo,hatujapata mfanowe.

Wimbo huu ulioimbwa na mashabiki wa akina Lulu unawahimiza kina Lulu wavute kamba kwa nguvu ili wapinzani wao waweze kuteleza mbio mbio. Wimbo unaendelea kusema kwamba wakishateleza, basi wapinzani wale wangeanguka na kubingirika na hapo wangeibuka washindi wa mchezo ule wa mtelezo, mchezo ambao haukuwa na mfano.

Mashabiki kwa upande wa Mato hawakubaki nyuma asilani. Nao waliimba nyimbo za kushangilia timu yao;

**2.** Mato wetu! Mato wetu! Kina Mato hoyeee!
Vuteni msibabaishwe, kelele zao ni za chura
Leo ni leo wataona, kwa nini matata
Utamu wa mtelezo, ni tuzo kuishinda…uk. 23

Wimbo huu uliwahimiza kina Mato wavute kamba bila kubabaishwa na kelele za wapinzani wao. Kelele za mashabiki wa wapinzani wao zilikuwa kama za chura, yaani hazikuwa na tisho lolote. Anaeleza kuwa, siku hiyo ilikuwa siku yao ya ushindi na wangefurahia utamu wa ushindi wa mchezo huo wa mtelezo.

Nyimbo hizi ziliimbwa hadi wakati washindi walishinda "Timu ya Mato ilijitahidi lakini wapi! Olewao! Wote walifagiliwa hadi upande wa Lulu, ambapo nyimbo za ushindi ziliimbwa na mashabiki wakibeba Lulu hobelahobela" (uk. 23).

**3.** Huree! Kina Lulu huree!
Vumbi tumewatifuliatifulia,
Sakafu waairambaramba!
Utamu wa mtelezo, ni tuzo kujishindia

Wimbo huu ulikuwa wa kushangilia washindi. Walioshinda ni timu ya kina Lulu. Wanasema waliwativua vumbi wapinzani wao. Kwamba, wameirambaramba sakafu na kwamba utamu wa mchezo wa mtelezo ni kujishindia tuzo.

Kimsingi, nyimbo hizi ni za kufurahisha na kuchangamsha watoto kwa sababu zinahusisha viungo vya mwili. Hali kadhalika, wimbo huu ulikuwa ni wa kutia moyo wanaohusika kwenye mchezo. Hata hivyo, mwandishi anatuarifu kwamba mchezo huu ulidhamiriwa kuleta funzo kwamba ingawa mchezo wenyewe ulianza "kuwa sehemu ya kila sherehe zilizowahusisha watoto, hawakuwa wakipaswa kusahau mtelezo katika bonde la mauti. Maudhui yanayochimuzwa hapa ni ushirikiano na suala la utiifu kwa watu wakubwa katika jamii.

Nandwa, (2013), katika kitabu chake *Kito Apepeta* anaeleza ya kwamba, wanafunzi wa darasa la nne walikuwa wameandaa wimbo kwa ajili ya kumtumbuiza mgeni wa heshima Bwana Benja Magonji. "Tuko tayari kuwatumbuiza kwa wimbo unaoitwa 'Apepetanga'…..walipoinuka, Kito alianza kuuimba wimbo:

**4.** *Mwana wa mama apepetanga*
*Mwana wa mama apepetanga*
*Yatsiayo, Yarulayo*
*Yaboola mama njonyi bilenje*

**(Tasfiri)**
Mtoto wa mama anazunguka
Alienda huku, huko na kule
Alirudi nyumbani na kumwambia mama yake
Kwamba alikuwa amechoka miguu

Wimbo huu ni wimbo mmojawapo wa nyimbo za Kiafrika unaoimbwa na jamii ya Waluhya nchini Kenya. Wimbo huu unarejelea mtoto anayezunguka hapa na pale na

mwishoni, anarudi nyumbani na kumwambia mamake kwamba alikuwa anaumwa na miguu.

Tunaelezwa kwamba, "wanafunzi wenzake walirudiarudia na kucheza kama walivyojifunza. Burudani ilivyopamba moto, shule yote ilijipata ikiimba wimbo huo. Mgeni wa heshima alisimama na kijiunga na wanafunzi hao. Ndiposa Kito akaamua kutaja jina la mgeni huyo wa heshima bwana Magonji" uk. 13.

**5.** *Benja Magonji apepetanga*
*Benja Magonji apepetanga*
*Yatsiayo, yarulayo*
*Yaboola mama njonyi bilenje*. Uk. 13

**(Tasfiri)**
Benja Magonji anazunguka
Benja Magonji anazunguka
Alienda huku, huko na kule
Alirudi nyumbani na kumwambia mama yake
Kwamba alikuwa amechoka miguu

Uwasilishaji wa wimbo huu una utendaji mwingi na mgeni huyu alizungushwa zungushwa kwamba alienda huku na kule na mwishoni kwenye wimbo alirudi nyumbani na kumwambia mamake kwamba alikuwa anaumwa na miguu.

Wimbo huu ulishangiliwa sana. Mwalimu mkuu alisema "Asante sana kwa wimbo huo wa kuchangamsha…" uk. 13. Wimbo wenyewe ulichangamsha kwa sababu kulingana na mchoro wa picha katika ukurasa wa 13, tunaona watoto wakihusisha viungo vyao, wakicheza kwa ushindani mkubwa pamoja na mgeni wao.

### 4.2.2 Matumizi ya wimbo katika Bunilizi ya Kitamthilia

Michezo ya kuigiza inahusu uigaji wa matukio mbalimbali ya kijamii kama vile vita, jando, kazi mbalimbali na hekaheka za kila siku. Katika jamii za jadi, michezo ya kuigiza, ilikuwa ikisawiri harakati za binadamu kupambana na mazingira yake. Michezo hii ya kuigiza hutumia maleba yanayoambatana na muktadha wa shughuli

zenyewe na pia huhusisha tanzu zingine kama nyimbo, hadithi na ngoma (Method, 2015). Kuna aina nyingi za michezo ya kuigiza lakini kwa ajili ya utafiti wetu, tunaangalia maigizo ya watoto.

Maigizo ya watoto hutendwa na watoto katika michezo yao ya kila siku. Maigizo ya watoto ni michezo ya kuigiza ambayo hutendwa na watoto wenye umri sawa (Ussi, 2015; Bwire, 2004). Maigizo haya hutumia watoto kama fanani na hadhira katika kuigiza mambo ambayo watoto hushuhudia katika mazingira yao (Bwire, 2004). Kwa ajili ya utafiti wetu, watoto tunaorejelea hapa ni wa daraja la tatu au darasa la nne hadi la nane kulingana na mfumo wa 8-4-4 wa elimu nchini Kenya. Tunapozungumzia usawa hapa, tunamaanisha umri karibu sawa na mara nyingi ni watoto wa kiwango au darasa sawa. Watoto hawa huelewana kimawazo na kuna uwezekano wa kuwa katika mazingira sawa, kwamba wanapoigiza matukio katika michezo yao ama kwenye nyimbo zao basi wanaelewana vizuri.

Aidha, maigizo haya hutendwa na watoto wakati wa michezo yao ya kila siku. Watoto, kwa kawaida hawahusishwi sana katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Kwa hivyo, wakati wao mwingi hutumika mchezoni. Muda wao mwingi ni wa mapumziko na hapo ndipo michezo mbalimbali huchezwa. Michezo hii hutofautiana kutegemea jamii, ingawa michezo hiyo huweza kufanana, lakini majina ya michezo huenda yakawa tofauti. Kubo na wenzake (2013) wanasema kwamba, uigizaji wa michezo unashirikisha tanzu zingine kama vile nyimbo, ushairi, ngoma na kadhalika. Kwa kweli,wimbo ukiambatanishwa na uigizaji hupendeza na huvutia watoto sana.

Ramadhan (2018) anasema kwamba utendaji ni tukio la aina yoyote ile inayojumuisha hadhira pamoja na fanani wake kwa minajili ya kuigiza au kuonyesha tabia za wanadamu. Anachomaanisha Ramadhan hapa ni kwamba, katika jamii nyingi za

Kiafrika, utendaji ni mojawapo ya kanuni za maisha ya kila siku. Katika ulimwengu wa mtoto, utendaji unaoambatana na wimbo unavutia mtoto kwa sababu utendaji unaibua suala la uhalisia na vilevile kiburudisho katika ulimwengu wao wa kitoto.

Nandwa (2013) katika kitabu chake *Kito Apepeta* anasema kwamba, “Njiani, waliimba wimbo huo huo wa ‘apepetanga’. Walijaza majina yao wakichezacheza na kuruka.Waliimba

**6.** *Kiki wa mama apepetanga*
*Titi wa mama apepetanga*
*Toni wa mama apepetanga*
*yatsiayo, yarulayo*
*yaboola mama njonyi bilenje (uk 16)*

(Tafsiri)
Kiki wa mama anazunguka
Titi wa mama anazunguka
Toni wa mama anazunguka
Alienda huku, huko na kule
Alirudi nyumbani na kumwambia mama yake
Kwamba alikuwa amechoka miguu (uk. 16)

‘Waliendelea kufanya mabadiliko wakihifadhi mdundo wake’. Wimbo wenyewe ulipamba sana kwa sababu ya utendaji unaohusika. Kitendo cha kuruka huku wakiimba na utendaji unaowashirikisha watoto ni kuwaburudisha. Hata hivyo, wimbo katika ulimwengu wa mtoto una manufaa sana;

### 4.2.3 Wajibu wa nyimbo katika fasihi ya watoto

Jukumu la kimsingi katika nyimbo za watoto ni kuburudisha na kuelimisha. Nyimbo hizi ni hazina kubwa katika ujenzi wa jamii mpya, kuanzia ngazi ya chini kabisa kwa maisha ya mtoto. Katika jamii ya Kiafrika, ni chombo kitumikacho katika kupambana na mambo muhimu katika mazingira yanayomzunguka mtoto. Yafuatayo ni baadhi ya majukumu ya nyimbo hizo za watoto kama ilivyojitokeza katika bunilizi teule.

**4.2.3.1 Kukuza watoto kiakili /kifikra**

Kama tulivyotanguliza kwamba nyimbo za watoto hubeba ile dhana ya kimsingi ya kuchangamsha, nyimbo hizi humjenga mtoto kiakili na kumfanya aweze kufikiria jambo fulani kwa wepesi. Ili mtoto aweze kuwa na upeo mkubwa katika kulidadisi jambo fulani, kulijua na kulitekeleza ni lazima nyimbo zitumike katika uwanja wake. Nyimbo humfanya mtoto kuelewa vitu vingi kwa urahisi kutokana na uwezo wake wa kujifunza. Kulingana na uwezo wa mtoto, suala la wimbo kupitia kwa ukariri hurahisisha mafundisho tofauti na ile ya kufundishwa au kuandika tu. Katika hali hii ya kuimba na kuukariri wimbo ndipo kunatokea upevushaji wa kiakili na hata fikra.

Tunapoangazia safari ya masomo ya mtoto kidaraja, tunagundua kwamba katika ngazi za awali, mtoto huanza masomo kupitia ule ukariri wa maneno hasa katika zile hatua za awali za ujifunzaji lugha (Ventriglia, 1992). Anavyosema Ventriglia ni kwamba, kuna hatua tano za ujifunzaji lugha. Hatua tatu za awali ni uzalishaji wa awali, uzalishaji wa mapema na uibukaji wa matamshi. Hivi ni viwango vya ukariri wa maneno tunayozungumzia kwa sababu mtoto bado hajamudu lugha vizuri ila ni kupitia urudiaji. Kiwango chake cha uelewa bado hakijaimarika. Hatua za mwisho ni hatua ya nne na tano; umilisi wa kati na umilisi stadi. Viwango hivi ni vya watoto wa umri kati ya miaka mitano na kumi. Katika umri huu, watoto wanaweza kuimba nyimbo zao za kitoto kama njia moja ya kupitisha ujumbe unaokusudiwa wakiwa na uelewa wa kinachozungumziwa.

Kuimba nyimbo ni kujijenga kwa mambo mengi kama kujipanua kiupeo, kujua na kutosahau vitu, kujiongezea maneno katika ubongo na kumfanya mtoto aweze kujifunza kutamka maneno. Haya yote hujengwa kwa nyimbo. Pindi mtoto aimbapo huweza kujifunza kwa kuwa mwepesi wa kutamka maneno na ndipo tunaona mtoto huanza kusikiliza jambo na yeye kulitamka jambo hilo baadaye na si kuandika. Suala

hili hujitokeza wazi pale ambapo unaweza kupata mtoto akiwa na ule uwezo wa kuimba nyimbo kadhaa na wakati huo huo anaweza kuwa ana shida ya kuandika au hata kusoma.

Katika uandishi wa bunilizi hizi za watoto, waandishi wa vitabu wamefanikiwa kutumia nyimbo katika kazi zao wakiwa na lengo la kupevusha akili za mtoto. Kwa mfano, Momanyi, (2009) katika kitabu chake *Mchezo wa Kobole* ametumia mbinu hii kwa lengo la kujenga fikra za mtoto. Anatueleza kwamba "Katika kikundi kingine, mwalimu Kabau alivutiwa na wanafunzi walioimba kwa kupokezana, huku wawili wao wakiwa wameshikana mikono na nyuma yao wakiwa wamefuatiwa na wengine walioshikana viunoni. Mmoja wa wanafunzi alijaribu kuibabatua mikono hiyo iliyoshikana akiiga ukataji.

**7.** *Hapa n'kate au n'sikate*
*Kuna mwiba wa mchongoma*
*Kwa panga*
*Haukatiki!*
*Kwa shoka*
*Haukatiki!* Uk. 18

Wimbo huu unajenga fikira kwa sababu mtoto lazima ajue jinsi ya kuukariri na kucheza mchezo wenyewe. Hali kadhalika, wimbo huu unaibua fikira ya umuhimu wa umoja na ushirikiano katika jamii. Katika uk. 19 wa '*Mchezo wa Kobole'* inaonekana kwa picha vikundi viwili; wasichana kwa wavulana wakivuta kamba kwa pamoja. Suala hili ni kioo cha ushirikiano katika jamii. Hali kadhalika, kuna wimbo katika uk. 19 ambao tunaelezwa na mwandishi kuwa ulichezwa na kikundi cha watoto wadogo. Msimulizi anasema, "wadogo waliamua kuchezea mchanga ambao ulikuwa na unyevu baada ya mvua kunyesha. Waliunda viduta vidogo vidogo vya mchanga huo huku wakivipigapiga na kuimba"

**8.** *Kipuupuu*
*Punga moto*
*Kipuupuu*
*Punga moto*…(uk. 19)

Mara nyingi, nyimbo za watoto wadogo hazina ujumbe wowote. Nyimbo zao huimbwa wakiwa michezoni kwa ajili ya kujiburudisha tu. Uradidi kwenye wimbo huu hujenga fikra za mtoto na kumfanya kuupenda mchezo wenyewe. Michezo hii mbalimbali iliyochezwa na vikundi tofauti vya watoto kando na suala la ushirikiano, inaonyesha majukumu mbalimbali yanayotekelezwa na jinsia tofauti katika jamii.

### 4.3 Utanzu wa Mashairi

Katika sehemu hii, tuliangalia jinsi waandishi wa bunilizi za watoto walivyofaulu kutumia utanzu huu wa ushairi katika kazi zao kwa lengo la kuwasilisha ujumbe maalum kwa msomaji. Kwanza kabisa, tulifafanua dhana ya shairi kisha tukajadili matumizi ya mashairi katika bunilizi teule.

#### 4.3.1 Ushairi

Wataalam wengi wamejaribu kufafanua dhana ya ushairi. Abedi (1954) anasema:

> "Ushairi au utenzi ni wimbo. Hivyo, kama shairi haliimbiki basi halina maana."

Shaaban (1958: 37) anasema:

> "Ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na tenzi. Zaidi na kuwa sanaa ya vina, ushairi una ufasaha wa maneno machache au muhtasari…mawazo, maono na fikra za ndani zinapoelezwa kwa muhtasari wa ushairi huvuta moyo. "

Wataalam hawa wawili wanaamini kwamba ushairi ni wimbo na hivyo hupaswa kukaririwa kwa mahadhi fulani. Mulokozi (2005) anasema kwamba, baada ya miaka kumi ya ufafanuzi wa Amri Abedi, mtunzi mwingine wa kipindi cha ukoloni, Mnyampala (1965) aliandika:

> "Ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale, ndicho kitu kilicho bora sana katika maongezi ya dunia kwa kutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata iliyopangwa kwa urari wa mizani na vina maalum kuwa shairi…..".

Hali kadhalika, Wamitila (2008) anasema kwamba ushairi ni utungo unaoelezwa kwa maneno mateule kwa kutumia mbinu za lugha zenye mnato na mbinu nyinginezo za kibalagha na kimtindo zinazomwezesha mtunzi kuwasilisha ujumbe kwa ufupi na kwa mkokotezo mkubwa unaoeleza kisa, hisia, tukio au hali kwa lugha ya mvuto. Wamitila anaeleza kwamba, uzito hasa wa shairi upo kwenye uwezo wake wa kugusa hisia.

Mulokozi (1996) anaeleza kuwa, shairi ni utungo wa kisanaa unaotumia lugha teule na mpangilio fulani wa maneno wenye kusawiri hisi, wazo, hali, kitu au tukio fulani na papo hapo kuvuta au kuathiri hisia zetu badala ya kutumia lugha nathari.

Shairi ni utanzu wa fasihi unaotumia mpangilio wa lugha mkato, picha na yenye mapigo mahsusi katika kutoa maudhui. Kwa hivyo, vigezo vinavyotumiwa kuchambua na kuainisha shairi ni umbo lake pamoja na matumizi yake ya lugha (Ngugi, 2018). Senkoro (1982) anasema kwamba, shairi hutumia lugha ya mkato yenye kueleza maudhui yake kimuhtasari na aghalabu huyaficha maudhui yake ndani ya taswira na ishara.

Kwa mujibu wa King'ei (2000), shairi ni sanaa inayotumia lugha ya muhtasari na lililochanganuliwa kiufundi ili kuleta athari iliyokusudiwa. Kulingana na ufafanuzi wa wataalam hawa, shairi ni sanaa inayotumia lugha ya mkato iliyo na ufundi mkubwa kwa ajili ya kupitisha ujumbe fulani. Katika uandishi wa bunilizi za watoto, mashairi hutumika katika usimulizi na mashairi haya yanapokaririwa huwa mafupi na mepesi kwa ujumbe unaokusudiwa. Katika baadhi ya bunilizi teule za watoto, matumizi ya mashairi yametumika kwa lengo la kupitisha ujumbe maalum kwa msomaji. Hata

hivyo, mashairi haya katika vitabu teule vya watoto hayana maana fiche. Hii hurahisisha uelewa wa ujumbe kwa mtoto.

Mashairi ya watoto sharti yawe na ujumbe unaoeleweka na ujumbe huo utiririke kwa njia ya moja kwa moja. Maneno hayo sharti yawe ni ya hekima, yanayobeba hisia fulani na yanapaswa kuwa yanaelezea mambo yanayohusiana na imani za watu wa jamii husika (Mulokozi, 2005).

### 4.3.2 Mashairi katika bunilizi za watoto

Mashairi ya watoto ni mashairi yaliyoandikwa kwa ajili ya watoto au yanayofaa watoto. Haya yanaweza kuwa mashairi kuhusu watu '*folk poetry'*, mashairi yaliyoandikwa maksudi kwa watu wachanga, mashairi yaliyoandikiwa watu wazima, lakini yanayofaa watoto na mashairi yanayotolewa kwa kazi za bunilizi (Maria, 1995).

Mashairi ya watoto hapa ni tungo za kisanaa ambazo zinatumia lugha teule na huwa na mpangilio maalum wa maneno ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa na hubeba maudhui maalum yanayomhusu mwanadamu na tabia zake (Silverstein, 1969).

Mashairi haya ya watoto ni mashairi ambayo yanawasilishwa na watoto au yanayowasilishwa kwa ajili ya watoto. Mashairi ni utanzu wa fasihi na jinsi anavyosema Wamitila (2010), fasihi ya watoto ni fasihi ambayo imeandaliwa makusudi, kidhamira na kifani kwa ajili ya hadhira ya watoto. Kulingana na maelezo ya Wamitila hapa ni kama anarejelea watoto ambao wana uwezo wa kusoma na kuelewa kazi za fasihi. Katika utafiti huu mashairi ya watoto yanarejelea mashairi yanayolenga watoto wa viwango vya daraja la tatu. Uwasilishaji huu huzingatia zaidi uwezo wa watoto kuukariri wala si wa kusoma mashairi hayo kwa kina.

Mashairi ya watoto yana sifa bainifu za ushairi (Jones, 2008). Mashairi ya watoto sharti yawe na maudhui mepesi (Reichard, 1998; Russell, 2005; Jones, 2008). Hii ni kwa sababu watoto hawana tajriba nyingi kuhusu maisha na hivyo hawataweza kufasiri masuala changamano jinsi ilivyo kwa mashairi ya watu wazima. Wao huelewa ulimwengu wao wa michezo, kuadhibiwa na wazazi na mazingira wanamoishi.

Bower na Barret, (2014) wanasema kwamba sifa bainifu ya mashairi ambayo inatenganisha mashairi na mifumo mingine ya maandishi ni uwepo wa muwala. Kwamba, lazima shairi liwe na muwala. Huku ni kule kukaribiana kwa matamshi ya sauti fulani. Sauti zenye midundo zinazokaribiana hupendeza watoto sana. Pia, shairi lazima liwe na ubeti. Ubeti huweza kutenganisha ujumbe mmoja na mwingine unaopatikana katika kila ubeti. Beti hizi ni sharti ziwe nyepesi maana ujumbe unaowasilishwa vilevile ni mwepesi. Vilevile, huwepo ruwaza mbalimbali kama vile uradidi katika muwala, hasa katika mishororo na mizani fulani.

Suala la kuainisha mashairi limejadiliwa na wengi wakiwemo Mnyampala (1975), El Kaiim (1985) na Shabaya na wenzake (2009). Wote wanakubaliana kwamba shairi huainishwa kutegemea kigezo cha dhima inayotekelezwa. Ingawaje Mnyampala (keshatajwa) anazingatia kigezo cha uhodari na ubora wa shairi husika hasa anapoainisha mashairi mazito, yaani yenye maudhui ya msingi kwa kutofautisha mashairi mepesi ambayo hayana maudhui muhimu au ya kimsingi. Mashairi ya watoto mara nyingi hayana maudhui mazito maana ujumbe unaopaswa kuwasilishwa ni mwepesi kutegemea umri wa mtoto.

Namlola (2019), katika bunilizi yake *Hidaya* ametumia utanzu huu wa ushairi katika usimulizi wake. Kilichomchochea mamake Hidaya kumkaririria shairi mwanawe ni

matatizo waliyopata kutokana na ugomvi na babake mzee Matata. Ugomvi unahusu suala la kuozwa kwa bintiye kwa lazima kwa bwana Mapesa. Msimulizi anasema, "Mama Pembe alikuwa kaiva macho kwa kwikwi za usiku kucha huku akimwomba Mola wake atoe mwanga (Uk. 20). Anasema, "Mwanangu usikate tamaa kwani haya ni mawingu, yatapita. Nakumbuka shairi moja la Malenga wa Mndani liitwalo Ganda la Muwa. Nakumbuka baadhi ya beti zake zisemazo:

**9.** Mola aliloamuwa, mja hana upinzani,
Ndilo litakalokuwa, hata mja afanyeni,
Nikama ganda la muwa, lilotupwa ardhini.

Ganda la muwa la jana, chungu kiwa mawindoni,
Huliona tamu sana, kilitia mdomoni
Japo halina maana, kwa watu wa mitaani.

Sawa na mkwaju mui, ukaavyo msituni
Tumbili haushitui, na kamwe hawauoni
Siku kwisha uadui, wakautia thamani.

Nawe punguza mtima, ingawa hujulikani,
Muhimu simama wima, itapita mitihani
Watakuja hima hima, wakuombe samahani". (uk 20)

Kulingana na maelezo ya msimulizi, hapo awali, Hidaya alikuwa amehuzunika na kushindwa na la kufanya. Hii ni kwa sababu babake (bwana Matata) alitaka kumlazimisha kwa ndoa ya mapema. Kulingana na Hidaya, elimu ilikuwa nguzo ya maisha. Hata hivyo, "Shairi hili lilimpa ari mpya Hidaya aliyefuta machozi na kuchukua ujasiri mpya ambao hakuwa nao hapo awali. Ujumbe alioupata kutokana na shairi lenyewe ni kwamba yeye hakuwa wa kwanza kufikwa na msukosuko." (uk. 21).

Ujumbe katika shairi hili unadhihirika katika kila ubeti. Katika ubeti wa kwanza, mama Pembe alimjuza mwanawe kuwa chochote alichoamua Mola, hakuna mja atakayetoa upinzani, kwamba kwa mipango ya Mola, binadamu hawezi akatoa upinzani. Anachomaanisha mama hapa ni kwamba ni mapenzi ya Mola kwa Hidaya kukamilisha masomo yake jinsi alivyokuwa amepanga.

Katika ubeti wa pili, mama Hidaya anamfahamisha mwanawe kwamba utamu wa kinachotafutwa si rahisi kupata maana wasioelewa utamu huo hawaoni maana ya kinachotafutwa. Utamu unaozungumziwa hapa ni utamu wa masomo aliyotaka Hidaya. Hali kadhalika, katika beti zinazofuata, mama Hidaya anamhimiza mwanawe asimame wima kwa tatizo ambalo lilikuwa likimsubiri, kwamba tatizo hilo lingepita na baadaye waliomkosea wangekuja kumwomba msamaha. Hata hivyo, alimkumbusha kwamba hangepaswa kujisumbua na tatizo hilo maana watenda mabaya duniani walikuwa wengi na kuna hata yale mabaya zaidi watendewayo binadamu kuliko yale ambayo ametendewa yeye.

Kwa hivyo, ujumbe katika shairi hili ni kuvumilia na kutokata tamaa licha ya matatizo kwani kuna matumaini ya kufanikiwa baadaye.

Kea (2013) katika kitabu chake *Msiba wa Kujitakia* anatuonyesha jinsi mbinu hii ya ushairi imetumika katika bunilizi yake. Hapa ni baada ya watu kusikia ungamo la Mwanakombo kwamba, alikuwa ametumwa na babake kwa akina Neema "ili awatilie dawa katika maji yao ya kunywa" (uk. 32). "Aliniambia kuwa hataki nicheze nao wala kwenda kwao. Akanionya kuwa nisimwambie yeyote, hata mamangu. Alinitishia hata kuniadhibu nisipotekeleza agizo lake…" (uk. 32). Watu waliposikia ungamo hilo, ndipo wakaelewa kiini cha maumivu ya mkewe bwana Katana. Wakabakia kuuma vidole kwa ukimya, isipokuwa mzee mmoja mkongwe aliyesema kwa masikitiko makuu:

**10.** Matanga ni kwomboleza, ufikwapo na mashaka,
Matanga pia yaliza, machozi yakaanguka,
Matanga yanatatiza, mtu tama akashika,
Matanga mbali pitia, mkosi usitutie.

Matanga pia msimu, wa kuwaaga wendao,
Matanga kwa wa kuzimu, na ahera wakaao,
Matanga yanalazimu, ni budi kwa wazikwao,
Matanga mbali pitia, mkosi usitutie.

Matanga likawa jina, alopewa binadamu,
Matanga ana hiana, ukuruba kwake sumu,
Matanga mkikosana, atakutia jahimu,
Matanga mbali pitia, mkosi usitutie.

Mwandishi anatueleza kwamba wote walimhongera mzee huyo kwa kuakisi hali halisi katika mazingira yale. Hali halisi katika mazingira yale ni masikitiko kuhusu hali ya mama Katana. Wengi walihofia maisha yake maana Matanga, baba Katana, mumewe mama Katana alikiri kwamba “Haina haja. Msipeleke sipitali. Hawezi kupona... kama inavyosemekana, akiiruka haponi. Dawa ni kumzika...” (uk. 31). Anavyoeleza Kea (keshatajwa) ni kwamba mgonjwa huyo alihitaji mganga ndipo agangue jinsi alivyosema Mwanakombo “Baba tutabaki na nani? Mgangue mama jamani…mama ee” Mtoto huyo alilia (uk. 31).

Kupitia kwa maelezo haya, ndiyo maana mzee huyo mkongwe alisikitika kupitia kwa shairi lake. Katika ubeti wa kwanza, mzee huyu anaonyesha jinsi watu huomboleza washikwapo na mashaka. Anasema kwamba matanga hutatiza mtu kwa kumpa mawazo ambayo yanaliza. Katika ubeti wa pili msimulizi anasema kwamba Matanga ni kama sherehe ya kuwaaga wenda zao; kwamba ni lazima kwa wale wanaozikwa. Katika ubeti wa mwisho, anasema kwamba, matanga ni lazima kwa binadamu yeyote maana sherehe hii ni mpito wa kuzimu ingawaje mzee huyu anaomba kwamba matanga iwapotelee mbali maana ingewatia mikosi au shida.

### 4.3.3 Umuhimu wa mashairi kwa watoto

Mashairi ya watoto huwa na umuhimu anuwai katika maisha ya mtoto ingawa katika kiwango kile cha watoto wa ngazi za awali huwa ni ya kuburudisha na kukuza usanii wa lugha. Mashairi ya watoto husaidia mtoto kupata ujuzi wa kiutambuzi wa misamiati kupitia ule urudiaji unaotokea kwenye mishororo. Hii huunda muktadha mpya wa misamiati mipya. Husaidia mtoto katika harakati zile za kujieleza kupitia ule

ubunifu na hisia zinazotokea kwenye maneno. Hali kadhalika mtoto anaweza kukariri mambo kupitia zile ruwaza za maneno na ule utaratibu unaohusishwa na ufundi wa mashairi.

Namlola, (2019) katika bunilizi *Hidaya*, kuna shairi alilokumbuka mamake Hidaya la *Diwani ya Malenga wa mndani* lililoitwa *Ganda la Muwa* ni shairi ambalo limeandikwa kwa ufundi mkubwa wa lugha. Ufundi huu unaweza kumvutia msomaji hasa kwa kuangalia ule mtiririko wa vina, usawa wa vina na uhuru ule wa ushairi unaomfanya msomaji ang'amue maana inayotarajiwa. Tazama katika ukurasa wa 21

**11.** Mola aliloamu**wa**, mja hana upinza**ni,**
Ndilo litakaloku**wa**, hata mja afanye**ni**,
Ni kama ganda la mu**wa**, lilotupwa ardhi**ni,**

Ganda la muwa wa ja**na**, chungu kiwa mawindo**ni**,
Huliona tamu sa**na**, kilitia mdomo**ni,**
Japo halina maa**na**, kwa watu wa mitaa**ni**

Mpangilio huu wa vina na urudiaji wa silabi ya mwisho ni ujuzi wa kipekee katika uwanja wa ushairi na ndio kivutio kwa msomaji. Mtiririko unaonekana katika usawa wa vina vya ndani na vina vya nje katika kila ubeti.

Utoaji wa sauti na hata kuwepo kwa kidatu huvutia mtoto katika uwasilishaji wowote wa mashairi. Hali kadhalika, hukuza usanii wa lugha. Hii ni kwa sababu ya ule mvuto unaoandamana na uradidi wa maneno pamoja na kupanda na kushuka kwa sauti.

### 4.4 Utanzu wa Barua

Kwa mujibu wa Kamusi ya TUKI (2004:23) 'barua ni maandishi yenye ujumbe unaopelekwa kwa mtu mwingine kwa njia ya mkono au kupitia posta. Aghalabu barua huwa na ujumbe ambao mwandishi hulenga kumpasha mpokezi wake'. Kimuundo, kuna aina mbili muhimu za barua ambazo ni barua rasmi na ya kirafiki (kindugu). Barua rasmi huwa na muundo funge ambapo hamna utokaji nje wa muktadha kwa

wingi. Kwa upande mwingine, barua huria hurejelea aina ya barua ambayo ina muundo huru wa kutamba kwingi katika uadishi wake (Onchangu, 2013).

Abdalla (2014), anasema barua ni njia kongwe ya mawasiliano baina ya mtu na mtu, mtu na watu, taasisi na mtu, taasisi na taasisi inayolenga kutoa taarifa au ujumbe fulani ambao ni muhimu kufahamika kwa upande uliolengwa na barua hiyo. Hata hivyo, kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia hivi sasa, barua huandikwa kama ujumbe katika simu na kisha kutumwa kwa mlengwa na kumfikia mara moja. Hii haimaanishi kuwa, mfumo wa zamani wa kuandika na kutumiana barua haupo lakini imepungua kiasi kutokana na maingilio ya sayansi na teknolojia. Hali hii imefanya barua za kuandika katika karatasi na kutumiwa kwa mlengwa huchukua muda mrefu kumfikia mhusika (Khamis, 2007).

Jamii ya sasa imekumbatia matumizi ya teknolojia katika kutuma ujumbe. Emhemmd (2017) anasema kwamba, utumiaji wa barua kwa njia ya simu na mtandao kama barua pepe unafanya barua kutumia muda wa kufumba na kufumbua macho. Hata hivyo, ingawa matumizi ya barua yamedidimia katika jamii, kuna baadhi ya watu ambao bado wanatumia barua kama chombo cha mawasiliano. Watunzi wa kazi za bunilizi za watoto wanatumia mbinu ya barua katika kujenga dhamira fulani. Hii ndiyo mbinu wanayoelewa watoto maana katika kiwango hiki, watoto hufundishwa uandishi wa insha kama njia moja ya kuwasilisha mawazo yao. Katika bunilizi za watoto zilizochunguzwa, kuna matumizi ya barua ndani ya tanzu zingine za kifasihi.

### 4.4.1 Utanzu wa barua ndani ya bunilizi

Barua ni ujumbe unaoandikiwa mtu kwa ajili ya kupasha habari fulani. Ujumbe unaoandikiwa mtu unaweza kuwa rasmi au yasiwe rasmi. Katika ulimwengu wa watoto hasa wa kiwango kile cha daraja la tatu, barua wanazojua watoto ni zile tu za

kirafiki. Barua hii ya kirafiki inafaa sana kwa kiwango kile, kwa sababu watoto wanaweza kueleza kuhusu mazingira ya michezo, uhusiano na wazazi wake, ndugu na hata nyanya na babu zake. Mara nyingi, mtoto huandika barua kwa wale ambao wana uhusiano wa karibu sana kwa ajili ya kujieleza hasa kuhusiana na maisha yao na changamoto anazopitia.

Syokau (2018) katika hadithi ya *Kade na Katana* anatuonyesha jinsi msimulizi alivyoandikiwa barua ya kirafiki na nyanyake akimsihi amtembelee. Msimulizi anaeleza kwamba alikuwa anajiandaa kwenda safari ya mbali na "safari hiyo ilikuwa ianze" (uk. 1) maana alikuwa tayari na alikuwa amewakosa jamaa zake. Katika barua hiyo ilisadifu kwamba nyanya kwa upande mwingine alikuwa amemkosa msimulizi.

**12.** *"Mjukuu mpendwa kibibi,*

> *Salamu chekwachekwa…nina bashasha nyingi kukuandikia barua. Natumai u salama salimini….*
>
> *Madhumuni ya kukuandikia barua hii ni kukuomba uje nyumbani angalau tuonane macho kwa macho. Ndugu zako wanakuulizia kila siku nami ninataka pia tuzungumze kwa kina. Jaribu uje wikendi hii ukipata idhini kwa bosi wako. Utakuwa umenifurahisha sana.*
>
> *Wasalimu wote huko uliko.Tunakungojea kwa hamu nyingi.*
>
> *Ni mimi bibi yako*
>
> *Zambarau Kajaza." (*uk. 1)

Katika maisha ya mtoto wa Kiafrika, tunafahamu kwamba kuna uhusiano wa karibu kati ya nyanya na mtoto. Katika tamaduni za Kiafrika kwa mfano, mtoto kumtembelea nyanyake ilikuwa muhimu sana. Tofauti na sasa ambapo watoto wamehusishwa na masuala ya kiteknolojia na utalii wa maeneo mbalimbali.Watoto walienzi matembezi hayo maana wana mengi ya kujifunza kwa nyanya kando na hadithi. Wanapata wosia na ukarimu jinsi wanavyopata kwa wazazi wao. Mara nyingi, suala la kuadhibu mtoto akiwa kwa nyanyake ni kwa njia ya maelekezo si kwa njia ya kiboko jinsi wafanyavyo wazazi wengine. Pia, hamna mabishano mengi mtoto

afanyapo kosa. Barua hiyo aliyoandikiwa kibibi na nyanyake ilikuwa na ujumbe ufuatao:

Kwanza, alitaka kumjulia hali. Ni jambo la kawaida katika tamaduni nyingi za Kiafrika, watu kujuliana hali. Hata katika mahusiano ya kila siku, watu walitanguliza kwa kujuliana hali kabla ya maendelezi ya mahusiano yao. Katika barua ama rasmi au ya kirafiki, Doyle (2019) anasema kwamba njia nzuri ya kutanguliza barua katika uandishi wa barua hasa za kitaaluma ni kuanza na salamu nzuri. Salamu nzuri hujenga toni katika barua na ni ishara nzuri ya ujuzi wa mawasiliano ya kimaandishi, vivyo hivyo katika barua ya kirafiki. Barua ya Kibibi ilianza kwa salamu hizo maana nyanya alitaka kumweleza kwamba walikuwa salama ila tu alitaka kujua hali yake Kibibi. Hii ni sababu moja ya kumwandikia barua mjukuu wake.

Sababu ya pili ni kwamba alimwomba aende nyumbani kwake nyanya ili aonane naye macho kwa macho. Ndugu zake walikuwa wanamuuliza kila siku. Pia nyanya alitaka azungumze naye kwa kina; na angefurahi sana ikiwa Kibibi angefika pale na mwisho, nyanya alitaka Kibibi awasalimie wote waliokuwa pale alipokuwepo.

### 4.4.2 Barua ndani ya hekaya kwenye bunilizi

Hekaya ni hadithi zinazomsawiri mhusika anayetumia ulaghai kupata matilaba yake kutoka kwa wengine. Mulokozi (1996) anaeleza kwamba hekaya ni hadithi ndefu inayozingatia matukio machache ya kusisimua na kustaajabisha. Msuko wake wa matukio ni sahili na wahusika wake huwa ni wachache. Wahusika katika hekaya ni binadamu au wanyama na wakati mwingi katika jamii za Kiafrika hadithi hizi huwa na funzo la kimaadili hasa kwa watoto. Katika jamii za Kiafrika, hususan Nchini Kenya, hekaya na hadithi nyingine zilisimuliwa katika mazingira alimolelewa mtoto. Kila utamaduni una namna yake ya kusimulia hadithi.

Syokau (2018) amefaulu kwa kutumia mbinu hii katika kazi yake *"Kade na Katana*". Tunaelezwa kwamba, Kibibi ambaye ni msimulizi baada ya kualikwa na nyanyake na mwishoni kumtembelea, alimsihi nyanyake awasimulie hadithi wakiwa na ndugu zake. Hapo ndipo nyanya "akakalia mkeka wake mweusi uliokuwa na michoro ya minazi na kutazama ufuo wa bahari na kuwaambia "Leo nitawasimulia hekaya" (uk. 5). Usimulizi wa hadithi katika jamii za Kiafrika ulihitaji maandalizi na wakati maalum hasa wakati wa mapumziko. Anavyotueleza Syokau (2018) ni kwamba fanani na hadhira yake walikuwa tayari kwa kitendo kile maana ilikuwa baada ya chakula na fanani tayari alikuwa kakalia mkeka.

Hekaya hiyo ilihusu kaka wawili Kade na Katana ambao walikuwa na mienendo tofauti. Kade alikuwa na mienendo mibaya iliyomfanya apate wivu kwa bidii ya kakake Katana aliyekuwa na mienendo mizuri. Mwishoni mwa hadithi, tunaelezwa kwamba Kade aliandika barua baada ya kupatwa na ugonjwa uliodhoofisha afya yake (uk. 33).

*Kwa naibu wangu,*

**13. *KUH: OMBI LA KUTAFUTIWA DAWA***

> *Ninaandika barua hii kwa nia ya kuomba usaidizi wako wa kutafutiwa dawa. Nimekuwa nikiugua kwa siku kadhaa sasa bila kupata nafuu. Sababu ya kutaka wewe na wenzako mnitafutie dawa ni kuwa nimejaribu kuitafuta ila nimeambulia patupu. Atakayeniponya nitampa zawadi kubwa, waarifu wote wanaoweza kunisaidia.*
>
> *Wako mwaminifu..(uk.34)*

Hali hii ya Kade ilitokana na kujilimbikizia mali baada ya kuiba mkufu wa kakake aliyopewa na nyanya wa kupanga. Wizi wake ulimsababishia mateso kwa sababu hakuwa ametambua siri ya mkufu huo. Basi akaandika barua kwa dharura akiomba msaada kwa yeyote ambaye angemponya na kuahidi kuwa angempa zawadi.

Matundura (2009) katika kitabu chake *Sitaki Iwe Siri* ametumia mbinu hii ya barua. Mwandishi ametuonyesha jinsi Musa aliweza kupokea barua kutoka kwa Wizara ya Afya. Mwalimu mkuu wa shule yake, Bw. Said Selemani, ndiye alimletea barua ya kumtangazia ushindi wake kwa uandishi wa insha ambao alikuwa ameushiriki katika shindano la uandishi wa insha lililotangazwa katika gazeti la *Taifa Leo*. "Mwalimu mkuu alishuka haraka kutoka kwenye gari. Katika mkono wake wa kulia alikuwa na barua huku mkono mwingine ukibeba gazeti la *Taifa Leo*." (uk. 53). Barua yenyewe ni ya Musa Matano.

**14.** *Kwa Musa Matano,*

*Rej: Ushindi wa Insha yako 'SITAKI IWE SIRI'*

*Wizara ya Afya kwa ushirikiano na shirika la Afya Duniani (WHO) ina furaha kukufahamisha kwamba mtungo wako,'Sitaki Iwe Siri' ndio uliokuwa utungo bora zaidi kwenye shindano letu.*

*Mbali na kukutuza zawadi kemkem, Wizara ya Afya pamoja na Shirika la Afya Duniani (WHO) zitagharamia masomo yako na ndugu zako katika viwango vyote vikiwemo vyuo vikuu… (Uk.56)*

*Wako mwaminifu,*

*Lilian Mokeira (katibu mkuu)*

Kando na kumtangazia ushindi wake, Musa alituzwa zawadi kemkem na kugharamiwa masomo yake pamoja na dada zake. Hii ilikuwa jibu la ombi ambalo walikuwa wakiliombea kila asubuhi kwa sala zao kabla waende shuleni. Ukwa alipokuwa akisali pamoja na Haki, alisema;

**15.** "Tusaidie masomoni
Kila siku shuleni
Amina" (uk.4)

Barua hii ilikuwa baraka kwa mayatima hao pamoja na nyanya yao.

### 4.5 Mazungumzo Ndani ya Hadithi kwenye Simulizi

Kamusi ya Karne ya 21 inaelezea mazungumzo kuwa utaratibu wa kuongea baina ya pande zote mbili ambapo kwa kawaida wahusika ni watu.

Syokau (2018) ametumia mbinu hii ya mazungumzo ndani ya hadithi kwenye bunilizi. Uzungumzi wenyewe umeanza kwa maamkizi na maamkizi hujikita katika miktadha ya kijamii ili kuonyesha heshima (Ndalu, 1997). Kwa mfano, "Shikamoo nyanya" (uk. 4). Katika tamaduni za kiafrika, kila jamii ina namna ya kuanzisha mazungumzo na hali hii huthaminiwa sana hasa mtoto anapokua, elimu ya kwanza anayopewa na jamii inahusu jinsi ya kuamkuana. Wanapokuwa wadogo, watoto hufunzwa namna ya kuanzisha na kuitikia maamkizi. Watoto wangekosa kufanya hivyo wangeonekana watovu wa nidhamu (Ngugi, 2014).

Vilevile, Mazrui (1998) anasema, vijana, wazee na watu wa makamo hutarajiwa na jamii kwa jumla kutumia maamkizi yenye heshima kwa yeyote anayehusika. Mazungumzo katika bunilizi huleta uhalisia katika ulimwengu wa mtoto. Mazungumzo haya yalianzia pale Katana alipompata ajuza akielekea nyumbani akitoka baharini. Ajuza yule alikuwa akiubeba mzigo mzito (uk. 13). Kama desturi, tunaambiwa kwamba Katana alikuwa anataka kumsaidia (uk. 13.)

**16. Katana:** Shikamoo nyanya
**Nyanya:** Marahaba, mjukuu wangu
**Katana:** Naomba nikusaidie kuubeba mzigo huu wako mzito
**Nyanya**: Nitashukuru sana.Wengi wamenipita hapa tu, bila neno.
**Katana:** Samahani kwa hilo...Twende basi. Ongoza ndipo nikufuate unakoenda
**Nyanya:** Haya basi. Lakini nakuonya. Niendako ni mbali. Nashukuru kwani tayari nimeburahi.

Mazungumzo haya pamoja na ukarimu wa Katana ndicho chanzo cha kubadilika kwa maisha yake. Kando na kusaidia familia yake, Katana alikata shauri amsaidie ajuza yule hasa baada ya kugundua kuwa "ajuza yule alikuwa akiishi maisha ya upweke'

(uk 15). Mabadiliko yalitokea baada ya ajuza yule kumpa mkufu wa thamani uliomtoa Katana katika hali ya ufukara na akawa tajiri wa kutajika. Mkufu huo aliopewa na ajuza ulipaswa kuuzwa ndipo apate mali. Mkufu uliokuwa ndani ya kibuyu haukupaswa kuuzwa maana ulipaswa kuwasaidia wanakijiji. Mkufu huo ulikuwa wa ajabu. Ajuza anamwambia Katana, “Sasa hivi, ibebe mikufu hiyo, uende hadi soko kubwa la Utende. Mikufu hii nimekupa kwa ukarimu ulionionyesha bila kuchoka…uiuze ili ufanye yanayohitajika nyumbani…” (uk. 21)

**4.6 Utanzu wa Ndoto ndani ya Hadithi**

Kamusi ya Karne ya 21 inatambua ndoto kuwa ni mfululizo wa picha, mawazo, mihemko na hisia ambao unatokea akilini, kwa kawaida bila makusudi katika hatua fulani fulai za usingizi.

Syokau (2018) katika kitabu chake *Kade na Katana* anasimulia ndoto aliyoota Katana kumhusu nduguye Kade. Badala ya fujo zake za kawaida, alizokuwa maarufu kwazo, anaamua kuwa mpole kwa nduguye. Akaagiza chakula kiletwe wale pamoja. “Mwana wa mama, nataka tule pamoja, kwa furaha na amani. Sisi ni ndugu, sio?” Kade akasema huku akimtazama Katana na kutabasamu...(uk.26). Ndoto hii ilitokea baada ya Katana kutambua kwamba kakake Kade hakuwa anafurahia ufanisi wake. Kwa hivyo kwa kiwango fulani inaonekana Katana alipatwa na wasiwasi kuhusu usalama wa mkufu wake kwa sababu Kade alikuwa amejulikana kwa wizi wake katika kijiji cha Wema.

Kutokana na ndoto hiyo, ukweli ni kwamba, Kade hakuwa amebadilika kuwa mwema ila alikuwa anataka kuunyemelea mkufu ule ili hata yeye aweze kutajirika kama kakake. Hakuwa mtu mwenye bidii ila alikuwa mzembe na mwenye wivu kupindukia. Mwishoni mwa ndoto, tunaarifiwa kuwa Kade alifanikiwa kuuiba ule mkufu,

akatajirika na kujiingiza katika maisha ya anasa yenye uchoyo mwingi. Maagizo aliyopewa Katana na ajuza yule kuhusu manufaa ya mkufu kwa jamii nzima hakuyaelewa Kade. Kwa hivyo, tunaarifiwa kwenye ndoto kwamba, Kade hakufurahia tena mali yake maana "mkufu aliokuwa ameuweka Kade kwenye chungu chumbani mwake ukawa hautulii. Kila alipokuwa akila, mkufu ulijitoma kwenye chakula chake….hangeweza kula kwa raha tena" (uk. 37). "Mkufu ukamcharaza na kumfukuza kutoka chumbani..." (uk. 38). Baadaye, Kade alimwomba nduguye msamaha kwa kuiba mkufu wake.

### 4.7 Hekaya/Hadithi Ndani ya Usimulizi

Hadithi ndani ya hadithi ni dhana inayomaanisha simulizi moja kuingiliwa na nyingine. Kwa mfano, mwandishi kama msimulizi mkuu wa hadithi anampa nafasi mhusika katika hadithi kusimulia hadithi nyingine. Katika dhana hii kunakuwa na hadhira tofauti kutokana na idadi ya usimulizi. Mathalani, tunaposoma hadithi, halafu ndani ya hadithi hiyo tukakuta mhusika mwingine ndani ya hadithi hiyo akiwasimulia wengine, hapo tunakuwa na hadhira ya aina mbili. Sisi kama wasomaji tunakuwa hadhira, na wale wanaosimuliwa na mhusika katika hadithi nao pia ni hadhira nyingine. Kwa mfano, ndani ya hadithi ya kitabu cha *Kade na Katana* kuna wasimulizi wawili. Mmoja ni mwandishi mwenyewe akisimulia msimulizi mwingine ni nyanyake Kibibi akiwasimulia wajukuu wake hekaya kuhusu vijana wawili Kade na Katana ambao walikuwa ndugu lakini tofauti kimaadili.

Kibibi alipofika kwa nyanyake, nyanyake aliwasimulia hadithi pamoja na nduguze. "..Leo nitawasimulia hadithi" (uk. 5). Nyanya akakalia mkeka wake mweusi uliokuwa na michoro ya minazi na kutazama ufuo wa bahari. Hadithi yenyewe ilihusu vijana wawili; Kade na Katana waliokuwa wanafanana sana lakini tofauti kitabia na kimwenendo. Kulingana na usimulizi wa hadithi, Katana alikuwa kijana mwenye bidii

maishani na bidii hiyo ilitokana na jinsi alijaribu kumudu maisha yake pamoja na ya familia yake. "…akijikaza na kufanya juu chini kuboresha maisha yake na ya familia yake" (uk. 12).

*"Aliosha nyumba, akawa Dobi na hata kupalilia mimea…*' (uk. 12)

Kakake Kade alikuwa mvivu na "aliamka wakati aliotaka" (uk.12). Na hali kadhalika alikuwa kiongozi wa genge la majambazi. "…Kade alijumuika na genge la majambazi" (uk. 12).

**4.8 Utanzu wa Sala**

Sala ni mawasiliano ya moja kwa moja na Muumba.

**17.** "Baba yetu uliye mbinguni
Watazame wanao ulimwenguni
Tunaotapatapa maishani
Mayatima maskini…" (uk. 2)

Sala hapa ni utanzu maalum unaoibuka kutokana na maombi. Sala hutokea katika maombi husika na hali kadhalika kutoka katika nyimbo zinazoibuka. Nyimbo nyingi zikiwemo za kidini na za kizalendo huhusisha sala. Katika vitabu teule, baadhi ya wahusika wameibua suala hili la sala kupitia kwa matendo yao.

Sala hii ilisemwa na Musa baada ya jimbi la kwanza kuwika na kutangaza kwamba kulikuwa kumekucha (Matundura, 2009). Inaonekana kwamba kijana huyu alikuwa anajutia kutokuwepo kwa wazazi wake maana anasema kwamba "angefurahia usingizi jinsi wanavyofurahia watoto wengine waliokuwa na wazazi" (uk 1). Mtoto huyu Musa anamwomba Mungu wake aliye mbinguni "awatazame wanawe ulimwenguni wanaopitia shida maishani hasa mayatima" (uk. 2)

Sala ya pili ilisemwa na Haki na Ukwa baada ya kuamshwa na Musa kaka yao. "..Punde tu baada ya kutoka kitandani, Haki na Ukwa walishikana mikono ili

wamshukuru Mungu kwa kumtunza nyanya yao.Walifumba macho na kuinamisha vichwa vyao tayari kwa maombi. Haki na Ukwa walisali kwa zamu ingawa siku hiyo ilikuwa zamu ya Ukwa kuongoza maombi, wao waliomba kwa ushawishi mkubwa”

**18.** “Mungu wetu wa haki
Shukrani kwa kumlinda Haki,
Asante kwa yetu siha
Shukrani kwa maisha
Asante kwa nyanyetu
Wahifadhi wazazi wetu
Mahala pema peponi
Tusaidie masomoni
Kila siku shuleni
Amina.” (uk.3)

Sala hii ilisemwa na Ukwa. Aliweza kuomba kwa ushawishi mkubwa sana jinsi ulivyosemwa na mwandishi.Yaliyomo kwenye sala ni kwamba, mayatima hawa waliweza kumtambua Mungu wao kuwa ni wa haki. Pia walimshukuru Mungu kwa ulinzi na kuwapa afya njema. Alimshukuru Mungu kwa kumlinda nyanya yao na hasa kuwepo kwa nyanya yao. Kuwepo kwa nyanya yao ni jambo walilolionea fahari maana nyanya alichukua nafasi ya wazazi wao. Hali kadhalika Ukwa alimsihi Mungu ahifadhi wazazi wao mahala pema peponi na awasaidie masomoni na kila siku shuleni.

### 4.9 Utanzu wa Insha katika Bunilizi

Kamusi Sanifu inaeleza maana ya insha kuwa ni kifungu cha maneno kilichopangwa kwa mpangilio maalum wenye kueleza kuhusu jambo fulani uliopangwa katika aya. Huweza kuelezea kuhusu matukio mbalimbali kama vile magonjwa, mafuriko, ajali, wanyama, michezo na matukio mengi.

Matundura (2009) ameonyesha kipengele hiki cha insha kinavyoweza kutumika ndani ya simulizi. Anatueleza kwamba baada ya Musa kuandika vidokezo kuhusu utungo wake na kumpelekea mwalimu wake wa Kiswahili, Bi. Rosa Mistika, mwalimu huyo

alimshauri aandike insha maana “Vidokezo katika uandishi wa insha ni kama dira tu ya kumwongoza mtunzi katika kuandika insha yake.” (uk. 44)

Mwandishi anasema, “Jumapili moja Musa alipokuwa nyumbani, alichonga penseli yake na kuandika insha ifuatayo:

**19.** SITAKI IWE SIRI

“Yuri alianza kuepukwa na marafiki zake anavyoepukwa mgonjwa wa maradhi hatari kama Ukoma (uk.44)

Kulingana na insha yake, Musa ameweza kuelezea kuhusu maisha ya msichana mmoja aliyekuwa akiitwa Yuri aliyeepukwa na marafiki zake baada ya kuugua ugonjwa wa Ukimwi. Kulingana na Musa, chanzo cha ugonjwa huo wa Yuri ni kujihusisha na mapenzi bila kinga. Anasema “yule msichana mwenye umri wa takriban miaka kumi na mitano alianza kuiramba asali ya maisha akiwa msichana mbichi.” (uk. 46)

Msichana huyu alishangiliwa na kuonewa staha na kila mwanamume na hata wasichana wenzake kumuonea gere. “Alianza ghafla kupungukiwa mikono. Hakuna hata mtu mmoja aliyetaka kumsalimia kwa mkono kwa kuhofia kuambukizwa maradhi…” (uk. 45). Hata hivyo, Musa ameweza kuelezea athari za maisha ya anasa na vile vile kuwaonya vijana kutolilia wembe maana “nyembe za ulimwengu zilikuwa zimemkata Yuri na kumjeruhi vibaya” (uk. 48)

Mwishoni mwa insha, msimulizi ametuonyesha kwamba, Yuri alifichua siri kwamba ugonjwa wake ulitokana na Ukosefu wa Kinga Mwilini na hivyo haikuwa siri tena. Huu ndio ulikuwa ufaafu wa anwani ya insha husika. Matundura (keshatajwa) ametumia utanzu huu kwa sababu ni utanzu unaoeleweka kwa watoto katika masomo yao. Watoto wa daraja la tatu huandika insha mara nyingi kuhusu masuala yanayowazunguka katika mazingira yao yakiwemo masuala ibuka kama janga la

UKIMWI. Lengo la mwandishi hapa ni kuhamasisha watoto kuhusu athari zinazotokana na maisha ya anasa.

### 4.10 Utanzu wa Picha au Michoro Mbalimbali

Matumizi ya picha na michoro ni uwakilishi wa sura ya mtu/watu au kitu/vitu kwenye karatasi au kitu chochote kinachoweza kuandikwa juu yake. Sura hiyo inaweza kuwa imechorwa au kupigwa picha kwa kutumia kamera au kuchorwa kwa kutumia mkono (Bakize, 2014).

Matumizi ya picha katika bunilizi za watoto husaidia mtoto kuelewa anachokisoma na kuchanganua hadithi husika (Lori, 2010). Lori (keshatajwa) anasema kwamba ikiwa mtoto amepata ugumu wa kuelewa kinachozungumziwa, basi michoro au picha kwenye kazi huweza kumsaidia kung'amua yale ambayo yanazungumziwa kwenye hadithi. Vilevile, watoto hupenda sanaa hasa ya uchoraji. Hii ndiyo maana watoto hupenda kuchora na kutumia rangi mbalimbali katika uchoraji wao. Watoto huvutiwa sana na picha au michoro kwenye vitabu vya bunilizi.

Katika bunilizi ya Matundura (2008), *Sitaki Iwe Siri*, picha zinaonekana katika jalada. Katika Uk. 3 kuna picha inayoonyesha Musa akiwaamsha dada zake Ukwa na Haki. Mwandishi ametumia picha hiyo kwa lengo la kusisitiza yaliyomo. Picha zinajitokeza katika uk. 5 11, 14, 18, 21, 24, 30, 33, 38, 51 na 54. Katika bunilizi ya Nandwa, (2013) *Kito Apepeta* kuna picha katika jalada, uk. 3, 5, 7, 8, 9, 11, 13, 15, 16, 18, 20, 25, 28, 30, 35. Mfano, katika uk 30, kuna picha inayoonyesha watoto wakiimba kwa furaha kwa kuzunguka kutoka upande mmoja hadi mwingine wakiwa wamevalia maleba kulingana na utamaduni ulimotoka wimbo huo. Utendaji huu katika wimbo unavutia sana katika ulimwengu wa mtoto. Katika bunilizi za watoto, dhana ya picha hujitokeza kwa sifa kadhaa za mwonekano wa wahusika wa hadithi zinazofafanuliwa

kwa msomaji. Kwa mfano, Momanyi (2009) katika *Mchezo wa Kobole* ametumia picha katika kurasa nyingi. Mfano katika uk 24 na 25, tunaona picha ya watoto darasani wakiwemo na walimu wao. Kutokana na maelezo ya mwandishi, inaonekana ni wakati ule walimu walikuwa wanajaribu kuwashawishi watoto waweze kufumbua siri ya mchezo huo wa kobole ambayo ilikuwa tisho kwa masomo ya watoto wale.

### 4.11 Michezo ya Watoto

Michezo ya watoto ni mila ambayo watoto hucheza wenyewe kwa wenyewe. Mara nyingi, michezo hii huchezwa na watoto katika mazingira yao kama vile nyumbani, malishoni, shuleni, wakienda mtoni na maeneo mengine.

Michezo hii hufungamana na utamaduni, uchumi na siasa ya jamii inayohusika. Isitoshe, michezo hii ya watoto huwasaidia watoto kujifunza mambo mbalimbali yanayotokea katika jamii yao pamoja na kuzifanyia hali anuwai za maisha yao majaribio (Slade, 1973). Kupitia michezo, mtoto hupata nafasi ya 'kubaki' mtoto huku akijiburudisha na kujielimisha kwa njia ya kipekee.

Lewis katika Fox (1976) na Siks (1977) wamejadili maudhui katika drama ya watoto. Wanadai kuwa kila hirimu ya watoto ina mtazamo tofauti wa maisha. Kwa hivyo, utungo ni lazima uzingatie maudhui yenye kuivutia hirimu hiyo. Siks (1977) anapendekeza drama bunilizi ya kifantasia au kinjozi kwa watoto wa miaka sita; hadithi mbabe kwa watoto wa miaka minane hadi kumi na mmoja. Nao watoto wa miaka kumi na miwili, kwa vile ni wadhanifu mno, anapendekeza kuwa watavutiwa zaidi na drama yenye wahusika walio na nguvu ajabu, ujasiri pamoja na uwajibikaji na ambao wataweza kutatua matatizo makubwa.

Maudhui kwa hirimu mbalimbali yanafaa kwa kiasi kwa vile yanathibitisha ukweli kwamba michezo ya watoto ni lazima ibobee raghba za watoto. Mfano mzuri ni

mchezo unaochezwa na watoto katika bunilizi ya Momanyi (2009) "*Mchezo wa Kobole*". Anatueleza kwamba "watoto wa madarasa ya chini waliimba na kucheza katika vikundi walivyounda wenyewe. Wale wa madarasa ya juu walicheza mpira…. Wale wa madarasa ya chini waliimba na kucheza michezo yao.Tofauti katika michezo hii ni umri na ulimwengu wanaoelewa. Ujumbe katika michezo yenyewe ni tofauti kutegemea  mwonoulimwengu wao.

Michezo ya watoto hufurahisha na kuchangamsha watoto sana kwa sababu huchekesha, hufunza juu ya maisha, humpatia mtoto madaraka katika hali ile na hali kadhalika hutoa adabu kwa wale wanaokosea jamii. Zaidi ya hayo, hufunza juu ya maisha, jinsi ya kuishi pamoja kama mtu mzima na kufunza kazi mbalimbali (Ojiambo, 2004).

**4.12 Dhima ya Mwingilianotanzu katika Bunilizi za Watoto**

Dhana ya mwingilianotanzu kama ilivyoelezwa na Senkoro (2011) na Macha (2013) ni kule kuingiliana na kutegemeana kwa tanzu. Yaani utanzu mmoja kupatikana ndani ya mwingine. Suala hili hujitokeza sana katika bunilizi za watoto maana mwingiliano huo una manufaa yake. Kwa mfano, Mnenuka (2010) alijadili jinsi ambavyo tamthilia inaweza kuingiliwa na matini za kidrama zinazotokana na mwandishi kuwavalisha uhusika mwingine wa kisanaa wahusika wa tamthilia na kuwapa nafasi ya kuigiza mchezo mwingine ndani ya tamthilia. Mwingiliano huu wa tamthilia ndani ya tamthilia unasadifu dhana ya mwingilianotanzu (Bakize, 2014). Mwelekeo huu wa Mnenuka (keshatajwa) ndio mwelekeo ambao tumeuchukua katika utafiti wetu kwa upande wa bunilizi za watoto. Mwingilianotanzu katika bunilizi za watoto una dhima anuai kama vile: Kudokeza maudhui, kuwawezesha watoto kupokea mambo mengi kwa wakati mmoja, kumwondoa mtoto katika ulimwengu wake halisi na kumweka

katika ulimwengu wa kifantasia, kujenga taharuki na kutambulisha utamaduni wa jamii husika.

### 4.13 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia lengo la kwanza ambalo ni kupambanua jinsi tanzu mahsusi zinajenga bunilizi teule za watoto. Bunilizi hizi ni kazi za kinathari ambazo huunda utanzu mkuu ambao vitanzu hujitokeza kwa lengo la kuchimuza maudhui husika kwenye kazi husika. Mwingiliano wa tanzu katika kazi za watoto huibua hamu ya mtoto kusoma kazi teule. Katika sura inayofuata, tutaangalia namna mwingiliano wa tanzu unachimuza maudhui katika bunilizi teule za watoto.

# SURA YA TANO

# NAMNA MWINGILIANOTANZU UNACHIMUZA MAUDHUI KATIKA BUNILIZI ZA WATOTO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii inaangazia lengo la pili. Lengo hili linajadili namna tanzu mahsusi zinaingiliana na kuchimuza maudhui katika bunilizi teule za watoto. Tanzu mahususi ni kama vile wimbo, shairi, sala, michezo ya watoto, picha na michoro, matumizi ya insha, barua, mazungumzo ndani ya bunilizi, nyimbo na hekaya katika bunilizi. Hapa, tunaeleza namna kwa pamoja tanzu hizi zinayaweka wazi maudhui kama vile utamaduni, uzalendo, ushirikiano na utangamano, ushujaa na maudhui mengine ambayo yamejadiliwa.

Bunilizi za watoto wa Kiafrika zina tanzu nyingi ambazo zinajitokeza ndani mwake. Hata hivyo, katika utafiti huu tulitumia tanzu chache tu zinazojitokeza katika bunilizi teule. Uchache huu ulitokana na uteuzi wa vitabu vya watoto vinavyopaswa kutumika. Katika kuangalia vipengele hivi, tuliongozwa na mhimili wa nadharia ya Mwingilianomatini kwa kuegemea kwa mtazamo wa Macha (2013) na Senkoro (2011) kuwa, kazi za kifasihi huwa na tanzu zingine ndani mwake zinazofanya zikamilike.  Ufaafu wa maudhui mbalimbali yanayochimuzwa na vipengele vya mwingilianotanzu kutoka kwa vitabu teule hufafanuliwa. Lengo hasa ni kuweka wazi masuala yanayomhusu mtoto Mwafrika katika mazingira yake.

## 5.1 Maudhui

Bunilizi za watoto ikiwemo fasihi zingine za watoto ni sanaa inayotumia lugha ili kuwasilisha ujumbe kwa jamii kuhusu jamii hususan watoto. Huwasilisha hali, maingiliano, mivutano na mikinzano miongoni mwa binadamu na mazingira yake. Fasihi hizi zinachibuka katika maisha ya binadamu ili kufungamana na malengo ya

mwandishi, hisia, fikra, mawazo, historia, utamaduni, na hata anasa yote yakiwa yanahusiana na jamii husika (Syambo na Mazrui, 1992).

Maudhui ni jumla ya masuala au mambo yanayoshughulikiwa katika kazi ya kifasihi. Ndiyo huendeleza na kukuza dhamira ya kazi hiyo ya kifasihi. Hujumuisha vipengele kadhaa vinavyoleta mahusiano na maingiliano na mbinu kadhaa ambazo ni pamoja na dhamira, itikadi, msimamo, maadili na falsafa ambavyo huchangizana na kukamilishana kuibua wazo la mtunzi kwa mkabala na muktadha fulani (Njogu & Chimerah, 1999; Masebo & Nyangwine, 2000; Wamitila, 2008; Ouma, 2013). Maudhui ni ujumbe unaozungumziwa na msanii. Ni kitu, mtu, jambo au tukio, sifa, mahali au hali ya maisha inayomzunguka. Katika ufafanuzi wake, Senkoro (1982) anayafafanua maudhui kama mawazo au mafunzo mbalimbali yaliyompa msukumo mtunzi au msanii wa kazi fulani hadi akaitunga kazi hiyo. Anayaona maudhui kama ujumbe wa msanii kwa hadhira yake. Maelezo zaidi yanatolewa na Msokile (1993) kuwa maudhui ni jumla ya mawazo, dhamira, msimamo, mtazamo, falsafa na ujumbe katika kazi ya fasihi.

Gataka (2012) anasema kwamba maudhui ni mawazo muhimu yanayoelezwa katika hadithi katika kazi ya fasihi na ambayo ni kioo cha jamii. Kutokana na mawazo hayo ya Gataka (k.h.j), jamii halisi huelezwa kupitia kazi ya fasihi yenye wahusika anuai wakiwakilisha binadamu katika uhalisia wao wa maisha.

Kwa jumla, maudhui kama kipengele cha kimsingi katika fasihi ya watoto, hufaa kuwa mepesi na ya wazi ili kueleweka na watoto. Aidha, maudhui haya yazingatie sana ukuaji wa mtoto katika jamii (Ngugi, 2011). Mawazo yanayowasilishiwa watoto na mtunzi wa mashairi bila shaka yatawaathiri hata katika maisha yao ya baadaye. Waandishi wengi wameibuka na kuandika mashairi yanayonuiwa kuwaonya

wanaowadhulumu watoto kwamba sheria imesimama kidete kuwalinda watoto. Masuala ambayo yanajitokeza katika bunilizi teule yanachunguzwa kwa kuyaegemeza kwenye uhalisia wa maisha katika jamii ili kubainisha jinsi yanawaathiri na kuwahusu wanajamii, hasa watoto.

Akoleit (1990) anasema kuwa katika vitabu vya watoto, kisa kinachozungumziwa kinapaswa kuonyesha ufanisi wa mtoto, vile kuonyesha thamani ya mtoto anayoipata anapoendelea kukua. Thamani hii hujumuisha mambo kama usalama, uhusika, mapenzi, uhuru, mabadiliko ya hali ya kimwili miongoni mwa mengine. Maudhui katika vitabu vya watoto aghalabu huakisi amali muhimu katika ukuaji wa watoto miongoni mwa mambo mengine jinsi itakavyodhihirishwa katika utafiti huu kwenye sehemu zinazofuatia. Amali hizi kama asemavyo Akoleit (k.h.j) hujumlisha mahitaji ya utotoni kama vile mapenzi, usalama na mafanikio.

Maudhui yaliyojadiliwa katika utafiti huu ni masuala ibuka yanayowaathiri watoto kama vile dini, haki za watoto, ushujaa, utamaduni, magonjwa, maadili na adabu, uzalendo, ushauri na nasaha, bidii na uvivu kazini, elimu na maarifa. Katika kuibua maudhui haya, waandishi wa bunilizi za watoto wametumia mbinu ya kimwingiliano tanzu ili ujumbe ujitokeze kwa namna ambayo mtoto anaweza kupata ujumbe kwa njia rahisi. Hivyo basi tuliangalia namna vipengele vya mwingilianotanzu vinaweza kuchimuza maudhui katika bunilizi za watoto.

### 5.1.1 Dini

Katika umri  mchanga, mtoto hana budi kufundishwa kuhusu sala maana sala hujenga mtoto kwa masuala ya kiroho yanayoambatana na dini husika. Katika jamii nyingi za Kiafrika, watu waliabudu miungu yao maana Mungu ni tumaini katika maisha.

Utanzu wa sala hapa umetumika kwa lengo la kuonyesha dini au imani inayokuzwa kwa watoto.

Dini ni imani katika kuwepo kwa Mungu au kiumbe mwenye nguvu zaidi ya binadamu. Dini huwa ni imani inayohusiana na mambo ya kiroho na kwamba kuna Mungu ambaye aliumba ulimwengu huu na ndiye mtawala wa kila kilichomo. Dini ni mfumo fulani wa imani na ni njia ya kuabudu, kusali na kuheshimu au kutii huyo Muumba kama wafanyavyo wakristo, waislamu na waumini wengine duniani. Kwa jumla, dini ni imani inayohusiana na mambo ya kiroho na ambayo humwongoza binadamu katika kutenda mabaya au mazuri ulimwenguni kulingana na imani anayoshikilia (Kiptum, 2017).

Maudhui ya dini yamejitokeza sana katika utanzu wa sala katika baadhi ya bunilizi hizi za watoto. Matundura (2008) ametumia mbinu hii ya sala ndani ya bunilizi kwa lengo la kuonyesha maudhui ya dini. Mfano, katika uk 2, ameeleza kwamba ‘Musa alishuka kutoka kitandani huku anayafikicha macho yake yaliyokuwa bado yamejaa usingizi na akapiga miayo. Alipiga magoti kando ya kitanda chake na kusema sala:

**20.** Baba yetu uliye mbinguni
Watazame wanao ulimwenguni
Tunaotapatapa maishani
Mayatima maskini…’ (uk 2)

Musa anamsihi Mungu aliye mbinguni, awatazame wanao walio ulimwenguni. Wana wanaorejelewa hapa ni yeye (Musa) na dada zake (Ukwa na Haki). Anamsihi Mungu awatazame wanaotapatapa maishani, yaani wasiokuwa na namna yoyote wa kujikimu.

Suala la sala hapa linaonyesha kwamba mtoto huyu anamfahamu Mungu na anaamini kwamba yeye ndiye atakayesimama kwa niaba ya wazazi wake. Kwamba, Mungu aweze kuwatazama na kuwaonea huruma mayatima kama yeye na dada zake Ukwa na Haki.

Katika uk 4, Matundura (keshatajwa) pia anatuonyesha kwamba "Ukwa alipohakikisha kwamba dada yake yuko tayari kwa maombi, alitoa kikohozi kooni na kwa sauti ya unyenyekevu iliyojaa ushawishi mkubwa akaomba:

**21.** "Mungu wetu wa haki
Shukrani kwa kumlinda Haki
Asante kwa yetu Siha
Shukrani kwa maisha
Asante kwa nyanyetu
Wahifadhi wazazi wetu
Mahala pema peponi
Tusaidie masomoni
Kila siku shuleni
Amina"

Katika jamii nyingi za Kiafrika, watoto hufundishwa kuwa na imani kwake Maulana. Hii hutokana na ule Uafrika wenyewe katika tamaduni zao za kuabudu miungu yao. Suala hilo la kuamini kwa miungu hurithishwa kwa watoto wao. Ukwa amemtambua Mungu kuwa ni wa haki na ameweza kumshukuru Mungu kwa kumlinda dadake na bila shaka kakake. Pia ametoa shukurani kwa Mungu kwa afya njema na ulinzi wa nyanyake. Ukwa pia amemsihi Mungu awaweke wazazi wake mahala pema peponi.

Katika uk 17, ubeti wa kwanza, kuna wimbo wa taifa ambapo unaotambulisha uwepo wa Mungu. Wimbo huu wa taifa huimbwa kabla ya shughuli ya shule kuanza rasmi katika ulimwengu wa masomo kwa mtoto mdogo. Nandwa (2013*)*, katika *Kito Apepeta* ametuonyesha wimbo huu wa taifa (uk 10). Utanzu huu wa wimbo ndani ya simulizi umechimuza maudhui ya dini kwa msomaji.

**22.** "Ee Mungu nguvu yetu
Ilete Baraka kwetu
Haki iwe ngao na mlinzi
Na tukae na undugu Amani na uhuru
Raha tupate na ustawi." (uk 10)

Ujumbe kwenye wimbo huu wa taifa ni kwamba, Mungu ni mwenye nguvu. Unamsihi Mungu alete Baraka na haki iwe ngao na mlinzi wao. Ombi hili linawasihi

watu wakae kwa undugu na waishi kwa Amani na uhuru. Ndiposa wangepata raha na amani.

Hapa kuna sala ndani ya wimbo kwenye simulizi. Wimbo wenyewe ni sala maana unaomba Mungu mwenye nguvu aweze kuleta Baraka na ulinzi katika jamii. Mtoto wa Kiafrika bila shaka atafahamu kwamba, Mungu ndiye huleta amani na mafanikio katika nchi wanamoishi.

Namlola (2019) katika *Hidaya* ametumia utanzu wa shairi katika simulizi yake kwa lengo la kuchimuza maudhui ya dini. Katika ubeti wa kwanza, msimulizi amemtambua Mola kuwa ni mwenye uwezo hasa kutokana na changamoto ambazo mwanawe alikuwa anapitia. Mama Pembe alikumbuka:

**23.** “Mola aliloamuwa, mja hana upinzani,
Ndilo litakalokuwa, hata mja afanyeni,
Ni kama ganda la muwa, lilotupwa ardhini. (uk. 21)

Shairi hili linasisitiza kwamba, Mola akishakupangia kitu, hakuna binadamu anayeweza kupinga. Hapa, alikuwa anamrejelea mwanake Hidaya kwamba, ikiwa ulikuwa mpango wa Mungu kwa mwanawe kumaliza masomo yake, basi, ingekuwa hivyo. Linasisitiza kwamba lililopangwa litabaki kuwa hivyo na hakuna atakayepinga, maana ni kama ganda la muwa linalotupwa ardhini baada ya kuliwa.

Kutokana na ombi hili, wote walipata matumaini kwamba wangeshinda katika jaribio hilo baada ya kutambua uwezo wa Mungu wao.

### 5.1.2 Maadili, bidii na utiifu

Maadili ni mwenendo wa kuwatendea watu kwa namna inayokubalika na wengi unaotokana na mafundisho, maelekezo na marekebisho mema (TATAKI, 2013; BAKITA, 2015). Kila jamii huwa na tabia ambazo hazikubaliki miongoni mwa

binadamu. Iwapo mtu anawaheshimu wenzake na kuwatendea utu na wema, basi mtu huyo ni mwadilifu. Kila mtu anastahili kuwatendea haki wenzake kwa kuwafanyia mambo yasiyowaudhi (Ngugi, 2018).

Uadilishaji wa mtoto ni mchakato wa kumrekebisha, kumkarabati na kumuumba mtoto kitabia, kiutambuzi, kiakili na kifalsafa ili aweze kuyatenda mambo yanayokubalika katika jamii kuwa ni mazuri au yanayoendeleza maadili (Ekiru, 2018). Ekiru (k. h. j) anaendelea kusema, jamii adili inarejelea jamii inayozingatia maadili ya Kiafrika au jamii yenye kuzingatia haki na usawa jinsi inavyotambuliwa na Mwafrika. Hivyo, mtoto Mwafrika alikuwa anafundishwa kuwa na maadili mema katika jamii tangu akiwa na umri mdogo.

Zipo faida nyingi za adabu na maadili ambazo watunzi wanasisitiza katika bunilizi za watoto. Hizi ni pamoja na ufanisi shuleni na kutii kila mtu bila kujali umri. Katika kufanikisha ujumbe wa kuwataka watoto wawe waadilifu, watunzi wanapitisha ujumbe huo kupitia masimulizi yaliyoko kwenye tanzu mbalimbali ndani ya usimulizi wenyewe. Hili linafanywa kimakusudi ili kumwezesha mtoto apate kukuza maadili katika ule mchakato wa kusoma bunilizi zao. Anavyosema Ngugi (2009) ni kwamba watoto husoma ili waweze kupata kukuza kipawa chao cha lugha, kuimarisha ubunifu wao pamoja na kujiepusha na tabia hasi. Matundura (2008) katika *Sitaki Iwe Siri,* amedhihirisha ubunifu wa Musa kupitia utunzi wake wa insha ulioshinda katika ushindani wa Kimataifa.

Elimu ya kujua kusoma na kuandika ni muhimu sana katika kupambana na maisha. Dunia ya leo inahitaji watu wenye ujuzi wa mambo mbalimbali. Ujuzi huu hupatikana kwa kusoma vitabu, makala, majarida na maandishi mengineyo. Kupitia kwa elimu, watoto hujifunza mambo mengi yanayowahusu ambayo wasingepata katika mazingira

ya nyumbani. Hali kadhalika, watoto wanaozaliwa katika jamii isiyojiweza na kuwajibika husaidika sana kupitia maadili yanayofundishwa shuleni.

Mbinu ya barua ndani ya bunilizi imetumika kwa lengo la kudokeza suala la utiifu. Utiifu ni jambo linalosisitizwa sana katika jamii na hasa katika ulimwengu wa mtoto. Watoto wanapotii wakuu wao, huepukana na changamoto ambazo zinaweza kuwakumba katika maisha yao. Hata hivyo, kutotii kunaweza kusababisha matokeo mabaya katika maisha ya mtoto, hivyo basi wazazi au walezi wana majukumu mengi ya kuwakumbusha watoto kila uchao kuhusiana na matendo mabaya.

Nandwa (2016) katika bunilizi yake *Mchezo wa mtelezo,* anawaonya watoto kupitia kwa barua ya mwalimu Juma. Mwalimu Juma alikuwa amemwandikia babake barua hiyo ili kumwomba msamaha kwa kutotii agizo la kushiriki katika mchezo wa mtelezo. Kilichotokea baada ya yeye kutotii ni kwamba mfupa wa kisigino chake ulivunjika na ndipo akawa anachechemea. Hii ilikuwa adabu itokanayo na kutotii.

**24.** Kwa baba,

> "Baba, nimebaki nikijuta nikikumbuka kuwa nimeua ndoto yangu ya kuwa mwanasoka. Daktari amesema mfupa wa Kisigino umevunjika na sitawahi kutembea kama kawaida…" (uk.19)

Barua hiyo iliwafaa sana akina Lulu na Brayo maana hawakuwa wametii amri ya kupeleka ujumbe kwa wazazi wao jinsi walivyokuwa wameelezwa na mwalimu mkuu. Badala yake, walikwenda kushiriki mchezo hatari wa mtelezo kwenye bonde la mauti. Sababu kuu ya mwalimu Juma kumpa Lulu barua hiyo aisome tena kwa sauti ni kwamba alitaka iwe funzo kwa watoto hawa ili wasije wakapatwa na janga kutokana na mchezo huo. Tena alitaka ahimize suala la utiifu kwa watoto hawa.

Syokau (2018) katika *Kade na Katana* katika utanzu wa mazungumzo ndani ya bunilizi ameonyesha suala la maamkuzi na heshima kwa watu wakubwa. Masuala

kama shikamoo, naomba, na samahani ni maneno ya heshima ambayo mtoto yeyote katika jamii anapaswa kutumia anapotangamana na watu wazima:

**25.** ***Katana:*** *Shikamoo Nyanya?*
***Nyanya:*** *Marahaba……*
***Katana:*** *Naomba nikusaidie…*
***Nyanya****: ……(uk. 14)*

Suala la maamkizi hapa ni muhimu sana hasa watoto wakifundishwa na kutambua jinsi ya kuamkuana na watu wazima. Maamkizi katika tamaduni za Kiafrika hutegemea tamaduni husika. Mfano katika jamii ya Kimaasai hapa nchini Kenya, inasemekana kwamba wao hutoa salamu zao kutegemea hadhi ya mtu katika jamii hiyo. Kwamba inategemea kama mtu ni mtoto, ametahiriwa ama bado, msichana au mvulana, mke mdogo au mke mzee na masuala mengine yanayoangaliwa katika jamii hiyo (Hodgson, 1999). Nadharia ya Uoniafrika inasisitiza kwamba, mtoto Mwafrika lazima ahusishwe na masuala yanayomhusu kwa hivyo, suala la maamkizi katika bunilizi ni suala ambalo mtoto analifahamu kutokana na tamaduni zao na inabidi akumbushwe njia ya kuamkua wakubwa wao kupitia kwa bunilizi zao.

Utanzu huu pia wa mazungumzo ndani ya simulizi unadokeza suala la maadili na adabu baina ya watoto wakiwa na wakuu wao. Mazungumzo haya yanafundisha mtoto jinsi ya kuwasiliana na watu wazima wanapojumuika pamoja. Hali kadhalika, watoto wanapaswa kuwa na adabu njema wakiwa na wakuu wao na hata kuwasaidia wakiwa na changamoto. Katika ukurasa wa 14, Syokau (2018) *Kade na Katana,* ajuza yule anamuonya Katana kwamba ‘Niendako ni mbali..’ lakini Katana alikuwa tayari kumsaidia ajuza huyo.

Syokau (keshatajwa) pia ametumia utanzu wa ndoto kwenye hadithi katika kudokeza suala la maadili. Msimulizi anaeleza kwamba, “Kade akamwotea ndugu yake akitoka matembezi yake. Badala ya fujo zake za kawaida, alizokuwa maarufu kwazo,

akaamua kuwa mnyenyekevu na mpole kwa nduguye…" (uk. 26). Ndoto hii ilitokana na uhusiano mbovu kati ya ndugu hawa wawili Kade na Katana. Hii ilitokana na kutofanana kimaadili. Katana alikuwa mwingi wa maadili ilhali nduguye Kade alikuwa kinyume. Funzo hapa ni kwamba, mtu anaweza kuwa na ubaya wa kila aina lakini anaweza kubadilisha mienendo yake na kuwa mtu mwema. Mtu anapokuwa mwema, anapaswa kukubaliwa katika jamii jinsi Katana alivyomkubali nduguye ingawa kwa tahadhari kwa sababu mtu mwingine anaweza kubadilisha mienendo yake akiwa na lengo fulani. "Katana hakuelewa hasa sababu yake Kade kubadilika sana hivyo…" (uk 27). Kade alikuwa na lengo la kuiba mkufu wa Katana ili aweze kutajirika kama alivyosema.

Katika uk 34, Kiongozi Bidii ambaye ni Kade aliandika barua akiomba atafutiwe dawa. Hii ni baada ya kupata ugonjwa ambao haukuwa unatibika. "Akaandika barua kwa manaibu wake ili waje kumwona ili kutafuta suluhisho" (uk 33).

**26.** *Kwa naibu wangu,*
"*Ninaandika barua hii kwa nia ya kuomba usaidizi wako wa kutafutiwa dawa. Nimekuwa nikiugua kwa siku kadhaa sasa bila kupata nafuu……" (uk. 34).*

Kinaya hapa ni kwamba, kiongozi huyu hakuwa akitaka watu wakaribie ikulu yake wakati alipokuwa na afya njema. Watu walipotaka usaidizi wake walipokuwa wagonjwa, aliwaambia "Mimi sio daktari. Nyumba yangu sio hospitali. Ondokeni! Sitaki mlete viroboto na kunguni katika nyumba yangu" (uk. 32). Funzo hapa ni kwamba hamna haja ya kiburi mtu anapopata mali kwa sababu maisha ni kusaidiana katika jamii.

Utanzu wa sala ndani ya bunilizi pia umechimuza maudhui ya maadili katika ndoa. Katika hali halisi ya maisha, suala la ndoa linahitaji uaminifu. Mmoja anapokiuka makubaliano ya uaminifu, migongano hujitokeza na hata ndoa kuvunjika. Kando na

ndoa hiyo kupata matatizo mengi, athari yake ni kuacha watoto kuwa mayatima na kuwepo na umaskini usiopigiwa mfano. Kulingana na Matundura (2008), Yusufu Matano huenda hakuwa mwaminifu katika ndoa, ndiyo maana aliweza kumwambukiza mke wake ugonjwa wa UKIMWI uliosababisha maafa na kuwafanya watoto wao kuwa mayatima.

Hali kadhalika, watu katika jamii hufundishwa jinsi ya kuzingatia maadili kwa kuepukana na tamaa na starehe zinazozidi mipaka. Tamaa na starehe zinaweza kusababisha janga la UKIMWI na matokeo yake ni kuacha watoto mayatima kwa wanandoa na umaskini uliokithiri kwa waathiriwa. Kupitia kwa utanzu wa sala waliusali mayatima, ulimfanya Mwalongo nyanya wa mayatima kuwaza kuhusu ugonjwa uliosababisha kifo cha wanawe. Matundura (2008) anasema 'Afya zao zilizidi kudhoofika. Wakakonda kama ng'onda na macho yao kuwaingia ndani. Mbavu zao zikaweza kuhesabika" (uk. 9).

Matumizi ya hekaya pia yamechimuza maudhui ya maadili na bidii kazini. Bunilizi za watoto huweza kutumiwa kuwaelimisha watoto kuhusiana na majukumu yao pindi watakapokuwa watu wazima. Huwa ni njia ya kuwaelimisha ili kuwaandaa kukabiliana na changamoto za maisha yao ya utu uzima. Kupitia kwa mafundisho hayo, ugumu wa maisha ya utu uzima yanaweza kuwasilishwa kama njia ya kufahamisha watoto kwamba wazazi wao hukabiliana na changamoto chungu nzima kuwalea (Gitonga, 2017). Syokau (2018) katika *Kade na Katana* kupitia hekaya aliyosimulia nyanyake Kibibi ilionyesha jinsi Katana aliweza kufanya bidii ili kuokoa familia yake kutokana na umaskini uliokuwa umekithiri.

Kwa upande mwingine, kuna wahusika ambao ni wavivu na walafi katika hekaya. Sifa hii inakemewa sana katika jamii nyingi za Kiafrika. Uvivu unasababisha tamaa

na ulafi wa mali. Katika hekaya, tunaelezwa kwamba Kade nduguye Katana alikuwa kinyume cha nduguye kitabia. Kade alikuwa "mtundu, kijana asiyeambilika, mvivu.." (uk. 7). Uvivu wake unazaa wivu dhidi ya kakake kiasi cha kupanga njama za kumdhuru. Tamaa yake inampelekea kuiba mkufu ambao Katana alikuwa amepewa na ajuza.

### 5.1.3 Umaskini

Umaskini ni hali ya ukosefu wa mahitaji ya kimsingi ya binadamu kama vile chakula, maji, usalama, mavazi, nyumba na huduma za afya kutokana na uwezo wa kununua (TUKI, 2004). Ulitima ni udhaifu wa maisha unaotokana na shida kuu za kiuchumi. Kuna umaskini utokanao na kifo na kuna umaskini utokanao na matatizo ya binadamu.

#### 5.1.3.1 Umaskini Utokanao na Kifo

Katika uandishi wa bunilizi za watoto, watunzi wanapaswa kuelimisha mtoto kuhusu chanzo cha umaskini kupitia kwa kazi zao na vilevile, jinsi ya kutatua suala la umaskini. Kuna umaskini unaotokana na uyatima ambapo, mayatima wanaachwa bila chochote cha kujikimu kwa maisha yao.

Matundura (2008) katika *Sitaki Iwe Siri* kupitia utanzu wa sala, Musa na dada zake wanamsihi Mungu awakumbuke mayatima wanaotapatapa maishani. "Mayatima maskini" (uk. 2). Umaskini unaorejelewa hapa ni wa ukosefu wa wazazi unaosababisha upweke. Hii ni kwa sababu watoto hawa hawakosi kitu maana wanapata lishe, mavazi na hata elimu lakini bado wanasumbuliwa na kiini cha kifo cha wazazi wao. "Kwa nini tunaishi pekee yetu? Wazazi wetu walikwenda wapi?" (uk. 7). Huu ni upweke.

Katika maelezo yake Matundura, inaonekana kwamba nyanya Mwalongo hakuwa na wana wengine baada ya kifo cha mwanawe Yusufu na mkaza mwanake Honorata. Kifo cha wana hawa kilimfanya nyanya huyo kuwa maskini wa watoto katika miaka hizo zote, aliwaza kuhusu “maneno katika sala ya Haki na Ukwa akisema “wahifadhi wazazi wetu mahala pema peponi” (uk.10)

**5.1.3.2 Umaskini Utokanao na Changamoto za Maisha**

Syokau, (2018) katika *Kade na Katana* ameonyesha umaskini katika simulizi yake ya katika hekaya ndani ya hadithi. Ameelezea kuhusu Katana na familia yake kuwa walikuwa maskini hohehahe. “familia yake ( ya akina Katana) ilikuwa inajulikana kwa umaskini wao. Yaani umaskini wao haukujificha” (uk.7). Yaani wazazi wake walikuwa wazee na hawakuwa na kazi au riziki yoyote ile. Kutokuwa na riziki hapa ina maana kwamba mahitaji ya kila siku ilikuwa shida kupata. Hii ilimfanya Katana aliyekuwa” maskini wa mali; tajiri wa maadili mema na mpenda watu” (uk.7). Kuamua kubadili maisha yake na jamii yake kutokana na dharau waliloonyeshwa kila walipopita ilimkera na kumuudhi. Angeweza kufanya lolote ili ainue familia yake kifedha. Huu ni umaskini.

Namlola (2019) katika hadithi yake *Hidaya* amedhihirisha umaskini kupitia kwa utanzu wa shairi lililohusiana na suala la ndoa ya lazima. Shairi hili alilokumbuka mama Pembe, liliweza kumtia moyo mwana wake Hidaya ili aweze kukabiliana na changamoto alizokuwa anazipitia. Inaonekana kwamba bwana Matata, babake Hidaya alikuwa anataka amwoze bintiye kwa bwana Mapesa kwa sababu ya kuhepa changamoto za umaskini. Suala la ndoa za mapema hufanyika sana katika mazingira wanamoishi watu maskini kwa sababu ya ukosefu wa pesa za kuelimisha mtoto maskini au tamaa ya mali katika jamii isiyokuwa na mipango kabambe kuhusu mtoto mwanamke.


Matumizi ya picha na michoro katika bunilizi za watoto hutumiwa na waandishi kwa lengo la kuweka wazi kilichozungumziwa. Watoto katika kiwango kile cha daraja la tatu hupenda picha ingawa katika bunilizi zao picha ni chache ikilinganishwa na kikundi cha daraja la kwanza. Sababu ni kwamba, katika kiwango kile cha daraja la tatu, watoto wameanza kuelewa kile ambacho wanakisoma. Waandishi wa bunilizi teule wametumia picha ndani ya bunilizi kwa lengo la kuchimuza maudhui kadhaa yakiwemo umaskini, haki za watoto, utamaduni, uzalendo, miongoni mwa mengine

Syokau (2018), katika bunilizi yake *Kade na Katana* ametumia utanzu huu wa picha ndani ya bunilizi kwa lengo la kusisitiza suala la umaskini katika jamii. Mfano katika ukurasa wa 14, kuna picha inayoonyesha Katana akizungumza na yule ajuza. Mavazi yake yaliyojaa viraka vya aina mbalimbali yanadhihirisha umaskini uliokithiri.



**Mchoro 1: Katana akiwa na ajuza**
**Chanzo: Syokau (2018). '*Kade na Katana' (uk.14)***

Pia katika ukurasa ukurasa 11, Katana anaonekana pembeni akielekea uvuvini. Ukimlinganisha na wavuvi wenzake, mavazi yake na umri ule wake mchanga unathibitisha kwamba, yeye alitoka katika familia maskini.



**Mchoro 2: Katana akielekea uvuvini**
**Chanzo: Syokau (2018). 'Kade na Katana' uk. 11**

### 5.1.4 Magonjwa

Magonjwa ni moja ya changamoto zinazokumba jamii. Mwaka wa 2002, Wizara ya Elimu nchini Kenya kupitia Taasisi ya Elimu iliunda mtaala mpya katika Kiswahili (Ministry of Education, 2002) ulipendekeza mafunzo ya Kiswahili yahusishe fasihi katika viwango vyote. Hii ni kwa sababu masuala ibuka yanayoathiri watoto na vijana kwa njia mbalimbali yalipaswa kushughulikiwa. Masuala ibuka yaliyopendekezwa ni pamoja na magonjwa hususan ugonjwa wa UKIMWI miongoni mwa masuala mengine (Ngugi, 2018).

Watoto walijuzwa kuhusu maendeleo ya jamii zao kwa njia ya fasihi. Papo hapo, ujenzi wa mazoea ya kusoma miongoni mwa watoto huwekewa mkazo ili

kuwaonyesha kuwa usomaji wa vitabu vya fasihi unaweza kuwapa burudisho la kutosha (Ministry of Education, 2002).

Katika kuangalia suala hili la magonjwa, kipengele cha barua ndicho kimechimuza maudhui haya ya ugonjwa. Waandishi wa bunilizi teule ( *Kade na Katana* ( syokau, 2018) , *Sitaki iwe Siri* ( Matundura, 2008) wametumia mbinu ya barua kwa sababu ilikuwa njia mojawapo ya kupitisha ujumbe. Kabla ya teknolojia ya kisasa, watu walikuwa wakiandika barua na kuweka kwenye bahasha na kutia stempu kabla ya kutuma kwa posta kwa mwandikiwa. "Nyanya alikubali kumpatia Musa pesa za nauli ya kwenda hadi mjini ilikokuwa posta pamoja na pesa za kununulia bahasha na stempu" (Matundura, 2008:50). Kulingana na waandishi hawa, inabainika kwamba, magonjwa hayo yana visababishi vyake.

#### 5.1.4.1 Ugonjwa utokanao na ushirikina

Kea (2013), katika *Msiba wa kujitakia* ametuonyesha jinsi magonjwa yanavyoweza kuathiri jamii kupitia utanzu wa ushairi mwishoni mwa usimulizi. Anajaribu kuonyesha jinsi ugonjwa unavyoweza kusababisha matanga na kwamba watu huomboleza tukio hilo likitokea. Mwandishi anasema kwamba mama Katana alipatwa na ugonjwa ambao mumewe aliuita 'kuruka' ambao ungetibiwa tu kwa uganga jambo ambalo jamii hiyo haikukubali. "Mtu akiiruka hafai kunywa maji" (uk. 29). Katika ubeti wa kwanza tunasoma:

**27.** "Matanga ni kwomboleza, ifikwapo na mashaka
Matanga pia yaliza, machozi yakaanguka
Matanga yanatatiza, mtu tama akashika
Matanga mbali pitia, mkosi usitutie" (uk. 29)

Shairi hili ndani ya bunilizi linaonyesha masikitiko na hofu itokanayo na ugonjwa huo.

Maelezo mengi kuhusu magonjwa yanajitokeza kupitia utanzu wa barua. Syokau (2018), katika *Kade na Katana* ameonyesha jinsi ugonjwa ulivyomwathiri kiongozi Bidii ambaye ni Kade kuwa lilikuwa tatizo. Hii ilimfanya kiongozi huyo kuandika barua akiomba usaidizi kwa wote. Aliahidi mali nyingi kwa yeyote ambaye angeweza kumtibu maana uhusiano wake na watu wengine ulikuwa ni duni mno.

> **28.** "Kwa naibu wangu,
> Ninaandika barua hii kwa nia ya kuomba usaidizi wako wa kutafutiwa dawa. Nimekuwa nikiugua kwa siku kadhaa sasa bila kupata nafuu" (uk. 34).

Ujumbe katika barua hii ni kwamba, Kade alikuwa akiomba usaidizi wa kutafutiwa dawa. Kulingana na barua, anasema kwamba, alikuwa ameugua kwa siku kadhaa bila kupata nafuu.

Barua hii imeandikwa kwa lengo la kuchimuza maudhui ya magonjwa katika bunilizi za watoto. Hali kadhalika, barua hii ilihimiza kwamba, ujirani mwema ni uti wa mgongo katika jamii yoyote ile.

Kinaya hapa ni kwamba, kiongozi huyu hakuwa akitaka watu wakaribie ikulu yake wakati alipokuwa na afya njema. Watu walipotaka usaidizi wake walipokuwa wagonjwa, aliwaambia "Mimi sio daktari. Nyumba yangu sio hospitali. Ondokeni! Sitaki mlete viroboto na kunguni katika nyumba yangu" (uk 32). Funzo hapa ni kwamba hamna haja ya kiburi mtu anapopata mali kwa sababu maisha ni kusaidiana katika jamii. Kwa hivyo, barua hii pamoja na simulizi na hekaya zinachimuza maudhui ya ushirikiano miongoni mwa wanajamii.

### 5.1.4.2 Ugonjwa utokanao na kutotii

Utiifu ni jambo linalosisitizwa sana katika jamii na hasa katika ulimwengu wa mtoto.Watoto wanapotii wakuu wao, huepukana na changamoto ambazo zinaweza

kuwakumba katika harakati zao. Hata hivyo, kutotii unaweza kusababisha matokeo mabaya katika maisha ya mtoto; hivyo basi, wazazi au walezi wana jukumu la kuwakumbusha watoto wao kujiepusha na matendo mabaya.

Katika *Mchezo wa mtelezo* (Nandwa, 2016), mwalimu Juma alifichua siri yake kuhusu kilichomfanya achechemee. Kutokana na barua aliyeimba Lulu pamoja na Brayo, chanzo cha ulemavu wake kilidhihirishwa.

**29.** “Kwa baba,

> ………………………..Baba, nimebaki nikijuta…Daktari amesema mfupa wa kisigino umevunjika na sitawahi kutembea kama kawaida wala kucheza mpira…” (uk 19)

Mwalimu Juma alikuwa amemwandikia babake barua akimjuza kwamba alikuwa anajuta. Daktari alikuwa amemwambia kuwa mfupa wa kisigino ulikuwa umevunjika”. Matokeo ni kwamba, hangeweza kutembea kama kawaida wala kucheza mpira. Hii ilikuwa ni dhihirisho kuwa tayari alikuwa amelemaa. Ulemavu huu ulitokana na kutotii wazazi wake.

### 5.1.4.3 Ugonjwa wa Ukimwi

Tangu kugunduliwa kwa UKIMWI katika miaka ya 1980, mkabala ambao umechukuliwa na wanajamii wengi umekuwa ni wa kulaumu, kukashifu, kunyanyapaa na kuwabagua watu wenye virusi vya Ukimwi au wale wanaohusiana nao (Kinara, 2012). Vile vile suala la ukimwi lilizungumziwa kwa mkabala wa vitisho uliotamalaki mno hasa katika miaka ya themanini (Njogu, 2007). Muhimu ni kwamba, wanajamii wanaendelea kuhamasishwa kuhusu namna ya kukabiliana na maradhi haya, wakiwemo waandishi wa hadithi mbalimbali (Mutembei, 2009).

Kutokana na namna watoto huathirika kutokana na janga la ukimwi, hadithi mbalimbali zimeandikwa kuhusu janga la ukimwi na athari zake kwa wanajamii kwa

njia ya kuwapa wanajamii mafunzo mbalimbali kuhusiana na janga hili (Ngugi, 2018).

Uandishi wa insha ni mojawapo wa muktadha wa fasihi zinazofundishwa shuleni. Uandishi huu humpa mtoto uzoefu wa kuweza kujieleza kuhusu mambo ambayo yanamzingira. Kimaandishi watoto wanafundishwa kuandika kuhusu masuala ibuka na hali kadhalika masuala yanayowazunguka kama vile ukulima, umuhimu wa miti na kadhalika. Mtoto wa Kiafrika bila shaka anaweza kuandika kuhusu masuala hayo maana yanahusu mambo ambayo wanayaelewa na wanakumbana nayo kila siku.

Matundura (2008) katika *Sitaki Iwe Siri,* amepitisha ujumbe huu kupitia kwa mbinu ya insha ndani ya usimulizi. Kutokana na uandishi huu wa insha, Musa alitoa maelezo kuhusu ugonjwa hatari wa UKIMWI uliomvamia Yuri hadi kusababisha kifo chake. "Aliposhiriki katika mhadhara vilevile, aliweza kufafanua chanzo na jinsi ya kuepukana na ugonjwa huo. Musa aliandika vidokezo kuhusu mtungo wake na kumpelekea Bi. Rosa Mistika kwa ushauri zaidi." (uk. 44).

**30. SITAKI IWE SIRI**

> *"Yuri alianza kuepukwa na marafiki zake anavyoepukwa mgonjwa wa maradhi hatari kama Ukoma.*
>
> *Msichana huyu aliyeshangiliwa na kuonewa staha na kila mwanamume na hata wasichana wenzake kumuonea gere. Alianza ghafla kupungukiwa mikono. Hakuna hata mtu mmoja aliyetaka kumsalimia kwa mkono kwa kuhofia kuambukizwa maradhi…(uk. 45.)*

Utanzu huu wa insha ndani ya bunilizi ulichimuza maudhui ya ugojwa wa UKIMWI ambao ulikuwa siri katika jamii hiyo.

### 5.1.5 Ushiriakiano na Utangamano katika jamii

Kwa mujibu wa Akoleit (1990), utangamano wa kitaifa unahusu uhusiano mzuri wa kijamii uliojengwa juu ya mhimili mkuu wa imani. Hoja hii inatuelekeza katika kuzingatia kile ambacho kinaweza kukuza na kudumisha umoja miongoni mwa

wanajamii. Umoja huo hukuzwa tangu utotoni kupitia michezo ya watoto na uimbaji wa nyimbo. Muge (2018) anatoa ufafanuzi kwamba, ili mti unawiri vyema, sharti utiliwe maji na kuwekwa virutubishi vya kutosha. Mti kama huo, anasema Muge utastahimili changamoto za kiangazi na utaendelea kukua itakikanavyo. Anachomaanisha Muge hapa ni kwamba, mtoto anayepata mahitaji ya kutosha, hatakuwa na wakati mgumu katika kukabiliana na changamoto za utu uzima.

Muge (Keshatajwa) anaendelea kusema kwamba, mtoto aliyekuzwa vyema hutangamana na wenzake bila matatizo mengi. Umoja na mshikamano huu haujali lugha au kabila jinsi tunavyouona katika wimbo wa *Apepetanga* na *Mchezo wa Mtelezo* (Nandwa, (2013) na 2016) mtawaliwa. Hii ni kwa sababu watoto hujua tu kuwa wenzao ni watoto kama wao bila kuzingatia iwapo wanatoka katika jamii tajiri au maskini, wanasema lugha moja au tofauti, ni weupe au weusi, jinsia, miongoni mwa mambo mengine. Utangamano wa aina hii hukuza umoja na uwiano miongoni mwa watoto na wanajamii.

Stebbing, (1999) akirejelewa na Nyoni na Nyoni (2013) anasema kuwa lengo kuu la michezo ya watoto ni kuwawezesha kushirikiana na wenzao kila wanapotangamana na kuwawezesha kuungana na wanajamii wenzao. Kuwashirikisha watoto katika shughuli za kijamii hutiliwa mkazo na mfumo wa elimu hivi kwamba elimu huwa daraja muhimu la kuunganisha nyumbani na shuleni (Ngugi, 2011). Jambo hili huwa muhimu kwa kuwawezesha walimu kufundisha masuala kutoka kwa wanayoyafahamu watoto kabla ya kuingiza masuala mapya katika ufundishaji wao. Kutokana na hayo, wanayoelewa watoto, mwalimu hujenga msingi wa ufundishaji wake kwa kuwa ni njia mwafaka wa kufundisha watoto kuanzia yale wanayoyajua na kuingia kwa mapya. Hii huwasaidia kujenga uwezo wa kujiamini kama wanafunzi. Nyimbo na michezo ya watoto katika hali hii huwachochea watoto kukua haraka

katika utambuzi wa masuala fulani katika jamii kwa kuwapa fursa kutumia wanayoyajua kujifunza wasiyoyajua.

Nandwa, (2013) katika *Apepetanga,* anatueleza kwamba, nyimbo za watoto zilizotumiwa huwa urithi muhimu wa utamaduni, lugha, mila na thamani za kijamii. Katika wimbo *Apepetanga*, Kito aliongoza uimbaji wa wimbo huo kwa lugha ya Kiluhya, mojawapo ya lugha za kiasili nchini Kenya. Kulingana na jinsi mwandishi ametumia picha kuonyesha jinsi watoto walivyochangamkia wimbo huo, ni kama kwamba watoto hao wanaifahamu lugha hiyo au huenda hawaielewi lakini cha muhimu hapa ni urudiaji unaoambatana na wimbo wenyewe. Kando na kuwa na lengo la kuburudisha, wimbo hujenga muktadha na mazingira ambayo ari na hamu ya mtoto hufufuliwa ili kutalii na kuuchunguza ulimwengu wake anamoishi (Ngugi, 2011). Ninaunga mkono mawazo ya Ngugi, (2011) kwa kuwa, watoto hutangamana na kushirikiana pamoja bila kujali jamii au utamaduni wao na hivyo kutambua ulimwengu wao wa uhalisia. Katika *Apepetanga* ( Nandwa, 2013:20), utangamano huu wa watoto huonekana pale ambapo mwandishi ametumia picha kuonyesha jinsi watoto hawa wamepewa ruhusa na mwalimu wachague nyimbo ambazo wangemwimbia mgeni wa heshima.



**Mchoro 3: Watoto wakitangamana na kushirikiana katika kuchagua wimbo**
**Chanzo: Nandwa (2013)**

Syokau, (2018) *Kade na Katana* katika mbinu ya hekaya ndani ya hadithi, ameonyesha jinsi watoto wanaweza kushiriki pamoja. Kwenye hekaya, nyanyake Kibibi amewasimulia watoto wale hadithi iliyokuza suala la ushirikiano katika jamii na familia na pia kuonyesha athari za kutoshirikiana katika jamii hiyo ya Wema. Kade na Katana hawakushirikiana katika kuinua uchumi wa familia yao. Hii ni kwa sababu wazazi wao walikuwa wazee sana na hawakuwa na riziki. Badala yake, Katana ndiye aliyeonekana kutia bidii kuwatunza ndugu na dada zake. Kade kwa upande mwingine alikuwa mzembe na kujawa na wivu. Matendo yake mabaya yalimfanya kuwa mwizi na baadaye akapatwa na ugonjwa uliokosa tiba. Mwandishi anatueleza kwamba, Kade alijutia matendo yake yalitokana na kutoshirikiana na jamaa na jamii.

Hali kadhalika, Syokau (2018) katika *Kade na Katana* ametumia utanzu wa barua mwanzoni mwa bunilizi yake. Msimulizi anasema, “Nyanya naye alikuwa ameniandikia barua akinisihi nimtembelee.” (uk. 2).

**31.** Mjukuu mpendwa Kibibi,

Salamu chekwachekwa kama mchanga wa bahari kutoka kwangu……..madhumuni ya kukuandikia barua hii ni kukuomba uje nyumbani angalau tuonane macho kwa macho. Ndugu zako wanakuulizia….

Ni mimi bibi yako,

Zambarau Kajaza ( uk. 2).

Katika barua hii, Zambarau Kajaza alikuwa ametuma salamu nyingi alizolinganisha na mchanga wa bahari. Madhumuni ya barua hiyo ni kumuomba Kibibi mjukuu wake aende kumtembelea angalau waonane macho kwa macho. Pia amemjuza Kibibi kwamba ndugu zake walikuwa wanamuulizia.

Barua hii ndani ya bunilizi imetumika kwa lengo la kuchimuza maudhui ya utangamano katika jamii. Katika jamii za Kiafrika, watu walitangamana kwa njia moja au nyingine na hasa utangamano ule wa watoto na nyanya zao ulikuwa unaenziwa na jamii. Hii ni kwa sababu watoto walipata mafunzo mengi sana kutoka kwa wakuu wao kupitia utangamano huo.

Aidha, Momanyi (2009), katika *Mchezo wa Kobole,* (uk. 18), kuna wimbo ufuatao:

**32.** Hapa n'kate au n'sikate
Kuna mwiba wa mchongoma
Kwa upanga
Haukatiki
Kwa shoka
Hukatiki! (uk.18)

Katika utendaji wa wimbo huu, mwandishi anasema kuwa wanafunzi walikuwa katika vikundi na waliimba kwa kupokezana. Hapa maudhui ya ushirikiano na uelewano yanakuzwa ili kutekeleza jambo lolote, lazima kuwepo ushirikiano na uelewano miongoni mwa wahusika.

Wimbo huu ulihitaji umakinifu mkubwa hasa katika utendaji wake. Mchezo wa mchongoma huchezwa kwa kuhusisha vikundi viwili ambapo kikundi kimoja huvuta kingine kwa lengo la kutafuta ushindi. Pengine wavulana kuvutana na wasichana. Watoto katika jamii huenda hawaifahamu michezo na nyimbo zingine lakini wakiwa katika mazingira ya shuleni huenda wakajifunza mengi. Tazama kwenye picha



**Mchoro 4: Watoto wakicheza mchezo wa mchongoma.**
**Chanzo: Momanyi (2009) '*Mchezo wa Kobole'***

Picha hii imetuonyesha vikundi kadhaa vya watoto. Wanaocheza mchezo wa mchongoma ni wale ambao wamepanga foleni huku wakivutana. Msokole, (1981), akijadili kuhusu nafasi ya nyimbo katika jamii inayobadilika, anadai nyimbo za watoto ni rahisi na ni wazi. Tunaweza kuongezea kwamba, ingawa nyimbo ni rahisi na ni wazi, kuna zile ambazo ni ngumu hasa zile hazirudiwirudiwi. Nyimbo za watoto hutegemea viwango vya watoto. Wale wa madaraja ya chini wana nyimbo zao zinazoambatana na uchezaji. Wale wa madaraja ya juu wana zao jinsi tunavyoelezewa na Momanyi (keshatajwa) kwamba "Watoto wale wa madarasa ya chini waliimba na


kucheza katika vikundi walivyounda wenyewe. Wale wa madarasa ya juu walicheza mpira, kufagia madarasa au kunywesha maua maji.” (uk.17)

Pia katika *Mchezo wa Kobole*, mwandishi anasema “…nao watoto wale wadogo waliamua kuchezea mchanga ambao ulikuwa na unyevu baada ya mvua kunyesha. Waliunda vidatu vidogovidogo vya mchanga huo huku wakivipigapiga na kuimba.

**33.** Kipupuu
Punga moto
Kipupuu
Punga moto..” (uk 19)

Kando na wimbo huu kukuza maudhui ya umoja na ushirikiano, maudhui ya majukumu na nafasi za kijinsia katika jamii yanakuzwa. Hii ni kwa sababu katika jamii nyingi za Kiafrika watoto walijiweka kwa makundi katika uchezaji wao na michezo yao mara nyingi ilisawiri majukumu yanayotendwa na jamii husika.

Maudhui ya utangamano pia yamechimuzwa katika baadhi ya picha zilizotumika ndani ya bunilizi teule. Mfano, Syokau (keshatajwa) ameonyesha picha ya nyanya akiwa ameketi na wajukuu wake akiwasimulia hekaya katika uk. 6. Hali hii inaoyesha utangamano uliokuwepo katika jamii za Kiafrika. Vilevile, katika Matundura (2009) katika *Sitaki Iwe Siri*, amedhihirisha utangamano huu kwa kuonyesha picha ya Mwalongo akiwa ameketi na wajukuu wake akijaribu kujitetea kwa swali ambalo alikuwa ameulizwa na wajukuu wale kuhusu maradhi yaliyoua wazazi wao. “Wazazi wetu waliuawa na maradhi gani?” (uk. 11).




**Mchoro 5: Nyanya Mwalongo na wajukuu wake.**
**Chanzo: Matundura, 2008. 'Sitaki Iwe Siri' (uk. 11)**

Momanyi, katika *Mchezo wa Kobole* katika uk 18, watoto wanaonekana wakicheza pamoja. Hali kadhalika uimbaji katika Nandwa (2013) katika *Kito Apepeta uk.7* unadhihirisha utangamano na ushirikiano. Watoto wanacheza wao wenyewe kwa wenyewe bila kuwepo na mwalimu wao. Jambo hili la utangamano lilisisitizwa sana katika jamii za Kiafrika maana lilimfundisha mtoto ashirikiane na wanajamii katika majukumu mbalimbali.





**Mchoro 6: Mchoro unaoonyesha utangamano wa watoto wanapocheza na kuimba pamoja.**

**Chanzo: Matundura (2008). '*Sitaki Iwe Siri*' na Nandwa 2013. '*Kito Apepeta'***

### 5.1.6 Haki za Watoto

Mswada kuhusu Haki za Watoto ulipitishwa katika mkutano wa Umoja wa Mataifa uliofanyika Novemba, tarehe 20 mwaka wa 1989 na ukaanza kutekelezwa katika nchi mbalimbali ulimwenguni Kenya ikiwemo kuanzia miaka ya 1990 (Ehlers na Frank, 2008). Wanachama wa Umoja wa Mataifa wanahitaji kurejelea mswada huu kama sheria za kulinda maslahi ya watoto. Mswada huu umejengeka kwenye mihimili minne ambayo ni; Haki ya kuendelea kuishi. Mhimili huu unahusika na haki za watoto kuzaliwa na kutunzwa ili waishi maisha bora; Wana haki ya kupata huduma za afya kila inapohitajika. Mhimili wa pili unahusu Haki ya kukua, ambapo mtoto ana haki ya kupata elimu bora ili iweze kumjenga kimwili na kiakili; kumjenga mtoto kitabia, kiroho na kiumbo. Mhimili wa tatu unahusu Haki ya kumkinga mtoto kutokana na kufanya kazi za sulubu na zinazohatarisha maisha yake. Mhimili unalenga, kumkinga dhidi ya dhuluma zozote zile zinazotokana na shughuli mbalimbali za kijamii na kitamaduni zinazomwathiri mtoto. Mhimili wa mwisho unahusu Ushiriki wa Mtoto, ambapo mtoto anahitaji kupewa nafasi ya kushiriki katika maamuzi yanayotolewa kuhusu maisha yake; aidha, watoto wanafaa wapewe nafasi ya kutoa maoni yao kulingana na shughuli zinazowahusu (Taylor, 2009; Ngugi, 2015). Mihimili hii ndiyo imekuwa msingi wa kuibua maudhui mbalimbali kuhusiana na suala la haki.

Mtunzi yeyote anatarajiwa kuelezea matatizo na malalamiko ya jamii yake, kwa kuelezea matarajio yao (White na Couzens, 1984). Kwa hivyo, mtunzi ndiye jicho la jamii yake. Anatarajiwa aangazie masuala yatokeayo katika jamii anamoishi. Mojawapo ya masuala haya ni haki za watoto. Haki ni kile mtu anastahili kupata, kuwa nacho au kufanyiwa kwa mujibu wa sheria, kanuni, kaida, taratibu na mazoea (Longhorn, 2014). Kwa mujibu wa utafiti huu, neno haki linamaanisha kile mtoto anapaswa kufanyiwa na mzazi au mlezi kwa mujibu wa sheria. Chimbuko la haki ni

katiba ya sheria za nchi kama vile Katiba ya Kenya ambayo imeweka wazi haki za mtoto (Republic of Kenya, 2010a). Haki zenyewe zinafaa kufahamika kwa wote ili ziweze kuwafaidi. Kwa sababu hii, watunzi huziangazia haki hizi ili kuifikia hadhira ambayo huenda haiwezi kuielewa lugha ya kisheria inayotumika pamoja na kuonyesha jinsi haki zenyewe hukiukwa na wanajamii wake.

Watoto wana haki ya malezi, elimu na hata kuvishwa mavazi. Ingawa sheria ipo, wakati mwingine watoto hujipata wakikosa haki zao kutokana na visababishi kadhaa. Kwa sababu hii, Kenya imeunda sheria kwa mtoto tangu mwaka wa 2009 inayoshughulikia haki za mtoto ambazo zilitiwa mkazo na katiba ya mwaka 2010 (Republic of Kenya, 2010a). Sheria hii inawahusu wanajamii wote hivi kwamba kila mmoja amepewa jukumu maalumu la kutekeleza ili kuhakikisha upatikanaji wa haki hizi (Republic of Kenya, 2010b). Kutokana na umuhimu wa maslahi ya mtoto, suala la haki zake huwa muhimu sana hivi kwamba hata wasanii huliangazia katika tungo zao (Ngugi, 2011). Kwa mantiki hii, suala la haki za watoto limeshughulikiwa na waandishi katika bunilizi teule za watoto wakiwemo Matundura (2008) *Sitaki iwe siri*, Namlola, (2019) *Hidaya*, Nandwa (2013 *Kito Apepeta* na 2016 *Mchezo wa Mtelezo)*, (Syokau (2018) *Kade na Katana*. Kwenye bunilizi hizi, aina mbalimbali za haki ambazo mtoto anastahili kupewa zimejitokeza. Katika sehemu inayofuata, tunachunguza jinsi aina hizi tofauti za haki zimeangaziwa.

#### 5.1.6.1 Haki ya kukua

Mtoto ana haki ya kupata elimu ili iweze kumjenga kimwili na kiakili miongoni mwa masuala mengine. Elimu ni uti wa mgongo wa binadamu katika ulimwengu wa sasa na mtu huishi salama iwapo ameelimika. Kwa mujibu wa sheria za watoto, elimu ni shughuli ya kuwapa watoto mafundisho ya kiakili, kitabia, kiroho au ya aina yoyote ile (Republic of Kenya, 2010b). Elimu ndiyo humtenga na kumtofautisha binadamu

kutoka kwa wanyama wengine; ni nyenzo muhimu ya kumkomboa mtoto kutoka kwa matatizo mbalimbali.

Syokau (2018), katika *Kade na Katana* mwandishi ametuonyesha jinsi mhusika Katana aliweza kutatizika katika masomo yake. Ingawa kijana huyo alikuwa na uwezo wa kuelewa masomo yake, yeye alikuwa tegemeo kwa familia yake maana alitoka katika familia maskini hohehahe. Hii ilitokana na wazazi wake kuwa wakongwe na hakuweza kujikimu kwa lolote. Kijana huyo alinyimwa haki ya Kukua kwa sababu, badala ya kijana huyo kuwaza kuhusu masomo yake, yeye alifikiria kuhusu jinsi angeweza kunusuru familia yake kutokana na umaskini.

Namlola (2019) katika *Hidaya*, anatuonyesha Mzee Matata alivyomnyima Hidaya bintiye masomo na kutaka kumuoza kwa Bwana Mapesa katika ule umri wake mdogo. Katika shairi alilokumbuka mamake Hidaya ni dhihirisho kuwa hakuwa na uwezo wowote wa kumpinga mumewe kuhusu tendo hilo. Katika ubeti wa tatu, anasema;

**34.** “Sawa na mkwaju mui, ukaavyo msituni
Tumbili haushitui, na kamwe hawauoni
Siku kwisha uadui, wakautia thamani”. (uk. 21)

Maana hapa ni kwamba mtu asiyeelewa umuhimu wa masomo ni kama kushtua tumbili msituni, yaani, ni kazi bure kujaribu kumpa ukweli wa maisha mtu kama huyo.

Kutokana na manufaa ya elimu, basi ni vyema watoto wapelekwe shuleni ili kuwahakikishia ufanisi wao pamoja na kuwaondolea mateso wanayoweza kukumbana nayo. Ni muhimu wazazi watambue kwamba mtoto ana haki ya kupewa elimu kutokana na manufaa yake. Hidaya aliuliza babake, “Baba, umekuwa ukiniambia siku zote kwamba elimu ndio ufunguo wa maisha. Elimu tena ndio urithi pekee tulio nao

kutoka kwako. Eti elimu ndiyo hazina isiyoweza kuibwa. Vipi leo wataka niolewe baada ya kukamilisha darasa la nane?" (uk 15).

Elimu ndiyo humtenga na kumtofautisha binadamu kutoka kwa wanyama wengine. Ni nyenzo muhimu ya kumkomboa mtoto kutoka kwa matatizo mbalimbali pamoja na kumwezesha kupata ajira mbalimbali kama vile rubani, uuguzi, ualimu, ukulima, miongoni mwa ajira nyingine (Ngugi, 2014). Namlola (keshatajwa) anasema kwamba elimu ndiyo msingi mkubwa wa kumwezesha mtu kufanya kazi mbalimbali ikiwemo udaktari aliousomea Hidaya baada ya kupitia machungu katika maisha yake.

Watoto wanahimizwa waende shuleni wanapofikisha umri wa kusoma kwa kuwa wana haki ya kupata elimu ambayo pia hujumuisha; elimu ya maisha na elimu ya kidini (Republic of Kenya, 2010b). Hii ndiyo sababu Namlola (2019) ametuonyesha kupitia kwa shairi kwamba, Hidaya pamoja na mamake walikuwa na imani na kumwomba Mola aweze kutimiza mapenzi yake kwa shida ambayo mwanawe alikuwa anapitia. Hii ni elimu ya dini tunayozungumzia. Kwa hivyo, Serikali na wazazi wana jukumu la kuhakikisha kwamba watoto wanapata haki hii muhimu.

Kupitia kwa elimu, madhila wanayoyapata watoto kama vile ajira, pamoja na ndoa za mapema ambazo zimeenea sana na kuwaathiri watoto huweza kuepukwa. Elimu huwa muhimu kwa watoto wote katika jamii. Kwa sababu hii, yeyote ambaye humnyima mtoto nafasi ya kuelimishwa huweza kupelekwa mahakamani na kufunguliwa mashtaka. Mfano Bwana Mapesa na Bwana Matata na wote waliomteka nyara mtoto huyo (Hidaya) walitiwa nguvuni (Namlola, 2019).

Katika shairi la *Malenga wa Mndani* alilokumbuka mama Pembe, mamake Hidaya, ni wazi kwamba wazazi ndio wanalaumiwa kuwa kikwazo kikubwa katika kufikiwa kwa haki hii. Watoto wanalalamika kukosa imani ya kusoma kutokana na wazazi wao

kutochangamkia elimu. Badala ya kuwatia watoto wao moyo, wazazi huwatamausha watoto wao kwa kupuuzilia mbali ndoto za watoto wao jinsi bwana Matata anamfanyia mwanawe.

Wazazi na walezi wa watoto hawaithamini elimu kama anavyodai msimulizi (Namlola, 2019), kuwa wakati mwingine watoto wanatolewa shuleni kwa sababu ya kuwaoza ndoa za mapema. Kwa hivyo, kumnyima mtoto elimu kwa msingi wa uchochole ni kisingizio tu. Ndoa yafaa ije baada ya mtoto kuelimishwa na kupata ajira yake. Tatizo ni kwamba, elimu kwa mtoto wa kike haijapewa nafasi ya mwanzo katika baadhi ya jamii na huwa tatizo kubwa linaloathiri kupatikana kwa haki ya elimu.

**5.1.6.2 Haki ya ushiriki wa mtoto**

Tulivyosema hapo awali ni kwamba mtoto anahitaji kupewa nafasi ya kushiriki katika maamuzi yanayotolewa kuhusu maisha yake. Aidha, wapewe nafasi ya kutoa maoni yao kulingana na shughuli zinazotolewa.

Mtoto ana haki ya kusikizwa na wazazi. Kuna mambo ambayo watoto wanakumbana nayo na wasipopata mtu wa kuwasikiza na kupata jawabu za maswali wanayotaka kujibiwa wanakufa moyo na kukosa kujiamini. Hii ndio sababu Namlola, (2019) anatuonyesha jinsi Hidaya alisononeka baada ya kutishwa na babake kuhusu ndoa yake na Bwana Mapesa. Yeye hakupewa nafasi hata kidogo kujieleza kuhusu haki yake ya masomo akilinganishwa na kakake Pembe. Mwandishi anatuambia kwamba, baada ya kukaririwa shairi na mamake, yeye alipata ari mpya ambayo hakuwa nayo hapo awali.


Kwa upande mwingine, kuna wale ambao wanapata haki hii ya ushiriki. Hao ni watoto ambao wamekuwa katika mazingira mwafaka yenye malezi ya kupewa nafasi

ya kujieleza na kusikizwa kwa masuala nyeti. Wao wanapata matumaini na ufanisi katika masomo na ukuaji wa talanta. Mfano mzuri ametueleza Matundura, (2008) katika *Sitaki Iwe* Siri, kwamba Musa alipewa nafasi hiyo ya ushiriki kwanza kabisa na nyanyake Mwalongo awe mfano mwema kwa dadaze. Pili, ni mwalimu wake mkuu Bw. Said Selemani ambaye alimtia shime ili ahusike kwa ushiriki wa uandishi uliomletea ushindi mwishoni. Hatua hiyo ilimpa matumaini na msukumo mkubwa Musa na akaweza kufanya kazi yake kwa ujasiri mkubwa.

#### 5.1.6.3 Haki ya Kutofanya kazi za Sulubu

Kazi za sulubu kwa watoto ni kazi ambazo ni ngumu kulingana na uwezo wao. Ni kazi ambazo watu wakubwa wanapaswa kufanya lakini watoto hujipata wamefanya kwa sababu ambazo hazieleweki. Kazi hizi za sulubu mara nyingi ni kazi ambazo zinahatarisha maisha na mara nyingi humzuia mtoto kwenda shuleni au hata kukwamiza ukuaji wake na hata shughuli mbalimbali za kijamii na kitamaduni. Syokau, (2018), kupitia utanzu wa hekaya ametuonyesha jinsi Katana alijihusisha na kazi ngumu ili aweze kuokoa familia yake kutokana na umaskini ambao ulikuwa umekithiri.

Matumizi ya picha ndani ya bunilizi pia yamesisitiza maudhui ya haki za watoto. Momanyi, (2009), katika *Mchezo wa Kobole* ameonyesha katika picha ndani ya bunilizi hiyo jinsi mwalimu Kabau aliwapata watoto wakifanyizwa kazi ya sulubu katika kasri la Bw. Manoti. Suala hili ni ukiukaji wa haki za watoto maana watoto katika umri huo wanapaswa kuwa wanasoma na hali kadhalika kuna sheria inayowatunza watoto dhidi ya unyanyasaji huo.



**Mchoro 7: Mchoro unoonyesha watoto wakifanyizwa kazi za sulubu.**
**Chanzo: Momanyi (2009) *Mchezo wa Kobole* (uk.33)**

### 5.1.7 Ushujaa

Katika taaluma ya fasihi, shujaa ni mhusika ambaye kwenye simulizi hukabiliana na masaibu ya hapa na pale lakini hupambana nayo na hatimaye kuibuka mshindi (Bakize na Senkoro, 2019). TUKI (2013) inaeleza kwamba mashujaa ni watu wenye moyo thabiti ambao wanaweza kukabili mambo, hata kama ni ya hatari. Mara nyingi, kutokana na mfumodume katika jamii nyingi za Kiafrika, mashujaa wengi hutarajiwa kuwa wanaume. Hivyo, watoto wa kiume hujengwa na kukuzwa katika mazingira ya kuamini kwamba wao ni mashujaa (Bakize, 2015). Ilivyo ni kwamba, shujaa ni yeyote yule ama mtoto wa kiume ama wa kike ambaye ameweza kukumbana na changamoto za maisha na kuebuka mshindi. Waandishi wa bunilizi za watoto wametumia mbinu ya kimwingilianotanzu katika kuchimuza suala la ushujaa katika kazi zao. Hata hivyo, tunaweza kugawa ushujaa huu kwa namna mbili: ushujaa utokanao na ujasiri na ushujaa unaotokana na ulimwengu wa kifantasia.

Ushujaa utokanao na ujasiri ni ule uwezo wa kukabiliana na changamoto za maisha zinazomzunguka mtoto. Mdee na wenzake (2011), wanasema ushujaa ni hali ya kuwa na moyo wa ujasiri. Kulingana na maelezo yao, tunakubali kwamba ushujaa ni hali ya kutenda mambo au jambo bila woga; yaani, kuwa na uhodari na ukakamavu katika utendaji wa mambo.

Ushujaa ni hali ya kuwa na ujasiri wa kufanya jambo bila woga. Kwa hivyo shujaa ni mtu mwenye moyo thabiti anayeweza kukabili mambo hata kama ni hatari yaani ni mtu jasiri (Kiptum, 2017). Ushujaa katika fasihi ya watoto ni ile hali ya kuwa na moyo jasiri na pia ni ile hali ya kufanya mambo bila woga.

Maudhui ya ushujaa yamechimuzwa na vipengele kadhaa vya kimwingilianotanzu kupitia kazi mbalimbali. Matundura (2008), katika *Sitaki Iwe Siri* ameonyesha ushujaa huu kupitia utanzu wa insha uliyoandikwa na Musa. Mwandishi anatueleza kwamba, tangazo la uandishi wa insha kuhusu ***Ukimwi* duniani** lililokuwa kwenye gazeti la *Taifa leo* ulipotolewa, Musa ndiye alionyesha ujasiri huo wa ushiriki. Mwandishi anatueleza kuwa, “Mwalimu mkuu alipendezwa sana na ujasiri wa Musa….” (uk 20). Mwandishi anasema, “Ni Musa pekee aliyekuwa jasiri kushiriki kwenye shindano hilo. Wanafunzi wengine hata kutoka madarasa ya juu waliogopa.” (uk. 20). Kutokana na ujasiri wake, Musa aliibuka mshindi kwenye shindano hilo na akaweza kutunukiwa zawadi kemkem na kutoka siku hiyo, akaweza kung’amua siri kuhusu chanzo cha kifo cha wazazi wake kupitia kwa hotuba iliyotolewa na nyanyake. (uk .64)

Hali kadhalika, Matundura, (2008), katika bunilizi yake *Sitaki Iwe Siri* ametumia utanzu wa barua katika uandishi wake. Kuna barua ya Musa Matano iliyotoka kwa Wizara ya Afya ikimtangazia Musa ushindi wake baada ya kushiriki katika uandishi

wa insha. Hapa, mwandishi alitaka kudokeza maudhui ya ushindi utokanao na bidii ya mtu.

**35.** Kwa Bw. Musa Matano,

> REJ: USHINDI WA INSHA YAKO' SITAKI IWE SIRI'
>
> Wizara ya Afya …….nina furaha kukufahamisha kwamba mtungo wako, 'Sitaki Iwe Siri' ndio uliokuwa utungo bora zaidi kwenye shindano letu.
>
> Mbali na kukutuza zawadi kemkem,….zitagharamia masomo yako na ya ndugu zako katika viwango vyote vikiwemo vyuo vikuu. Pia shule yako itanufaika…
>
> Asante,
>
> Wako Mwaminifu,
>
> Lilian Mokeira (Katibu Mkuu)

Ushujaa wa Musa katika ubunifu wake ulidhihirika katika barua hii. Katibu mkuu Bi. Mokeira alikuwa na furaha kumfahamisha Musa Matano kwamba, mtungo wake "Sitaki Iwe Siri" ndio uliokuwa utungo bora zaidi kwenye shindano lao. Barua hiyo ilimjuza Musa kwamba, kando na kutuzwa zawadi kemkem, Wizara ya afya ingegharamia masomo yake na ya nduguze katika viwango vyote vikiwemo vyuo vikuu. Aidha kutokana na ushindi wake, shule yake ingenufaika.

Nandwa, 2013 katika hadithi yake *Kito Apepeta*, ametumia mbinu ya nyimbo kwa lengo la kuchimuza maudhui ya ushujaa. Kati ya nyimbo hizo ni wimbo wa *Apepetanga* ulioimbwa na Kito. Ushujaa wa Kito unaonekana pale ambapo aliitikia bila wasiwasi kufundisha wanafunzi wenzake wimbo huo kwa minajili ya kuburudisha mgeni aliyekuwa akipaswa kuwatembelea shuleni mwao. Wimbo huo aliuimba kwa ujasiri mwingi. Baadaye, mwandishi anatuambia kwamba, wimbo wenyewe ulishinda katika mashindano ya muziki katika eneo lao.

Baada ya wanafunzi hawa wa Khwisero kupewa tuzo la ushindi, mkaguzi mkuu alitambua ujasiri wa Kito. Alisema "Mwanafunzi Kito alionyesha ujasiri pamoja na

mbwembwe za hali ya juu. Alijiamini na kuvutia hisia za kila mmoja…" (uk 35). Huu ni ushujaa tunaozungumzia maana kupitia ushindi huu wa wimbo wa Kito, shule yao iliweza kupata sifa nyingi.

Utanzu wa ushairi uliotumika katika bunilizi ya Namlola, (2019), *Hidaya* unadokeza maudhui ya ushujaa. Mama Pembe alimsihi mwanawe asikate tamaa kwa yale ambayo alikuwa anayapitia " kwani haya ni mawingu, yatapita" (uk 21).

**36.** Nawe punguza mtima, ingawa hujulikani,
Muhimu simama wima, itapita mitihani,
Watakuja hima hima, wakuombe samahani….ubeti wa 4

Shairi hilo lilimpa ari mpya Hidaya aliyefuta machozi na kuchukua ujasiri mpya ambao hakuwa nao hapo awali. Ushujaa wake unaonekana pale ambapo aliweza kupigania haki yake mpaka mahasidi wake wakatiwa mbaroni. Hapo akaweza kuendeleza elimu yake hadi akawa daktari, kinyume na alivyosema babake kuhusu mtoto msichana kwamba "Sitaki maneno ya kitoto. Eti elimu... elimu.,. elimu ukwaju. Wangapi wamesoma hadi vyuo vikuu na twawaona humu mabarazani wakitafuta kazi za jua kali?" (uk. 16). Ugomvi huu ulitokana na suala la ndoa ya mapema kwa Bwana Mapesa ambaye babake Hidaya alikuwa anataka amwoze bintiye kinyume na sheria inayolinda watoto.

Hali kadhalika, kuna ule ushujaa utokanao na ulimwengu wa kifantasia. Fantasia ni hali ya uajabuajabu au undotondoto unaojitokeza katika kazi za fasihi, (Bakize, 2014). Bakize anasema, fasihi ya Kiswahili yenye fantasia ni ile ambayo imesheheni mambo ya ajabuajabu, ya kinjozi, majitu ya kutisha, nguvu zisizo za kawaida na kadhalika. Ikumbukwe kwamba fasihi ya watoto yenye fantasia ni ile ambayo imesheheni mambo yasiyo ya kawaida. Hii ni kwa sababu ingawa fasihi inapaswa kutoa mtoto katika ulimwengu wake watoto hadi ulimwengu asioufahamu au halisia, mtoto huyo

hapaswi kutishwa kwa mfano kuhusiana na majitu. Hata hivyo, katika jamii za Kiafrika, watoto walikuwa wanapewa masimulizi kuhusu majitu kwa lengo la kuwaonya kuhusu mambo fulani. Mathalan, kwenda mahali hatari, mwandishi anapaswa kuujenga hali hiyo kwa njia isiyoogovya.

Mambo hayo yasiyo ya kawaida hutumika pamoja na uhalisia wa maisha. Fantasia nyingi huwa na motifu ya safari, au msako wa utafutaji au ufumbuzi wa kitu fulani. Anavyosema Bakize (keshatajwa) ni kwamba, mambo ya kifantasia sio ya kweli yaani hayawezi kutokea na hayatarajiwi kutokea isipokuwa hutumiwa kwa makusudi ili kukidhi haja fulani za kifasihi.

Fantasia hutumika zaidi katika maandishi yanayolenga hadhira ya watoto. Hutumiwa katika kazi za kinathari ambazo huwa na mandhari ya ajabu, matukio magumu kukubalika katika hali ya kawaida na hata wahusika wasioweza kupatikana katika uhalisia. Mtoto huamini kuwa kila kitu kinawezekana. Kwamba wanyama wote wana uwezo wa kuongea; hasa watoto wale wadogo wanaoanza masomo yao. Ingawa utafiti huu unarejelea kazi za watoto wa daraja la tatu, watoto wawa hawa bado wana imani waliyokuwa nayo tangu utotoni kwamba, kila kitu kina uwezo wa kibinadamu. Hali hii ni muhimu sana katika bunilizi za watoto kwa vile huwawezesha kupata mafunzo yanayowasilishwa.

Ujio wa teknolojia mpya ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA) umeendeleza fasihi hii ya kifantasia. Ibala (2018) anadai kuwa, katika runinga, vipindi vya watoto ni anuai, mojawapo kikiwa sinema za vibonzo. Vibonzo hivi huwa na wanyama ambao wanachukua sifa za kibinadamu kama vile kuongea. Fasihi hii husaidia kuhifadhi na kuendeleza utamaduni, mienendo ya watu, mavazi na kadhalika

(Mohochi, 2000). Katika hali hii, watoto huelimishwa na wakati uo huo kupata burudani.

Syokau, (2018) katika hadithi yake *Kade na Katana* kupitia utanzu wa hekaya ndani ya bunilizi ameweza kutuonyesha ushujaa wa Katana, kijana shupavu na mwenye akili nyingi aliyeweza kuokoa familia yake kutokana na umaskini. Pia ujasiri mwingi inaonekana pale anapofanya vibarua na kazi nzito hasa ya kuvua samaki usiku kwa minajili ya kutafutia mlo familia yake. Huu ni ujasiri mwingi. Hali kadhalika, kukubali kumsaidia yule nyanya ajuza baada ya wao kuamkuana kupitia dayalojia/ mazungumzo (uk 13 hadi 14) ni ujasiri mkubwa; uhusiano huu kulingana na hekaya hiyo ulimletea ushindi mkubwa na mwishoni akawa shujaa wa kijiji chao.

Ushujaa wa aina hii ndio tunaouita ushujaa wa kifantasia. Suala la kufanya uvuvi wakati wa usiku ukilinganishwa na umri wake Katana jinsi alivyoeleza Syokau, (2018) ni fantasia maana mtoto kama huyo kwa kawaida, hana uwezo wa kustahimili changamoto zinazohusiana na uvuvi. Mwandishi pia ametuonyesha kuhusu uhusiano ule wa Katana na ajuza ambaye alimpa mkufu uliokuwa jaha ya maisha yake. Usimulizi kuhusu mkufu huo ni kitu ambacho hakieleweki kwa namna ambayo uliweza kutenda mambo ya kiajabuajabu yasiyoeleweka. Ili kushika makini ya mtoto, lazima mwana fasihi akiuke uhalisia na kumfanya mtoto aende mbali kifikra.

### 5.1.8 Malezi

Neno malezi lina maana ya kipekee katika jamii nyingi duniani. Maana hii pia imeweza kufafanuliwa na baadhi ya wataalam na hivyo kuchukua maana kadhaa. Jamal, (1980) anasema kuwa malezi ni amali aifanyayo mzazi kumlinda na kumhifadhi mtoto kimaumbile kutokana na mazingira yaliyomzunguka. Pia, anaendelea kusema kwamba, ni budi mzazi na jamii kuwa ni kigezo chema kwa

watoto, wapate kuiga mema kutoka kwao" (Tafsiri yetu). Malezi ni taratibu zinazotumiwa na wazazi au walezi katika kusimamia misingi sahihi ya ukuaji wa mtoto (Othman, 2018). Kwa ujumla, malezi ni ile hali ya kudhibiti mtoto katika hali ya ukuaji ili awe na tabia inayokubalika katika jamii. Lengo la malezi ni kumjenga mtoto katika tabia njema zenye kukubalika na jamii husika zikiwa ni pamoja na elimu, maadili mema, mavazi, lishe na malazi bora. Katika kuzungumzia malezi, inabidi tuangalie mazingira inayomzunguka mtoto; yaani malezi nyumbani na shuleni.

### 5.1.8.1 Malezi ya mtoto nyumbani

Malezi ya watoto nyumbani ni malezi anayopewa mtoto akiwa katika mazingira yanayomzingira, yaani akiwa na wazazi wake au walezi. Maadili mema kwa mtoto hutegemea sana wale ambao wanamlea mtoto huyo akiwa nyumbani. Sanders (1967) anadai kuwa, jinsi tunawachukulia watoto, ndivyo watoto hawa wanavyojichukulia. Anasisitiza kuwa iwapo watoto wanapewa heshima, basi hata wao watajiheshimu katika matendo yao. Lakini iwapo tutawapa mkebe kutumia kama kikombe kwa sababu tunafikiria kuwa hawajali au watavunja kikombe cha kauri, basi hata wao hawatajali lakini iwapo watapewa kikombe cha kauri ili waone umaridadi uliomo katika kikombe hicho, basi wataweza kukithamini kikombe hicho. Hii ina maana kuwa watoto wanapaswa kupewa mafundisho ambayo yanawawezesha kujitathmini ndipo waweze kudhihirisha tabia zinazokubalika.

Malezi ya mtoto ni mchakato wa maandalizi ya mtoto utakaomwezesha kupata maslahi bora. Malezi hayo humjenga mtoto kukua, kukubalika na kushiriki katika shughuli za kijamii na kiutamaduni kwa kumlinda na kumpatia huduma za kimsingi. Watoto wanatakiwa waonyeshwe malezi kwa njia nzuri wakiwa bado wachanga, kwa kuanzia kwa upendo na kuthaminiwa kikamilifu kutoka kwa wazazi au walezi wao na jamii kwa ujumla (Othman, 2018).

Suala la usasa, sayansi na teknolojia katika jamii limesababisha kuwepo kwa changamoto katika malezi ya watoto hasa, kwa wazazi au walezi. Hii huathiri sana malezi kwa kuwa, wazazi/walezi, hawana nafasi kuishi na wanawe kutokana na ajira na majukumu ya kikazi. Waandishi wa bunilizi za watoto wana nafasi kubwa ya kuiongoza jamii wakiwemo watoto kuwa na maadili mema kupitia uandishi wao. Teknolojia hufanya watoto kuelewa mambo mengi wakiwa wachanga na wasipoongozwa kujua jinsi ya kukabiliana na mambo haya, matokeo yake huwa si ya kufurahisha. Teknolojia ni nzuri ikitumika vyema kuendeleza ukuaji wa tabia ya watoto lakini majukumu ya wazazi katika karne ya ishirini na moja yanaelekea kuwafanya wawatelekeze watoto kimalezi.

#### 5.1.8.2 Malezi ya mtoto shuleni

Shule ni miongoni mwa taasisi zinazojikita katika kutoa malezi na maadili mema kwa mtoto, ambapo wazazi huwapeleka watoto wao ili wapate elimu, malezi na maadili mema kwa ujumla. Hata hivyo, malezi ya kwanza huanza nyumbani pale wazazi wanapopanda mbegu za uadilifu na tabia njema. Malezi shuleni huendeleza yale yaliyoanzishwa nyumbani. Utanzu wa Hadithi ndani ya Hekaya katika *Kade na Katana* (Syokau, 2013), una hadithi inayosimuliwa na Zambarau Kajaza kwa wanawe. Lengo la hadithi hiyo ni kuadilisha, kwamba hakuna haja ya kuwepo na chuki baina ya ndugu mmoja. Hadithi hiyo ilihusu vijana wawili; Kade na Katana. Ndugu hawa wawili walitofautiana kitabia. Ktana alikuwa na wema na nduguye alikuwa na wivu chungu nzima. Matendo ya wawili hawa ilikuwa funzo kwa wajukuu wake Kibibi na wasomaji kwa ujumla. Walipaswa kufuata mienendo ya Katana wala sio Kade.

### 5.1.9 Utamaduni

Dhana ya utamaduni ni pana sana. Hii ni kwa sababu inajumuisha njia zote za maisha za watu wa jamii fulani. Utamaduni hujumuisha shughuli za kiuchumi, mfumo wa kisiasa, vyakula, mavazi, imani, mila na desturi na mambo mengine ya maisha ya watu (Omar, 1981). Ifahamike kwamba, jamii hutambulika kwa utamaduni wao: vyakula vyao, mavazi, imani, mila na desturi ambazo huwa tofauti sana na jamii nyingine. Hata hivyo, kuna uwezekano wa utamaduni wa watu kufifia na kubadilika. Omari, (k.h.j) anasisitiza kuwa, utamaduni unaweza kubadilika kwa kufuata mahali na mazingira yaliyopo. Hii haimaanishi kuwa mazingira ya mahali yanazaa utamaduni wa aina fulani. Bali utamaduni unaweza kuishi na kuhifadhi kizazi hata kizazi, mwanadamu katika uhusiano wake na mwenzake, maumbile na mazingira, hana budi kuurekebisha utamaduni wake katika kila hatua ya maendeleo yake (Method, 2015). Kufifia kwa tamaduni za watu hutokana na mazingira mapya katika jamii yenye teknolojia na utandawazi ambao watu wanaukumbatia na kukubali mabadiliko. Hivyo basi, waandishi wa fasihi, hususan fasihi ya watoto hawana budi kuwakumbusha watoto kuhusu tamaduni zao katika bunilizi zao. Matumizi ya mwingilianotanzu katika uandishi wa bunilizi za watoto kwa kiwango kikubwa yamesaidia kuchimuza maudhui ya utamaduni.

Momanyi, (2009) katika *Mchezo wa Kobole*, kuna wimbo unaimbwa na watoto wanapocheza uwanjani. Msimulizi anasema; "..wengine waliimba nyimbo mbalimbali huku wakicheza kwa furaha. Nyimbo hizo zilimkumbusha mwalimu siku za utoto wake. Akasimama na kusikiliza." (uk.17)

**37.** Salaale hiyo!
Meli imekuja
Imekuja na tanga za manjano
Bei yake ni shilingi tano
Mwaiona Haaa lele
Mwaiona ina madirisha hiyo! (uk 17)


Wimbo huu unakuza maudhui ya utamaduni wa pwani ambako usafiri wa bahari unadokezwa kwa kutajwa kwa meli. Watu waliolelewa kwa utamaduni wa pwani wanafahamu vizuri kuhusu usafiri wa bahari. Vyombo vya usafiri ni kama vile, meli, jahazi, motaboti na kadhalika. Hivyo basi, watoto walio na utamaduni wa pwani wanapoimba wimbo huo, hukumbushwa kuhusu mazingira yao. Hata hivyo, watoto wanaoishi kwenye maeneo ya bara huenda wasielewe kwa sababu usafiri wa bara huhusisha magari, pikipiki na hata baiskeli. Kilicho muhimu ni kwamba, watoto hawa wanaposoma bunilizi hizi, wanapata kufahamu tamaduni za sehemu mbalimbali za nchi yao. Hali hii inawasaidia wanafunzi kuelewa mazingira wanamoishi vizuri kwa upana zaidi.

Katika hadithi yake *Kade na Katana* ( Syokau, 2018), msimulizi ametuonyesha kupitia utanzu wa barua kwamba msimulizi alialikwa na bibi yake. Alipofika kwa bibi huyo, alikuta bibi yake pamoja na dada zake pale jikoni wakipika chakula. Mara, nyanya aliuliza Mueni “umeosha mchele? (uk. 4). Pia mwandishi kupitia kwa picha katika (uk. 4), ameonyesha nyumba ya kiasili. Uasili wa nyumba hii huonekana kwa muundo wake. Paa limeezekwa kwa nyasi na ukuta kubomwa kwa matope.Nyumba hii ni ya kiasilia na unadhihirisha utamaduni husika. Hali hii ni tofauti na majengo ya kisasa ambayo paa huweza kuwa la mabati au vigae na ukuta kujengwa kwa matofali au mawe.



**Mchoro 8: Nyumba ya kiasili**
**Chanzo: Syokau, (2018), *Kade na Katana (uk. 4)***

Katika uk 5, mwandishi ametuonyesha utamaduni wa Kiafrika kupitia utanzu wa hekaya ndani ya bunilizi. Suala la utambaji wa hadithi kwa watoto au wajukuu ni suala lililojulikana katika tamaduni za kiafrika. Utambaji huo wa hadithi ulifanyika wakati wa mapumziko. Aidha, maandalizi ya uwasilishaji huo ulibainisha utamaduni husika. Tazama picha hii katika Syokau, (2018), *Kade na Katana* (uk. 6)



**Mchoro 9: Taswira ya maandalizi ya uwasilishwaji wa hadithi katika baadhi ya jamii za Kiafrika.**
**Chanzo: Syokau (2018), *Kade na Katana***

Nandwa, (2013), katika '*Apepetanga'* amechimuza maudhui ya utamaduni kupitia kwa utanzu wa wimbo wa watoto uliotumiwa kuwa urithi muhimu wa utamaduni, lugha, mila na thamani za kijamii. Katika wimbo *Apepetanga,* Kito aliongoza uimbaji wa wimbo huo kwa lugha ya kiasili.

**38.** *Mwana wa mama apepetanga*
*Mwana wa mama apepetanga*
*Yatsiayo, yarulayo*
*Yaboola mama njonyi bilenje..(uk 12)*

*( Tafsiri)*
Mwana wa mama anazunguka

> Mwana wa mama anazunguka
> Alienda huku, huko na kule
> Alirudi nyumbani na kumwambia mama yake
> Kwamba alikuwa amechoka miguu (uk. 12)

Kupitia kwa matumizi ya wimbo ndani ya bunilizi, waimbaji hawa wameweza kuhifadhi historia na utamaduni wa jamii zao. Ingawaje, maendeleo ya kisayansi na teknolojia yameanza kuingiza jamii nyingi katika fasihi ya televisheni na video na hivyo kuonekana kwamba jambo hili linafifisha starehe inayopatikana katika nyimbo. (Mlacha, 1998).

Mabadiliko katika jamii yamesababisha mabadiliko katika nyimbo na hivyo basi nyimbo zimekuwa na maudhui na fani tofauti kutegemea namna jamii ilivyobadilika (Ngugi, 2000). Hii ndio maana tamaduni za kiafrika huhimizwa sana katika tamasha za muziki katika nchi nyingi za Kiafrika.

Tunavyofahamu ni kwamba katika mazingira ya shuleni, watoto hutoka kwa jamii tofauti tofauti zenye tamaduni tofauti tofauti. Bila hata kufahamu maana yake, watoto hupenda nyimbo na wana wepesi wa kujifunza kwa njia ya urudiaji. Huenda watoto hawa wanaufahamu utamaduni huo au la (muhimu ni utendaji wa wimbo huo.)

Hali kadhalika, wimbo huo wa *Apepetanga* uliambatana na ala za muziki kama vile *isukuti* na '*olwika*'. Mwandishi anasema, "Toni na Baraka walijipanga na ala za '*isukuti* na '*Olwika*' (uk 27). Pia katika picha iliyochorwa katika (uk. 28), tunaonyeshwa mavazi waliyovaa waimbaji hawa kuwa dhihirisho la utamaduni wa jamii husika.



**Mchoro 10: Mavazi zenye dhihirisho la utamaduni wa jamii**
**Chanzo: Nandwa (2013)** ***Kito Apepeta***

Mavazi haya ni dhihirisho la utamaduni wa jamii husika kwa sababu watoto huiga kile kinachotendeka katika jamii yao ukilinganishwa na nyimbo za kisasa. Wimbo huu uliimbwa kwa Kiluhya, mojawapo ya lugha ya jamii ya Kiafrika nchini Kenya. Kwenye picha, kuna wavulana wawili katika upande wa kushoto wanaoonekana wakitumia ala hizo za kitamaduni za jamii hiyo.

Maamkizi katika utanzu wa mazungumzo katika kazi ya Syokau (2018:13) hudokeza maudhui ya utamaduni wa kiafrika. Hili ni suala ambalo watoto hufunzwa tangu wakiwa wadogo jinsi ya kuamkua watu wazima kutegemea jamii husika. Maamkizi haya huendelezwa hadi watoto wanapoanza masomo yao wakiwa katika madarasa ya chini maana katika viwango hivyo, watoto hufundishwa kwa lugha asilia. Hapo watoto bado wanakumbushwa kuhusu tamaduni zao. Hata hivyo, maamkizi katika lugha ya Kiswahili hufunzwa katika somo la Kiswahili kwa lengo la kuimarisha umilisi wa mawasiliano. Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Nchini Kenya (K. I. C. D) katika

silabasi imesisitiza kuwa somo la maamkizi lifunzwe kuanzia shule za msingi hadi za upili. Suala hili ni muhimu katika ule mchakato wa kuhusiana, kuwasiliana na hali kadhalika katika utangamano wa watoto na watu wazima.

### 5.1.10 Uzalendo

Osore, (2020) anachukulia uzalendo kuwa ni upendo wa nchi yako na watu wake. Waandishi wa bunilizi za watoto hawana budi kuwajuza watoto wapende nchi yao pamoja na jamii zao kupitia kwa bunilizi zao.

Katika *Sitaki Iwe Siri*, (Matundura, 2009), kuna wimbo wa Taifa la Kenya ndani ya bunilizi. Mwandishi anasema 'Musa aliwaongoza maskauti wenzake katika kupandisha bendera kwenye mlingoti. Huku shughuli hiyo ikiendelea, Musa aliwaambia wanafunzi wote wa shule, "Tuimbeni wimbo wa taifa" (uk 17). Nao wanafunzi wakauimba kwa ufasaha:

**39.** Eeh Mungu nguvu yetu
Ilete Baraka kwetu
Haki iwe ngao na mlinzi
Na tukae na undugu
Amani na undugu
Raha tupate na ustawi… (uk 17)

Kupitia kwa wimbo huu, maudhui ya uzalendo yanakuzwa. Ni wimbo unaowahimiza wanafunzi kuwa raia wema ambao wanaipenda nchi yao.

Uzalendo ni ule upendo wa mtu kwa nchi yake. Upendo huu huonekana pale ambapo watu hufanya kazi kwa pamoja na kuthamini mambo ambayo wanahitajika kufanya kama jamii moja. Aidha, Nandwa, (2013) katika *Kito Apepeta* tunaelezwa kwamba 'Susana, kiranja mkuu wa shule, ndiye aliongoza kipindi cha kukaribisha mgeni kwa shuleni. Alianzisha wimbo wa taifa kisha wote wakaimba kwa pamoja: *Ee Mungu nguvu yetu*…' (uk.10). Wimbo huu unasisitiza mambo matatu makuu ambayo mwanajamii anapaswa kuzingatia kama mzalendo.

#### 5.1.9.1 Uraia na Amani

Tunapozungumzia uraia hapa, tunachukulia maana ya kujivunia kuwa Mkenya au kuwa raia wa nchi fulani. Akiwa raia wa nchi, mtoto anapaswa kuomba baraka zake Mwenyezi Mungu, aliye na nguvu ili watu wakae kwa amani na uhuru. Kando na kujivunia nchi yao, mtoto anapaswa kujivunia mahali anaishi; nyumbani kwao katika mazingira asilia. Hali kadhalika, anapaswa kutafuta amani kwa wote wanaomzingira, shuleni na hasa katika ulimwengu wao wa michezo na katika mahusiano yao nyumbani.

#### 5.1.9.2 Umoja na Bidii

Wimbo wenyewe vilevile unahimiza suala la umoja na bidii.

**40.** Amkeni ndugu zetu
Tufanye zote bidii
Nasi tujitoe kwa nguvu…(uk. 10)

Wimbo huu unawahimiza wazalendo waamke na kufanya bidii. Kwamba wajitolee kwa nguvu kwa sababu wanaipenda nchi yao. Watu walipaswa kuungana pamoja na kufanya bidii ili wajenge nchi yao. Waandishi wa bunilizi hizi za watoto wamejaribu kuhimiza umoja na bidii kupitia bunilizi zao. Umoja unadhihirika pale wanaposhirikiana pamoja wanapoimba nyimbo mbalimbali wakiwa michezoni.

#### 5.1.9.3 Upendo

Maudhui ya upendo pia yanasisitizwa katika wimbo huu wa taifa. Watu wanahimizwa wapendane hata wakiwa kazini wakionyeshana shukurani.

**41.** Na tukae na undugu
Amani na uhuru
……………… (ubeti wa kwanza)
Tuungane mikono
Pamoja kazini….. (ubeti wa mwisho) (uk. 10)

Wimbo huu wa taifa unawahimiza watu wakae kwa undugu, kwa amani na uhuru. Hali kadhalika, waungane mikono wakiwa kazini na kila siku wawe na shukurani.

Watoto wanapoimba wimbo huu, wanajifunza kuwa, wao lazima wadumishe upendo kwa nchi yao na kwa wote wanaowazingira. Wimbo huu wa taifa unapaswa kufundishwa watoto wakiwa katika madarasa ya chini ili waweze kutambua uzito wa maneno kwenye wimbo huo na hasa kuhusiana na nchi yao wanapoendelea kukua.

### 5.1.10 Uwajibikaji

Waandishi wa bunilizi za watoto mara nyingi hutumia utanzu wa michezo ya watoto ndani ya bunilizi zao. Sababu ni kwamba, watoto hawa huelewa ulimwengu wao wa michezo katika usomaji. Utanzu huu wa michezo ndani ya bunilizi ni mbinu ya kimwingilianotanzu na waandishi hutumia mbinu hii kwa lengo la kuchimuza maudhui waliyokusudia.

Msimulizi katika Momanyi (2009) ametumia utanzu wa michezo ya watoto ndani ya bunilizi kwa lengo la kuchimuza suala la uwajibikaji wa watoto. Uwajibikaji hapa ni suala ambalo linathaminiwa sana katika jamii za Kiafrika. Watoto hufunzwa suala la uwajibikaji wakiwa wachanga na wanatarajiwa kuendeleza jukumu hilo hadi wakiwa wakubwa.

Uwajibikaji wa watoto hushuhudiwa katika ile harakati yao ya kucheza na hata katika majukumu wanayopewa wakiwa nyumbani. Watoto wakiwa pekee wakati mwingine hawahitaji mwelekezi ila wanajipanga wao wenyewe kwa wenyewe. Momanyi, (2009) katika *Mchezo wa kobole* anasema “watoto wa madarasa ya chini waliimba na kucheza katika vikundi walivyounda wenyewe” (uk. 17). “Nao watoto wale wadogo waliamua kuchezea mchanga ambao ulikuwa na unyevu baada ya mvua kunyesha. Waliunda viduta vidogo vya mchanga huo huku wakivipigapiga na kuimba.” Mfano rejelea wimbo nambari **8** (uk. 44) katika tasnifu hii.

Utendaji katika wimbo huu unaonyesha kuwa watoto wana uwezo wa kufanya mambo yao bila kuwepo na mwelekezi yeyote katika ulimwengu wao. Wao wana uwezo wa kujiamulia wanayotaka kufanya. Kando na wimbo huu kukuza maudhui ya umoja na ushirikiano, maudhui ya majukumu na nafasi za kijinsia katika jamii yanakuzwa.Tunavyoona kwenye picha katika uk. 18 na 20, kuna vikundi vya wasichana na wavulana na kila kikundi kinaonekana kufanya matendo yanayooana na jinsia zao. Kwa mfano, katika picha hizo, wavulana wanaonekana wakicheza mchezo wa kandanda unaopendwa na jinsia hiyo na wasichana kuunda viduta inayoashiria upomaji wa nyumba ya kiasili na vilevile kunyunyizia maji maua, kitendo kinachoshabikiwa na wasichana wakiwa nyumbani.

Hekaya ndani ya simulizi pia inachimuza maudhui ya uwajibikaji. Tunapozungumzia suala hili la uwajibikaji, linaweza kuwahusu wazazi ama mtoto mwenyewe. Syokau (2018) kupitia kwa hekaya aliyosimulia nyanyake Kibibi anatueleza kwamba ilibidi Katana "kubadili maisha yake na jamii yake. Angefanya lolote ambalo angeweza ili ainue familia yake kifedha." (uk.7). Hali hii ya Katana kuchukua nafasi ya wazazi wake inaonyesha kwamba ingawa tumeelezwa kuwa wazazi wake walikuwa wazee sana, si halisi mtoto kufanya kazi ya kutafutia familia yake mahitaji. Wazazi hawa wangehifadhi ama kuwekeza mali yao ili iwafaidi watoto wakiwa wachanga. Uzee hapa haupaswi kuwa sababu ya kutowajibikia watoto katika umri wao mchanga. Funzo ni kwamba, katika jamii ya Kiafrika, watoto walifundishwa majukumu ili waweze kukabiliana na changamoto za maisha.

### 5.2 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia lengo la pili ambalo ni kuchunguza namna mwingilianotanzu unachimuza maudhui katika bunilizi za watoto. Maudhui hayo ni kama dini, maadili, bidii na utiifu, umaskini, magonjwa, ushirikiano na utangamano, haki za watoto,

ushujaa, malezi, utamaduni na uwajibikaji. Maudhui hayo yote yanaafikiana na yanafaa kueleweka na mtoto Mwafrika katika mazingira yake halisi.

# SURA YA SITA

# UAMILIFU WA MAUDHUI NA VIPENGELE VYA MWINGILIANOTANZU KATIKA BUNILIZI TEULE KWA MTOTO MWAFRIKA

## 6.0 Utangulizi

Sura hii inashughulikia lengo la tatu ambalo linaangazia utendakazi wa maudhui yanayowasilishwa kupitia kwa tanzu maalum kwa mtoto Mwafrika na mazingira yake. Hapa tulichunguza ikiwa tanzu ambazo zimetumika zinafahamika na mtoto Mwafrika katika mazingira yake asilia. Pia, tuliangalia ikiwa maudhui ambayo yamechimuzwa yanaeleweka kwa mtoto mwenyewe katika mazingira yake asilia pamoja na utamaduni wake. Katika sehemu hii, mhimili wa nadharia ya Uoniafrika ulitumika ili kuhakikisha kwamba, masuala yanayozungumziwa yanamhusu mtoto Mwafrika katika mazingira yake asilia. Hali kadhalika, tuliangalia ufaafu wa vipengele vya mwingilianotanzu kwa mtoto Mwafrika. Vipengele hivyo ni kama vile matumizi ya barua, picha na michoro, hekaya, sala, maigizo, nyimbo, mashairi, mazungumzo ndani ya hadithi, matumizi ya insha na matumizi ya ndoto katika simulizi.

## 6.1 Uamilifu wa Maudhui na Tanzu mbalimbali katika bunilizi teule

Katika sehemu hii, tulijadili ufaafu wa maudhui mahsusi katika bunilizi teule za watoto. Hali kadhalika ufaafu wa nadharia ya Uoniafrika umeangaziwa kwa kujibu swali la Je, maudhui haya ambayo yamechimuzwa na vipengele hivyo vya mwingilianotanzu zinafaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake asilia? Mtoto anaelewa na kufahamu maudhui hayo?. Maudhui hayo ni kama dini, umaskini, ushujaa, utamaduni, ushirikiano na utangamano, magonjwa, malezi, haki za watoto, maadili na adabu, uzalendo na bidii kazini. Pia katika sehemu hii, tulijadili uamilifu

wa tanzu mbalimbali zinazojenga bunilizi kuu. Kwanza tulianza kwa kujadili uamilifu wa maudhui hayo.

### 6.1.1 Dini

Dini ni asasi ya jamii inayohusiana na masuala ya kiroho au imani ya binadamu katika maisha anayoishi ulimwenguni (Kiptum, 2017). Asasi hii huongoza matendo ya binadamu katika hali ya maadili. Hivyo dini huchangia katika ukuaji wa maadili ya binadamu. Imani ya binadamu hutegemea mwabudu wake na uelekezi wa waumini wake kulingana na sheria za dini husika. Kiptum (2017) anasema kwamba, dini inayoamini katika miungu huegemeza imani yake kwa kiumbe fulani au pia katika sanamu.

Waafrika kwa ujumla, walikuwa wanaabudu miungu yao tangu nyakati za mababu zao. Wamishionari walipozuru nchi za Kiafrika, waafrika walijiunga na dini mbalimbali ikiwemo Uislamu, Ukristo, Uyahudi na nyingine. Anavyoeleza Mbithi, (1992) ni kwamba, ingawa Waafrika walijiunga na dini mbalimbali zilizoletwa na wamishionari na wakoloni, Waafrika walichanganya dini hizo pamoja na dini zao za kiasili. Hivyo basi, hawakuweza kupoteza thamani yao. Badala yake, walinufaika kutokana na imani za ngeni. Katika kusisitiza kuhusu dini hizi za Kiafrika, Awolalu, (1976) anasema kwamba, dini za kiasili zilipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na hivyo Waafrika waliunganishwa na imani za dini zao kwa njia moja au nyingine kwa maisha wanayoishi kwa sasa. Hii ni kwa sababu ya kuamini na kutofahamu kwamba, Mungu na miungu huwa si kitu kimoja. Mtoto wa Kiafrika bila shaka anafahamu dini za pande zote mbili; dini za kiasili na ngeni kwa njia moja au nyingine kupitia kwa wazazi na mababu zao. Kwa hivyo. kuhusisha dini kwenye bunilizi zao jinsi anavyosema Kete, (1980) katika nadharia yake ya Uoniafrika, ni suala ambalo wanalifahamu katika mazingira wanamoishi.

Dini ina umuhimu wake katika kukuza tabia za watu katika jamii nyingi za Kiafrika. Katika bunilizi za watoto, waandishi wanajaribu kukuza suala hili la dini kupitia utanzu wa wimbo, na hata sala jinsi ilijadiliwa katika sura ya tatu na nne katika utafiti huu. Wimbo katika jamii ya Kiafrika ni utanzu unaoshabikiwa sana. Hii ni kwa sababu nyimbo zilitumiwa kuwasilisha ujumbe fulani katika sherehe mbalimbali za Kiafrika zikiwemo nyiso, harusini, kuzaliwa kwa mtoto, vitani, kazini na kadhalika.

Watoto wa Kiafrika vilevile, wana nyimbo zao za kitoto na nyimbo hizi ziliimbwa michezoni, na hata shuleni. Wanapoimba, watoto hawa mara nyingi hujaribu kuiga jinsi jamii yao huimba nyimbo hizo. Hivyo basi, waandishi wengi wa vitabu vya watoto hujaribu kuhusisha nyimbo hizi katika kazi za watoto maana watoto hawa wanazielewa katika mazingira yao. Suala la dini hapa hutegemea imani ya mtu binafsi na vilevile, jinsi anaabudu Muumba wake. Wakati mwingine, suala la dini ni suala la jamii husika.

Matundura (2008) katika *Sitaki Iwe Siri* na Nandwa (2013) katika *Kito apepeta*, wameibua suala hili la dini kupitia wimbo wa taifa katika uk. 17 na uk. 10 mtawaliwa. Wimbo wa taifa hapa nchini Kenya huanza kwa kumtambua Mungu kuwa mwenye uwezo.

**42.** Eeh Mungu nguvu yetu
Ilete Baraka kwetu
Haki iwe ngao na mlinzi
Na tukae na undugu Amani na undugu
Raha tupate na ustawi

Katika jamii za Kiafrika, watoto hufunzwa kuipenda nchi yao. Kigezo kimoja cha kuipenda nchi ni kuiombea nchi hiyo na ndiyo maana mtoto mdogo kiasi cha daraja la tatu hata bila yeye kuelewa maana ya wimbo wenyewe, huimba tu kwa kuukariri.

Utambuzi huu wa Mungu ni suala ambalo jamii huamini kuwa ni mwenye uwezo na mkuu kuliko binadamu yeyote.

Matundura (2008) vile vile ametumia utanzu wa sala kuonyesha dini katika jamii hii ya Kiafrika. Ametuonyesha jinsi Musa na dada zake wanavyorauka na kutoa sala kwa mwenyezi Mungu. “Musa alipiga magoti kando ya kitanda chake na kusema sala zake”

**43.** Baba yetu uliye mbinguni
Watazame wanao ulimwenguni
Tunaotapatapa maishani
Mayatima maskini….(uk. 2)

Mwandishi pia ametueleza kwamba ‘punde tu baada ya kutoka kitandani, Haki na Ukwa walishikana mikono ili wamshukuru Mungu kwa kumtunza nyanya yao, kuwalinda wao pamoja na kumtunza kaka yao Musa.

**44.** Mungu wetu wa haki
Shukrani kwa kumlinda Haki
Asante kwa yetu siha
Shukrani kwa maisha
Asante kwa nyanyetu
Wahifadhi wazazi wetu
Mahala pema peponi
Tusaidie masomoni
Kila siku shuleni
Amina. (uk4)

Suala la sala si jambo geni katika jamii ya Kiafrika. Hii ni kwa sababu Waafrika waliomba miungu yao kwa sababu kadhaa ikiwemo kuleta utulivu wa moyo baada ya jambo au tatizo fulani kutendeka. Kinachochochea maombi katika jamii hii ya Kiafrika mara nyingi ni wingi wa changamoto za kijamii. Hivyo basi, Mwafrika hujipata akiomba ili angalau matatizo yake yaweze kuwa mepesi. Watoto katika jamii hii huiga mambo hayo kutoka kwa wakubwa wao kwa kuwa dini ni suala ambalo wanalielewa. Hii ndiyo sababu Musa na dada zake, punde tu wanapoamka wanatoa

sala zao ili Mungu awaonee imani na kuwasaidia sana katika masomo yao na hasa kumlinda nyanya yao baada ya kupoteza wazazi wao kwa ugonjwa ambao ulibaki kuwa siri kwa miaka mingi.

Imani katika dini kwa maisha ya mtoto inafaa sana katika kukuza maadili na amali au tamaduni za jamii. Achieng (2012) anasema kwamba dini ni suala muhimu katika kukuza tamaduni za kidini ambazo jamii hukua nazo na kupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Watoto katika jamii ya sasa hukua kwa kurithi amali au tamaduni ambazo walirithishwa na kizazi tangulizi hivyo tabia zao na maadili kwa jumla hutegemea mafunzo ya jadi. Kwa hivyo, sala wanazotoa mayatima wale hutokana na jinsi walifundishwa na watangulizi wao.

Dini pia humpa mtoto matumaini katika maisha. Kupitia kwa Sala, Musa na dada zake wana matumaini kuwa nyanya yao angeishi miaka mingi na kwamba wangefaulu masomoni na vilevile walitumaini kwamba Mungu anawalinda wazazi wao mahala pema peponi. Kupitia kwa imani hii, baada ya Musa kupewa tuzo kwa ushindi wake, ndoto yao ilitimia maana walipata ufadhili wa masomo yao.


### 6.1.2 Umaskini

Suala la umaskini hapa si jambo geni katika mazingira ya Kiafrika. Kutokuwa na cha kutosha kimavazi, vyakula na hata mahala pa kuishi kunaweza kuashiria umaskini kwa kiasi kikubwa. Maudhui ya umaskini yalidhihirika sana katika kazi ya Syokau (2018), *Kade na Katana* kupitia utanzu wa hekaya ndani ya bunilizi iliyosimuliwa akina kibibi na nyanyake.

Tunapozungumzia utendakazi wa hekaya hii kwenye bunilizi za watoto ni kwamba katika jamii za Kiafrika, watoto walikuwa wanasimuliwa hadithi mbalimbali na wazee wao, ikiwemo hekaya. Utambaji wa hadithi hizi zilifanywa baada ya kazi jioni

watoto wakiota moto huku wazazi wao wakishughulika na majukumu ya nyumbani. Watoto kupatana na hekaya katika usomaji wa bunilizi zao ni suala ambalo wanalifahamu na linawafurahisha na kuwachangamsha.

Syokau (2018) anatuelezea kupitia hekaya kuhusu vijana wawili Kade na Katana waliotoka familia maskini, "…familia yake (Katana) ilikuwa inajulikana kwa umaskini wao. Yaani umaskini wao haukujificha. Madharau waliyoonyeshwa kila walipopita lilimkera na ..." (uk 7). Katika utanzu wa picha iliyoko katika uk. 14, mwandishi ametuonyesha kuhusu hali ya Katana akivalia nguo kuukuu iliyojaa viraka vya rangi aina aina. Pia, katika uk. 11, nyanya anasimulia kwamba 'Katana hakuwa na nguo nzuri za kujisitiri. Tena, zilikuwa kuukuu na zenye aibu nyingi'. Tazama (uk. 14).



**Mchoro 11: Hali ya Katana akiwa amevalia nguo kuukuu iliyojaa viraka**
**Chanzo: Syokau (2018)** ***Kade na Katana***

Katika mazingira ya Kiafrika, si jambo la ajabu kupatana na watoto wanaovalia jinsi hiyo katika mtaa. Hata hivyo, watoto wanaelewa hali kama hiyo maana watoto wenzao huenda wanapitia changamoto kama za wahusika vitabuni. Ndoa za mapema wakati mwingine hutokana na umaskini uliokithiri katika jamii. Kupitia kwa utanzu wa shairi alilokumbuka mamake Hidaya, tunaona umaskini wa uwezo kwa sababu mume wake alitaka amwoze binti yake kwa Bwana Mapesa kwa ajili ya tamaa ya

mali na ama ukosefu wa pesa za kumsomesha mtoto huyo. Baada ya mama Pembe kumkariria shairi hilo, tunaelezwa kwamba, Hidaya alipata mwamko mpya kuhusu changamoto hiyo.

Katika jamii nyingi za Kiafrika suala la ndoa za mapema hutokana na tofauti za kiuana ambapo jinsia ya kike hubaguliwa na kudunishwa katika jamii. Suala la mwanamke halipewi uzito katika jamii za Kiafrika na kwingineko ulimwenguni. Jambo hili linatokana na ukweli kwamba, jamii nyingi zimekita katika mfumo wa kuumeni ambao unahalalisha asasi za kijamii zenye kuendeleza tofauti za kiuana katika majukumu ya uzalishaji mali na ugawaji majukumu (Eagleton, 1986). Katika mfumo huu, mwanamume anapewa nafasi zaidi katika nyanja zote za kiuchumi, kijamii na kisiasa ikilinganishwa na mwanamke (Mwita, 2017). Kwa hivyo, mwanamke katika jamii nyingi za Kiafrika alionekana kama chombo cha mwanamume bali si wa kuzalisha mali katika jamii.

Namlola (2019) anatueleza kwamba “mzee Matata aliwabagua wanawe na kumpendelea yule wa kiume. Nyakati hizo, elimu ya wasichana haikuthaminiwa” (uk.9). Msimulizi anasema “kile alichompa mkewe aweke kama karo ilikuwa ya mvulana wao, Pembe” (uk. 9). Wasichana wengi huacha masomo yao maana wanaozwa pindi tu wanapofikia umri wa kubaleghe. Hivyo basi, waandishi hawana budi kuhusisha masuala hayo ya ndoa za mapema katika kazi zao ili watoto wajifundishe namna ambavyo wanaweza kuepukana na changamoto hizo.

Utanzu wa ushairi uliotumika hapa si mpya kwa watoto wa Kiafrika. Hii ni kwa sababu katika kuangalia historia kuhusu asili ya ushairi simulizi, kuna maelezo kuwa asili ya shairi ilikuwa ni ushairi simulizi hususan nyimbo (Method, 2015). Nyimbo hizi ziliimbwa katika jamii ya uswahilini barani Afrika na katika uimbaji huo ikawa

shairi la kukaririwa. Watoto hupenda nyimbo zao sana wakiwa michezoni na vilevile mashairi yao mepesi yanayohusiana na mazingira yao na vilevile umri ama madaraja yao. Hii ni kwa sababu ya ule utendaji unaoambatana na michezo hiyo.

### 6.1.3 Ushujaa

Ushujaa ni ile hali ya kuwa na moyo thabiti wenye uwezo wa kufanya mambo hata kama ni hatari (TUKI, 2004). Katika jamii ya Kiafrika, mashujaa hawa waliaminiwa kuwa viumbe wenye sifa za kiajabuajabu. Wao walikuwa wanafanya mambo kwa njia ya kushangaza. Mara nyingi, ushujaa ulionekana katika mazingira ya vitani au hata katika sherehe anuwai katika jamii ambapo mtu aliibuka kuwa mshindi.

Ushujaa katika mazingira ya mtoto hurejelea ile hali ya mtoto kufanya mambo kwa njia ya ujasiri bila kuogopa hatima yake. Mwandishi ametuonyesha mhusika Katana kwa mfano, mtoto mdogo lakini jinsi aliweza kujitahidi kutunza familia yake kwa kufanya mambo ya kiajabuajabu, ni ushujaa wa kiwango chake (Syokau, 2018). Yeye alikuwa shujaa mwanamume. Hali kadhalika, Hidaya, katika Namlola (2019) ni msichana aliyependa masomo yake na kuibuka shujaa baada ya kupambana na hali yake ya kuepuka ndoa za mapema.

Ukweli ni kwamba jamii nyingi za Kiafrika, anavyosema Balisidya (1982) ni kwamba, mwanamke katika fasihi  ya Tanzania (sawa na nchi zingine za Kiafrika) anachorwa kama mama, chombo cha starehe cha mwanamume na mali ya kumilikiwa na mwanamume. Anasisitiza kwamba kutokana na mfumodume, haishangazi kuona mtoto wa kike akidunishwa na kunyanyaswa kwa masuala ambayo yangesikizwa. Katika hali zote mbili kwa mfano, mwandishi alitaka kumwonyesha mtoto Mwafrika kwamba, changamoto za maisha husuluhishwa na watu jasiri katika jamii.

### 6.1.4 Utamaduni

Utamaduni ni suala linalomzunguka na kumtofautisha mtu mmoja na mwingine katika jamii fulani. Mwafrika asilia ni mtu anayeenzi utamaduni wake kwa njia zote; mavazi, malazi, mila na desturi zao. Tamaduni za watu fulani hujulikana kupitia kwa zana kama vile nyimbo katika sherehe mbalimbali na vile vile maandalizi ya vyakula aina fulani ambavyo watu husika huithamini sana. Waandishi wa fasihi za watoto wanajaribu kuwakumbusha watoto kuhusu tamaduni zao kupitia kwa kazi zao.

Tunapoangalia kuhusu ufaafu wa utamaduni katika bunilizi za watoto, waandishi wameweza kusisitiza suala hili kupitia mwingiliano wa tanzu ambao unawapa ari watoto kusoma zaidi bunilizi zile. Kwa mfano, nyimbo zimetumika katika bunilizi ili kuwasilisha ujumbe fulani, kando na kuburudisha na kuchangamsha. Watoto hupenda burudani. Nandwa (2013) katika bunilizi yake *Kito Apepeta* anatueleza kwamba mwalimu Pendo alipoingia darasa la nne, wanafunzi waligundua kwamba mgambo unapolia lazima kuna jambo maana halikuwa jambo la kawaida kwa mwalimu huyo kuingia darasa lile. Mwalimu Pendo alisema, "Kesho mchana, afisa mkuu wa elimu wa eneo hili atatutembelea… ninataka wanafunzi wa kumburudisha" (uk. 4). Msimulizi anaeleza kwamba "Nyuso za wanafunzi zilijaa furaha waliposikia tangazo hilo" (uk.4). Hii ni thibitisho kuwa watoto wanapenda burudani sana.

Wimbo *apepetanga* ni wimbo ulioimbwa kwa lugha moja ya kiasili. Nyimbo za kiasili huambatana na ala za muziki "*isukuti* na *Olwika*". *Isukuti* ni ngoma kutoka jamii ya Abaluhya kutoka sehemu ya magharibi mwa nchi ya Kenya. Ngoma hii imepata jina lake kutokana na ala za kienyeji ambazo ni ngoma zinazochezwa kwa mitindo maalum (Murimi, 2016). Midundo ya ala hizi huashiria utamaduni fulani maana katika jamii nyingi za Kiafrika ala za muziki hutofautiana na vile vile midundo

huashiria tamaduni za jamii fulani. Hali kadhalika, nyimbo za kiasili huwa na mavazi maalum au maleba yanaoambatana nayo yanaweza kuashiria tamaduni fulani.

Vifaa hivi vyote vinavyoambatana na wimbo huu wa *apepetanga* vimetumika kwa minajili ya kusisitiza ujumbe kwamba, waafrika lazima wazienzi tamaduni zao hata ingawa mazingira ya watoto huenda yamebadilika.



**Mchoro 12: Matumizi ya ala za muziki katika utendaji**
**Chanzo: Nandwa (2013)**

Kwenye picha nambari 13, kuna utendaji mwingi unaoambatana na mapigo ya '*Isukuti'* na '*Olwika*'. Katika kufanya hivi, watoto wanaweza kuelewa jinsi nyimbo za kitamaduni zilivyokuwa zikichezwa.


Katika hadithi ya Momanyi *Mchezo wa Kobole* (2009), kuna wimbo unaoimbwa na watoto wanapocheza uwanjani. Mwandishi anasema, "…wengine waliimba nyimbo mbalimbali huku wakicheza kwa furaha". Nyimbo hizo zilimkumbusha mwalimu siku za utoto wake. Akasimama na kusikiliza.

**45.** Salaale hiyo!
Meli imekuja
Imekuja na tanga za manjano
Bei yake ni shilingi tano
Mwaiona Haaa lele
Mwaiona ina madirisha hiyo! (uk. 17)

Wimbo huu unakuza maudhui ya utamaduni wa pwani ambako usafiri wa bahari unadokezwa kwa kutajwa kwa meli. Hii inawasaidia wanafunzi kuelewa mazingira wanamoishi wakaazi wa pwani.

Tunapoangalia kuhusu suala la hadithi, Syokau (2018) ametumia mbinu hii ya hekaya ndani ya bunilizi ili kusisitiza maudhui ya utamaduni na utiifu. Inasemekana kwamba, ngano (hadithi za simulizi za mapokeo) ndizo zilizotamalaki zaidi katika jamii za Kiafrika. Kwa mujibu wa Msokile (1999), ngano zilikuwa za awali kuzuka katika jamii baada ya wimbo wa kazi na ushairi huku athari zake zikihusu mazingira yaliyomzunguka binadamu. Katika jamii nyingi za Kiafrika, watoto walikuwa wanapewa mafundisho mengi kuhusu maisha na wakuu wao. Ilikuwa kama mila na desturi kwa sababu ilikuwa njia ya kipekee ya kupata mafundisho.

Tofauti na hadithi za vitabu, ilikuwa inapokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya moja kwa moja kupitia kwa mdomo. Mwandishi ametumia mbinu hii kwa lengo la kuonyesha kuwa tamaduni za Kiafrika bado zinaendelea ila tu ni kwa njia za maandishi. Mazingira huenda ni tofauti na uwasilisho wake pia lakini hadithi ni zile zile. Picha kwenye uk 6, mwandishi amemkumbusha mtoto jinsi hadithi hizo zilikuwa zinawasilishwa. Huu ni utamaduni unaodhihirika.



**Mchoro 13: Taswira ya maandalizi ya uwasilishwaji wa hadithi katika jamii ya Kiafrika.**

**Chanzo: Syokau (2018), *Kade na Katana***

Ndoa za mapema katika jamii za Kiafrika si jambo geni. Hii ilitokana na ule ubabedume uliokuwa umekithiri katika jamii. Mtoto wa kiume alikuwa anaenziwa ilhali mtoto wa kike alikuwa anadunishwa jinsi ilivyokuwa kwa mwanamke katika jamii nyingi. Udunishwaji huu ulitokana na mtoto wa kike kutoelimishwa au kupewa nafasi ya kusoma. Mtoto wa kike alikuwa anaozwa pindi tu alipokuwa amefikisha umri wa kubaleghe kwa ajili ya kuleta mali kwenye familia. Waliopata elimu ni watoto wa kiume.

Namlola (2019) katika bunilizi yake *Hidaya* ametuonyesha jinsi mamake Hidaya aliweza kumshauri mwanawe kupitia shairi kwamba, awe jasiri maana matatizo aliyoyapitia Hidaya kuhusu kuozwa kwa Bwana Mapesa yangepita. Suala hili la ndoa za mapema ni suala ambalo mtoto Mwafrika analielewa maana mambo hayo hufanyika katika jamii, hasa jamii zilizokithiri umaskini. Ingawaje katika jamii ya kisasa, ndoa za mapema zimepigwa marufuku, kwa sababu kuna sheria zinazowalinda watoto kuhusu haki zao.

**46.** Mola aliloamuwa, mja hana upinzani,
Ndilo litakalokuwa, hata mja afanyeni,
Ni kama ganda la muwa, lilotupwa ardhini.. (ubeti wa kwanza) uk 21

Ujumbe katika shairi hili alilokumbuka mama Hidaya ni kwamba, ingawa tamaduni zao hazikuwa zikimtambua mtoto mwanamke, alimpa moyo kwa kumwambia kwamba, kile ambacho Mungu alikuwa amepanga kumhusu, hakuna binadamu ambaye angepinga; kwamba Mungu ana mipango mizuri inayoweza kupinga tamaduni zilizokuwa zimepitwa na wakati.

Ujumbe unaotokana na shairi hili linamfaa mtoto mwafrika kwa sababu kuna jamii isiyothamini mtoto kike hususan kwa masuala ya elimu. Muhimu ni kuwahimiza watoto husika kutia bidii na kustahimili changamoto kama hizo. Mtoto mwafrika anaposoma bunilizi hii ya Namlola (2018), anatambua kwamba kuna nguvu zinazoweza kupinga tamaduni zilizopitwa na wakati.

### 6.1.5 Ushirikiano na Utangamano

Maudhui ya ushirikiano na utangamano ni jambo ambalo linawaweka Waafrika pamoja. Ushirikiano huu ulikuwepo tangu jadi maana Waafrika walifundishwa na mababu zao kushirikiana kwa masuala yaliyowahusu. Katika jamii asilia, ushirikiano ulionekana pale ambapo watu walifanya kazi pamoja mfano; kulima, kujenga, vitani, na hata katika sherehe mbalimbali kutegemea tamaduni zao. Hata hivyo, watoto

walifundishwa jinsi ya kushirikiana hasa katika kufanya majukumu mbalimbali wakiwa nyumbani. Ifahamike kwamba, majukumu hayo yalikuwa tofauti: yale ya watoto wa kike kama vile kupika, kuvua, na hata kutunza watoto wachanga. Majukumu ya watoto wa kiume yalibainika wazi vile vile kama kuchunga mifugo, kutegemea jamii husika.

Watoto huwa na umoja na mshikamano bila kujali lugha au kabila (Muge, 2018). Ushirikiano wao ni wa moja kwa moja. Watoto hawabagui wanaoshirikiana nao hasa katika ulimwengu wao wa michezo. Hii ni kwa sababu watoto hujua tu kuwa wenzao ni watoto kama wao bila kuzingatia iwapo wanatoka jamii tajiri au maskini. Mathalan, kupitia utanzu wa nyimbo, watoto huimba na wenzao katika hali ya ushirikiano na utendaji ili nyimbo husika zipate maana. Nandwa (2013) katika hadithi yake *Kito Apepeta* ametuonyesha watoto wa shule ya Khwisero walivyofurahia kuimba wimbo huo ukiwa na utendaji mwingi. Pia, ametuonyesha jinsi watoto wanashirikiana wakiwa shuleni wakifanya michezo yao bila kuwa na mwelekezi yeyote. Kwa hivyo, suala la ushirikiano linahimizwa nyumbani na wazazi na kuendelezwa kule shuleni.

Ushirikiano katika jamii za Kiafrika ulifanyika ili kukuza umoja miongoni mwa watoto na vilevile katika ugawanyaji wa majukumu. Syokau (2018) katika bunilizi yake *Kade na Katana,* anatueleza kwamba, Zambarau Kajaza anamfundisha mjukuu wake jinsi ya kupika wali na hali kadhalika kuwa makini katika kufanya kazi hiyo. "Umeosha mchele?" Nyanya alimuuliza Mueni (uk. 4). Mara nyingi watoto huiga yale ambayo wazazi wao hufanya katika mazingira ya nyumbani.

### 6.1.6 Magonjwa

Hii ni hali ya kutokuwa sawa kiafya. Suala la ugonjwa ni suala ambalo linaeleweka na mtoto Mwafrika katika mazingira yake. Hii ni kwa sababu katika hali ya kawaida,

watoto wachanga mara nyingi hukumbwa na matatizo ya homa na maumivu mengine yanayomfanya mtoto kutohisi vizuri. Katika kiwango cha daraja la tatu, watoto huwa wameanza kuelewa aina mbalimbali za magonjwa na kwa kiwango fulani visababishi vya magonjwa hayo.

Ugonjwa katika jamii ya Kiafrika, haukuchukuliwa kama jambo la kawaida, ila ulihusishwa na misukosuko ya maisha, kwamba ulitokana na kutotii wazee, miungu ama ushirikina. Mtoto Mwafrika hukua akiwa na mawazo hayo yote kuhusu ugonjwa wowote ule. Usasa umeweza kubadilisha mawazo mabovu kuhusu asili ya magonjwa kwa sababu kuna mabadiliko katika jamii yaliyoletwa na teknolojia ya kisasa na hali kadhalika, elimu wanayopata watoto kupitia shuleni.

Waandishi wa bunilizi za watoto wameibua suala la magonjwa kwa lengo la kumkumbusha mtoto Mwafrika kwamba magonjwa yapo. Kwamba, masuala ya ushirikina yamepitwa na wakati. Kea (2013) katika *msiba wa kujitakia* amejaribu kutuonyesha suala hili kupitia imani ya baba Katana kwamba, Mtu ‘anaporukwa’ hapaswi kunywa maji na hivyo aliamini kwamba mkewe hangepona. Ndio maana mzee aliweza kuomboleza kupitia shairi katika (uk 32).

**47.** Matanga ni kwomboleza, ufikwapo na mashaka
Matanga pia yaliza, machozi yakaanguka
Matanga yanatatiza, mtu tama akashika
Matanga mbali pitia, mkosi usitutie.
Matanga pia msimu, wa kuwaaga wendao (uk. 32, ubeti wa kwanza)

Mtoto Mwafrika bila shaka hukua akiwa na imani ya Kiafrika kwamba, magonjwa husababishwa na ama kutotii wakuu ama miungu na imani katika uchawi au ushirikina. Hivyo basi watoto wanapaswa kufundishwa kwa njia ya moja kwa moja kwamba imani kama hizo zimepitwa na wakati na kwamba, kila ugonjwa lazima uwe na visababishi vyake na lazima uwe na tiba yake kupitia kwa hospitali au zahanati. Kwingineko, watoto wanapaswa kuelimishwa kuhusu dawa za kiasili ambazo

zinaweza kutumika kwa mbadala ya dawa za hospitali. Dawa hizi za kiasili huaminika na Mwafrika asilia kuwa yanaweza kutumika kutibu magonjwa mbalimbali.

Kuhusu visababishi vinavyotokana na kutotii, Nandwa (2016) katika *Mchezo wa Mtelezo* kupitia barua aliyosoma Lulu na Brayo ni kusisitiza kuhusu utiifu miongoni mwa watoto. Mwalimu mkuu alikuwa anasisitiza kuhusu hatari inayotokana na mchezo wa mtelezo bondeni lakini wanafunzi hawakuwa wanaitikia. Hivyo basi ilibidi awaonyeshe kwa uhalisia kuhusu hatari inayoweza kutokea iwapo hawangetii amri hiyo kupitia kwa barua.

***48.*** *Baba…*

> *Nimebaki nikijuta…Daktari amesema mfupa wa kisigino umevunjika na sitawahi kutembea kama kawaida wala kucheza mpira…"(uk. 19)*

Matokeo ya kutotii husababisha madhara na ulemavu kwa mtoto. Barua aliyoandika Kade baada ya kuugua ugonjwa ambao hakuwa anauelewa ni msisitizo wa suala la utiifu (Syokau, 2018). Utiifu hapa hutokana na uadilifu. Jamii ya Kiafrika ilisisitiza uadilifu. Walihimiza kuwepo na mienendo mizuri kwa watoto, mwenendo na tabia inayokubalika katika jamii kuwa ni yenye haki na inayofungamana na utamaduni wa jamii husika (Ekiru, 2019).

Mwandishi pia amedokeza kuhusu ugonjwa wa UKIMWI kupitia insha aliyoandika Musa (Matundura, 2008). Mwandishi alitaka mtoto Mwafrika atambue kwamba ugonjwa huu hutokana na kuishi maisha ya anasa hasa ya kufanya mapenzi bila kinga. Wagonjwa wowote wanaougua ugonjwa huu hawapaswi kubaguliwa, ila wanapaswa kutunzwa kama wagonjwa wengine. Sababu ya kuwepo kwa ugonjwa huu kwenye bunilizi za watoto ni kwamba, itikadi za Kiafrika kuwa ugonjwa huu huenda unatokana na ushirikina, ni upotovu. Hapa, mtoto anapaswa kujua kwamba maisha ya kufanya mapenzi kiholela ni hatari kwa maisha.

### 6.1.7 Malezi

Jamii adili ni jamii huzingatia maadili za Kiafrika katika mafundisho ya watoto wao katika jamii kwa maisha ya kila siku, jamii huelekeza watoto kwa namna ambayo inakubalika. Malezi na mafundisho ya maadili huanza tu pindi mtoto anapoanza kujitambua na kuelewa mazingira anamoishi. Hivyo, mtoto anahitaji kuelekezwa katika hatua zake zote za maisha.

Ngugi, (2016) anaeleza kuwa watoto bado wanaendelea kukua kimwili, kisaikolojia na wanategemea watu wazima kuwaelekeza. Mbali na ushauri wa moja kwa moja kutoka kwa wazazi, fasihi inaweza kuchangia katika kumsaidia mtoto kukubali hali fulani na hata kujua namna ya kukabiliana na hali nyinginezo ambazo zitaendelea kuibuka katika maisha yake kila kukicha. Ngugi (2016) anaendelea kusema kwamba matumizi ya fasihi ama vitabu kama chombo cha kutolea ushauri ndiyo hurejelewa kama bibliotherapia. Hii ni mbinu ya kutumia vitabu ili kuwasaidia watu kupata suluhisho kwa hali mbalimbali zinazowakumba katika kipindi fulani cha maisha.

Sababu ya kuwepo kwa maudhui ya malezi ni kumkumbusha mtoto Mwafrika kwamba, lazima azingatie mahusiano mema akiwa popote; iwe shuleni ama katika yale mahusiano ya moja kwa moja na watu wengine. Syokau (2018) katika hadithi yake *Kade na Katana* ametuonyesha jinsi watoto wanapewa mafundisho na wakuu wao kupitia hekaya ndani ya simulizi. " ..Leo nitawasimulia hekaya. Nyanya akakalia mkeka wake mweusi uliokuwa na michoro ya minazi na kutazama ufuo wa bahari….(uk 5). Katika hekaya hii, Zambarau Kajaza nyanyake Kibibi aliweza kuwasimulia hadithi iliyokuwa na lengo la kuonyesha umuhimu wa mahusiano mema baina ya jamaa na marafiki. Kwamba, hamna haja ya husuda baina ya ndugu na dada. Pia nyanyake kibibi alisisitiza kwamba lazima kuwepo na heshima kwa wakuu.

Kupitia mhusika Katana, tunaelezwa jinsi aliweza kumsaidia ajuza yule aliyekuwa anabeba mizigo mizito.

**49.** ***Katana****: Naomba nikusaidie kuubeba mzigo huu wako mzito*

***Nyanya****: Nitashukuru sana. Wengi wanenipita hapa tu, bila neno…(uk 13)*

Mtoto anaposoma kazi hii, anatambua umuhimu wa kuwasaidia wakuu wao katika jamii. Katika ukuaji wake, ataweza kuhusiana vyema na watu. Hali kadhalika suala la bidii maishani lilisisitizwa katika hadithi. Malezi mema kwa mtoto wa Kiafrika yalibainika wazi kupitia bidii aliyotia mtu. Walezi walihimiza watoto wao watie bidii kwa lengo la kumaliza umaskini. Mara nyingi watoto walikua wakijionea mambo hayo kupitia kwa wakubwa wao. Kwa hivyo waandishi wa bunilizi za watoto hawana budi kuwajuza watoto kuhusu jambo hili kupitia kwa kazi zao.

### 6.1.8 Haki za Watoto

Suala la haki za watoto katika mazingira ya Kiafrika halikuwepo kwa sababu jamii nyingi zilisheheni ubabedume. Mara nyingi, watoto hawakusikizwa kwa masuala ambayo yalikuwa yanawahusu. Ingawa tunasema kwamba ilikuwa jamii ya ubabedume, mtoto wa kiume wakati mwingine pia angekosa mahitaji yake maana wazee ndio walikuwa wa kutoa amri. Wazee walikuwa wanaamua kila kitu katika jamii hiyo mathalan katika masuala ya ndoa. Nyakati hizo, wao wangeamua ni nani wa kuoa ama kuolewa kwa nani. Hawangeruhusu mtoto wa kiume kufanya uamuzi wao; kwa hivyo haki za watoto hao wa kiume zilikuwa zimetekwa nyara kwa kiwango fulani.

Mtoto wa kiume wakati mwingine angechukua nafasi ya babake ikiwa baba ni mnyonge/ mzee sana ama kama hayupo kabisa. Bila kuzingatia hata umri, haki zake za kulishwa na kulindwa zilikiukwa. Mathalan, Katana katika Syokau, (2018) *Kade na Katana* ambapo mwandishi anatueleza kupitia hekaya ndani ya bunilizi kwamba,

ilibidi afanye kazi ya sulubu likizoni ili kuokoa familia yake kutokana na umaskini ambao ulikuwa haufichiki. Msimulizi ametuonyesha kuhusu ukosefu wa haki kwa mtoto wa kiume ili kudhihirisha kwamba katika jamii, kuna watoto wa kiume ambao wanakosa haki zao kwa kuchukua majukumu ya wazazi wao.

Hali kadhalika kuhusu ndoa za mapema, mwandishi alitaka kuonyesha mtoto Mwafrika kwamba, mila hizo zimepitwa na wakati na kwa hivyo, serikali ina nguvu ya kukabiliana na wale ambao wanakiuka sheria za kulinda mtoto wa kike kuhusiana na tamaduni hizo. Kila mtoto ana haki ya kumaliza masomo yake ndipo aweze kujiamulia mchumba na mwelekeo wake kuhusu maisha. Katika *Hidaya* yake Namlola (2019), mwandishi ametuonyesha jinsi Hidaya, mhusika mkuu ananyimwa haki ya kuendeleza masomo yake na kutaka kuozwa kwa Bwana Mapesa katika umri wake ule mdogo. Mtoto Mwafrika asiyekuwa na maarifa haya anaweza kuerevuka kupitia kwa usomaji wa vitabu na wanaweza kupata maarifa ya kuepukana na matatizo ambayo yanawakumba, maana kuna haki zinazowalinda watoto wote kwa ujumla.

### 6.1.9 Maadili na Adabu

Jamii adili ni jamii inayochangamkiwa na wengi maana ni jamii iliyo na wingi wa amani na utulivu. Watoto katika jamii za Kiafrika walifundishwa wawe na tabia njema kwa watu wote na vilevile kuheshimu wakuu wao. Maadili islionekana katika maamkizi; kwa mfano, kuna baadhi ya jamii za Kiafrika ambazo mtoto kamwe hapaswi kuamkua mtu mzima. Hii ilitokana na mafundisho waliyopewa kuhusiana na heshima kwa watu wazima. Aliyevunja amri hizi alionekana mtovu wa nidhamu na kwa hivyo angepewa adabu kali na yeyote katika jamii hiyo. Kwa mfano, katika jamii ya Kipsigis, ni mwiko mtoto kutanguliza maamkizi kwa mkubwa wake. Angefanya hivyo, angeonekana mtovu wa nidhamu kwa wakubwa wake.

Kuwepo kwa maudhui ya maadili na adabu hapa ni dhihirisho kwamba, mwandishi alitaka kusisitiza heshima waliyofundishwa watoto hawa kutoka nyumbani. Walipaswa kuwa na maadili toka utotoni hadi utu uzima. Barua aliyoandika Kade baada ya kujiweka mamlakani na kupata ugonjwa usiotibika jinsi tunaelezwa katika hekaya ndani ya bunilizi ya Syokau (2018) ni funzo kwamba, mtoto huyo (ingawa mzima sasa) alikuwa ameyaasi mafundisho ya wazazi wake ya kutokuwa mjeuri na mzembe hali kadhalika kujitakia makuu. Matokeo yake, alihangaika na mwishowe kuomba msamaha kwa kumsaliti kaka yake.

### 6.1.10 Uzalendo

Watoto wanapaswa kufundishwa jinsi ya kupenda nchi yao maana ni mahali ambapo wataishi kwa siku zao zote. Upendo huu huonyeshwa ikiwa wataiombea na kuendeleza amani na upendo katika nchi yao. Kilicho muhimu haswa ni kufanya bidii katika kazi ili waepukane na changamoto za umaskini. Uzalendo huu unasisitizwa kupitia wimbo wa taifa katika Nandwa (2013) *Kito Apepeta* (uk. 10) na *Sitaki Iwe Siri* (uk. 17) yake Matundura (2008). Wimbo wa taifa huimbwa shuleni asubuhi na baada ya masomo. Lengo ni kuiombea nchi na mtoto anapokua, atatambua umuhimu wa ombi hilo kwa nchi yao.

Katika jamii za Kiafrika, watoto walifundishwa kuipenda jamii yao na kuilinda kutokana na adui walioweza kuwaangamiza. Katika jamii za kiasili, watu walipendana na kujiona kama jamii moja, kiwango kwamba vita vya kikabila vilipotokea, watu walishirikiana kumkabili adui. Huu ni uzalendo unaodhihirishwa katika jamii. Hali kadhalika, watu walifanya kazi pamoja ili kuzilinda familia zao.

### 6.1.11 Bidii na uvivu

Bidii ni jitihada anayofanya mtu katika kutenda jambo fulani. Jamii ya Kiafrika ilithamini sana suala la bidii na kila mcha alifundishwa kutia bidii kwa lolote lile. Hata katika ule mchakato wa kupanga masuala ya ndoa, waliohusika walichunguza ikiwa mwanandoa husika alikuwa wa bidii. Waliokuwa wavivu walikemewa vikali na hawakupendwa kabisa maana walihusishwa na umaskini na kurudisha maendeleo ya jamii nyuma.

Waandishi wa bunilizi za watoto hawana budi kuhusisha maudhui haya maana watoto wanafahamu kuwa, ufanisi hutokana na bidii katika maisha. Mhusika Katana, katika hadithi ya Syokau (2018) anatuonyesha hali halisi ya watoto wanaotia bidii nyumbani. Katana alitia bidii ili familia yake iweze kupata walichohitaji kwa sababu wazazi wake walikuwa wazee na hawakuwa na ajira yoyote. Suala hili hutokea ikiwa hali ya familia imekumbwa na changamoto za hapa na pale. Waliokosa kutimiza majukumu hayo waliadhibiwa vikali na wakubwa wao.

## 6.2 Uamilifu wa Tanzu mbalimbali katika Bunilizi za Watoto

Sehemu hii inaangazia uamilifu wa tanzu malimbali zinazojenga bunilizi kuu. Tanzu hizo ni kama, barua, mashairi, mazungmzo, insha, nyimbo, ndoto ndani ya simulizi, sala, maigizo, picha na hata hekaya ndani ya simulizi. Katika kutambua uamilifu huu, nadharia ya Uoniafrika umetumika ili kuona ikiwa tanzu hizo zinafaa kwa mtoto Mwafrika katika mazingira yake asilia.

### 6.2.1 Barua

Katika jamii nyingi za kiafrika, kulikuwepo na njia nyingi za kupitisha ujumbe. Wengine waliwasha moto juu ya mlima, wengine walipuliza tarumbeta na wengine wakapiga ngoma (KLB, 2013). Ingawaje barua imetumika baada ya ukoloni na

Umishenari, watoto wanaifahamu sasa kuwa ni njia ya kisasa ya kupitisha ujumbe. Hata hivyo, Matundura (2008) anapotumia mbinu hii ya barua katika uandishi wake, anajaribu kumfahamisha mtoto kwamba, njia moja ya kupitisha ujumbe katika jamii ni kutumia barua.

### 6.2.2 Picha na Michoro

Mtoto mchanga kwa kawaida anapenda kuangalia picha na michoro ya vitu vinavyofahamika na vilevile viumbe vya wanyama na watu wanaoelewa. Picha na michoro humpa hamu ya kusoma fasihi kwa njia moja au nyingine. Kwa hivyo, matumizi ya picha na michoro katika kazi za fasihi inafaa kwa sababu inamfanya mtoto kuelewa zaidi anachokisoma.

### 6.2.3 Hekaya ndani ya bunilizi

Watoto hushabikia sana hadithi hasa zinazohusiana na mazingira wanayoelewa ama mazingira ya kifantasia. Hadithi hizi zilikuwa njia moja ya kupitisha ujumbe wa uadilifu kwa mtoto Mwafrika. Tunapozungumzia hekaya, hizi ni hadithi zinazohusu binadamu au wanyama zilizosheheni ujanja kwa kiwango fulani. Katika baadhi ya bunilizi za watoto, waandishi hutumia hekaya kwa lengo la kuonyesha ujanja wa watu au wanyama wanaotumia akili zao ili kuhepa changamoto za maisha.

### 6.2.4 Maigizo

Katika mazingira ya kawaida, watoto huigiza mambo mengi katika michezo yao. Wao huigiza kuhusu matukio ambayo wameshuhudia katika mazingira wanamoishi mathalan matukio yanayomzingira kama vile maisha ya familia zao, mahusiano, masuala ya kiuchumi na hali kadhalika tamaduni zao zinazoambatana na mila.Watoto hupenda nyimbo kwa mfano zinazoambatana na utendaji katika tamaduni zao. Nandwa, (2013) katika *Apepetanga* ametuonyesha jinsi wanafunzi walifurahia

kuimba huku wakitumia ala za muziki kama ‘isukuti’ na ‘Olwika’ ikishirikishwa na utendaji mwingi. Utendaji huu unaashiria utamaduni wa jamii husika unaoonyeshwa kupitia usomaji wa bunilizi za watoto. Hali kadhalika, uigizaji katika michezo ya watoto katika Momanyi, (2009) *Mchezo wa Kobole* unamulika matendo ambayo yanafanywa katika jamii husika. Kwa hivyo, mtoto Mwafrika anaposoma bunilizi hizi humkumbusha tu kuhusu mambo ambayo tayari anayaelewa.

### 6.2.5 Utanzu wa sala ndani ya bunilizi

Sala katika jamii za Kiafrika ni suala ambalo lilitiliwa mkazo sana. Waafrika waliabudu miungu yao iliyoaminiwa kuwa ni kinga katika jamii. Hii ni kwa sababu Waafrika waliamini kuwa walikuwa wamezingirwa na maadui wengi. Hali kadhalika, kuamini kwa miungu yao kuliwapa matumaini katika maisha yao ya kila siku. Katika Matundura (2008), Musa anasali kwamba “ Watazame wanao ulimwenguni” (uk 2). Hii inamaanisha kwamba watoto hao wana matumaini kwa maisha yao. Kwa hivyo, kuhusisha sala katika maandishi ya bunilizi ni muhimu kwa sababu zinampa mtoto kutambua umuhimu wa kuwepo kwa Mungu na dini katika maisha yao ya kila siku.

### 6.2.6 Utanzu wa ndoto ndani ya simulizi

Kuota ndoto si jambo geni kwa maisha ya kila siku. Watoto huota kuhusu matukio ya hapa na pale. Ndoto hizo huja kutegemea mambo ambayo yamewazunguka, michezo, mambo ambayo wameyasikia na mengine ambayo wamekumbana nayo. Kuhusisha kipengele cha ndoto katika uandishi ni muhimu kwa sababu unamulika hali halisi ya maisha. Syokau (2018) katika *Kade na Katana* ameonyesha jinsi Kade kakake Katana kuhusu nduguye Katana akitoka matembezini. Badala ya fujo zake za kila siku, aliamua kukaa mtulivu akiwa na lengo la kumnyang’anya mkufu. Syokau (2018) ametumia ndoto katika kazi yake ili kumtahadharisha mtoto Mwafrika kuhusu ujanja

wa watu ambao wanaweza kujifanya ni wazuri na kumbe wana ubaya katika matendo yao.

### 6.2.7 Insha ndani ya bunilizi

Watoto wa daraja la tatu wana uzoefu wa uandishi wa insha kwa Kiswahili au Kiingereza. Wao hufundishwa kuandika insha kuhusu masuala mengi katika mazingira yao. Wao huandika kuhusu masuala ibuka kama vile magonjwa mbalimbali, uchumi, siasa na mengine. Pia, huandika kuhusu wanyama mbalimbali, shule yao na insha zozote za kubuni. Insha inapotumika katika kujenga bunilizi kuu, ni jambo ambalo watoto wanashabikia sana.

### 6.2.8 Mazungumzo ndani ya hadithi

Olagunju (2013) anachukulia mazungumzo kuwa hali ya kuongea na kuzungumza pamoja. Katika mpangilio wa jamii ya Kiafrika, watu waliishi pamoja kutegemea utamaduni husika na kufanya kazi pamoja. Hii ni kwa sababu walichukuliana kama ndugu mmoja (Olagunju, 2013). Hii ndio sababu watu hawa walihitaji wawasiliane kuhusu mambo ambayo yalikuwa yanawazunguka kwa kutumia lugha moja.

Watu uhusiana katika jamii kupitia uzungumzi wa moja kwa moja au usiokuwa wa moja kwa moja. Kila mtu huzungumzia mwenzake kutegemea mahitaji. Wakubwa kwa wadogo, vijana kwa wazee, watoto kwa watoto na kadhalika. Katika jamii nyingi za Kiafrika, watoto walipaswa kuonyesha heshima hasa walipozungumza na wakubwa wao. Hii ilidhihirika katika maamkizi kutegemea jamii husika. Syokau (2018), alihusisha kipengele cha uzungumzi katika kazi yake kwa lengo la kuonyesha maadili yatakikanayo kwa mtoto anapohusiana na wazee wake. Suala hili linasisitizwa katika jamii nyingi za Kiafrika.

### 6.2.9 Utanzu wa nyimbo ndani ya bunilizi

Nyimbo katika mazingira ya mtoto ni kitu kinachopendwa sana. Watoto huimba wakicheza, huimba darasani na walimu mara nyingi huhusisha nyimbo katika mafundisho yao. Katika jamii nyingi za Kiafrika, watoto huiga nyimbo zinazoambatana na tamaduni zao. Watoto hupenda nyimbo zinazoambatana na mila zao. Aidha, hufurahia wakiimba pamoja na wenzao wakiwa shuleni. Hali kadhalika, watoto hushuhudia nyimbo mbalimbali katika kikao cha tamasha za muziki ambapo nyimbo na sanaa nyingi huandaliwa. Sanaa hizi husheheni tamaduni mbalimbali za jamii za Kiafrika. Msimulizi katika Matundura (2008) anasema kwamba "Kito aliongoza wimbo. Bila uoga, aliimba akiwatazama wanafunzi wenzake, akizunguka kutoka upande mmoja hadi nyingine….aliwageukia watazamaji na wakaguzi" (uk 31). Mtoto mara nyingi hufahamu uimbaji huu hasa wakati wa mashindano ya tamasha za muziki. Ikumbukwe kwamba, uimbaji huu huandamana na maleba. Mavazi haya huchangamsha watoto kwa sababu wanafurahia utamaduni wao. Nyimbo hizi za kitamaduni hukuza umoja na ushirikiano na huibua hisia chanya kuhusu uasilia wa mazingira wanamotoka watoto (Abby, 1989).

### 6.2.10 Mashairi katika bunilizi

Kando na watoto kupenda nyimbo, wao pia hupenda kuyakariri mashairi. Mashairi ya watoto huwa nyepesi na hubeba maudhui mepesi. Mashairi hayo husheheni masuala katika mazingira ya mtoto, mathalan wanyama, maua, chakula chao, shule na wazazi wao. Shairi huweza kukaririwa au kuimbwa kutegemea umri wa watoto. Katika kiwango cha daraja la tatu, watoto hukariri mashairi kutegemea mada husika. Mashairi hayo hutoa funzo kwa mtoto kwa njia moja au nyingine.

### 6.3 Hitimisho

Sura ya tano imeshughulikia uamilifu wa maudhui yaliyochimuzwa na vipengele vya mwingilianotanzu kwa mtoto Mwafrika. Maudhui mbalimbali pamoja na vipengele vinavyojenga bunilizi teule za watoto vinaeleweka kwa njia ya moja kwa moja na mtoto Mwafrika katika mazingira yake ya kiasili.

Maudhui kama vile dini, umaskini, ushujaa, utamaduni, ushirikiano na utangamano, magonjwa, malezi, haki za watoto, maadili na adabu, uzalendo na bidii kazini yalijadiliwa.Vilevile, hadithi, maigizo, nyimbo, sala, hekaya ndani ya simulizi zilijadiliwa. Tanzu hizi pamoja na maudhui hayo yanaeleweka na mtoto Mwafrika. Ikumbukwe kwamba mtoto hukua hata kama mazingira yatabadilika, wao hucheza, huota, husimuliwa hadithi, huzungumza na jamaa zao na hali kadhalika huigiza mambo ambayo yanawahusu. Kwa hivyo, watunzi wamefaulu kuweka kati mtoto Mwafrika katika bunilizi zao kimaudhui na kifani.

# SURA YA SABA

# MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

## 7.0 Utangulizi

Sura hii imetoa muhtasari wa tasnifu kwa kurejelea kila sura, matokeo na mapendekezo ya utafiti kutokana na ufasiri wa data iliyochanganuliwa katika sura ya tatu, nne na tano. Yafuatayo ni maelezo kuhusu muhtasari wa kila sura ya utafiti huu.

## 7.1 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii ina sura saba ambazo zimeingiliana na kuchangiana katika kukamilishana. Sura ya kwanza imeshughulikia usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada na umuhimu wa utafiti. Pia imeshugulikia upeo na mipaka ya utafiti na misingi ya kinadharia ambapo tulijadili nadharia za mwingilianomatini na nadharia ya Uoniafrika. Mwisho, mbinu za utafiti ambapo njia za kukusanya data, uteuzi wa sampuli, vifaa, uwasilishaji na uchanganuzi wa data ilijadiliwa.

Katika suala la utafiti, uchunguzi wa namna mwingilianotanzu unachimuza maudhui katika bunilizi za watoto wa daraja la tatu limeangaziwa. Hii ni kwa sababu mwingiliano tanzu katika bunilizi za watoto una uamilifu mkubwa katika kuwasilisha ujumbe unaodhamiriwa na mtunzi kwa mtoto Mwafrika. Mwingiliano huu wa utanzu huwezesha bunilizi za watoto kuwa na ladha kwa msomaji na kufikisha ujumbe kwa mtoto kwa njia rahisi.

Suala hili la utafiti liliongozwa na malengo matatu: Kupambanua namna tanzu mahsusi zinajenga bunilizi teule za watoto, kuchanganua namna vipengele vya mwingilianotanzu vinachimuza maudhui mahsusi kwa mtoto Mwafrika na mwisho,

kuhakiki ufaafu wa maudhui yanayowasilishwa kupitia tanzu husika kwa mtoto Mwafrika katika mazingira yake.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini ambayo ilizalisha dhana ya mwingilianotanzu. Nadharia hii ilitusaidia katika kuchanganua lengo la kwanza na lengo la pili. Aidha nadharia ya Uoniafrika ilishirikishwa ili kutusaidia kutathmini ikiwa maudhui yaliyochimuzwa kupitia vipengele vya mwingilianotanzu vilimfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake asilia. Nadharia zote mbili zina umuhimu maana katika kuangalia jinsi vipengele vya mwingilianotanzu vinachimuza maudhui, maudhui hayo yanafaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake asili.

Sura ya pili ni ufafanuzi wa mbinu za utafiti ambapo njia za kukusanya data, uteuzi wa sampuli, vifaa, uwasilishaji na uchanganuzi wa data ilijadiliwa. Utafiti ulichukua muundo wa kimaelezo. Katika kukusanya data, utafiti wa maktabani ulifanywa ambapo vipengele vya mwingilianotanzu vilihakikiwa kutoka kwa bunilizi teule.

Sura ya tatu inahusu mapitio ya maandishi na kiunzi cha kinadharia. Katika sura hii, tumepitia baadhi ya maandishi yanayoeleza kuhusu Mwingilianomatini na vilevile maandishi kuhusu mwingilianotanzu. Kadhalika, kuna maandishi yanayoelezea kuhusu nadharia ya Mwingilianomatini na nadharia ya Uoniafrika. Nadharia ya Mwingilianomatini ilitufaa katika upambanuzi wa vile vipengele vya kimwingilianotanzu katika bunilizi za watoto. Nadharia ya Uoniafrika ilitufaa katika kuangalia ikiwa vipengele hivyo na maudhui yaliyochimuzwa yanamfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake. Matumizi ya nadharia hii yalibaini pengo ambalo halikuwa limeshughulikiwa katika tafiti zilizotangulia. Pengo inayozibwa ni kuchunguza ikiwa vipengele vya mwingilianotazu pamoja na maudhui yanayochimuzwa yanafaa mtoto Mwafrika katika Mazingira yake asilia.Maudhui

yanayochimuzwa na vipengele vya mwingilianotanzu vinapaswa kumfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake asilia. Hivyo basi nadharia hizo mbili zilituongoza katika kufikia malengo na maswali ya utafiti huu.

Katika sura ya nne, tulishugulikia lengo la kwanza ambalo linahusu upambanuzi wa vipengele vya mwingilianotanzu katika bunilizi za watoto. Katika sura hii, tumefafanua vipengele kama vile nyimbo, ambapo tumeangalia kipengele hiki katika tanzu mbalimbali kama vile wimbo ndani ya usimulizi, wimbo ndani ya michezo ya kuigiza. Hali kadhalika katika utanzu wa wimbo, tumeangalia wajibu wa nyimbo katika bunilizi za watoto. Vipengele kama vile matumizi ya mashairi, barua, mazungumzo ndani ya hadithi kwenye usimulizi, ndoto, hekaya ndani ya hadithi kwenye usimulizi, sala, insha, maigizo na vipengele vingine vimechanganuliwa. Hali kadhalika, dhima ya mwingilianotanzu katika bunilizi za watoto imepitiwa.

Katika sura ya tano, tumeshughulikia lengo la pili ambapo kuna uchanganuzi wa namna vipengele vya kimwingilianotanzu vinachimuza maudhui mahsusi kwa mtoto Mwafrika. Vipengele kama nyimbo, hekaya, mazungumzo, matumizi ya sala, picha na michoro, insha, mashairi, michezo ya watoto vimehakikiwa. Vipengele hivi vimetumika kuchimuza maudhui kama vile, dini, maadili na adabu, umaskini, magonjwa, ushirikiano na utangamano katika jamii, haki za watoto, ushujaa, malezi na utamaduni.

Sura ya sita linahusu lengo la tatu na imejadili uamilifu wa maudhui yanayowasilishwa kupitia tanzu maalum kwa mtoto Mwafrika. Hapa uamilifu wa maudhui katika sura ya tano umechunguzwa ikiwa mtoto Mwafrika anaufahamu katika mazingira yake asilia. Hali kadhalika, uamilifu wa vipengele vya mwingilianotanzu umejadiliwa ikiwa mtoto anayafahamu vipengele hivyo au la.

Hatimaye katika sura ya saba tumehitimisha kwa kufafanua muhtasari, matokeo, mahitimisho na mapendekezo ya utafiti.

### 7.2 Matokeo na Mahitimisho ya Utafiti

Sura hii imeshughulikia matokeo ya utafiti kwa mujibu wa malengo ya utafiti. Malengo haya yamefanikishwa kwa kutumia nadharia ya mwingilianomatini na nadharia ya Uoniafrika. Nadharia zote mbili zina umuhimu katika kuangalia jinsi vipengele vya mwingilianotanzu vinachimuza maudhui, maudhui hayo yanafaa kumfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake ndipo malengo matatu ya utafiti yakaweza kutimizwa. Hali kadhalika mahitimisho ya utafiti yameshughulikiwa. Yafuatayo ni matokeo kuhusu malengo haya ya utafiti.

#### 7.2.1 Mwingilianotanzu katika Bunilizi za Watoto

Utafiti huu uliohusu mwingilianotanzu na uchimuzi wa maudhui katika bunilizi za watoto ulikuwa na matokeo kadha wa kadha. Mathalan, kuhusu vipengele vya kimwingilianotanzu, utafiti ulibaini kwamba katika bunilizi za watoto, kuna vipengele vingi ambavyo hutumiwa na waandishi wa kazi za watoto ambapo humpa mtoto msukumo wa kusoma kazi zao. Utafiti huu ulibaini kwamba, vipengele hivi huwekwa na waandishi kwa lengo la kuibua maudhui fulani kwa msomaji.

Katika upambanuzi wa vipengele hivi, ilibainika kwamba, bunilizi teule*; Mchezo wa Kobole* (Momanyi,2009), *Hidaya* (Namlola, 2019), *Mchezo wa Mtelezo na Hadithi Nyingine* (Nandwa, 2016), *Kito Apepeta* (Nandwa, 2013) *Msiba wa kujitakia* (Kea, 2013) *Sitaki Iwe Siri (*Matundura, 2008), *Kade na Katana* (Syokau, 2018) umesheheni mwingiliano wa tanzu kama nyimbo, shairi, picha na michoro, hadithi ndani ya simulizi, maigizo na michezo ya watoto, matumizi ya ndoto, mazungumzo, na barua hupatikana kwenye bunilizi kuu. Hii inamaanisha kwamba, kuna mwingiliano wa

tanzu katika bunilizi kwa sababu tanzu hizi hutegemeana na kuathiriana kwa lengo la kuwasilisha ujumbe fulani kwenye kazi za mwandishi.

### 7.2.2 Uchimuzi wa Maudhui

Utafiti huu uliweza kudhihirisha kwamba, maudhui mbalimbali katika bunilizi teule za watoto huchimuzwa na vipengele kadhaa vya kimwingilianotanzu. Maudhui kama vile umaskini, dini, maadili, utamaduni, uzalendo na mengineyo huweza kuibuliwa na vipengele kama vile sala, nyimbo na hadithi kwa lengo la kutoa funzo fulani kwa msomaji.

Ni bayana kwamba, watoto wanapenda burudani na michezo mingi katika mazingira yao. Ulimwengu wa mtoto ni michezo na ufumbuzi wa masuala mengi yanayowahusu katika jamii. Matundura, (2008) katika bunilizi yake '*Sitaki Iwe Siri'* alithibitisha kwamba watoto hucheza michezo mingi ikiwemo ya mwaficho. Wengine walicheza mpira uliotengenezwa kwa karatasi ya plastiki. Huu ni mfano tu lakini inabainika kwamba katika bunilizi nyingi, waandishi wa bunilizi za watoto huhusisha michoro mingi katika kazi zao. Hata hivyo wanapokuwa nyumbani au shuleni, wao hupenda nyimbo na michezo yao ya kitoto. Kwa mfano, Momanyi, (2009) katika *Mchezo wa Kobole* (uk. 17, 18 na 20) anathibitisha hali hii. Watoto hujiweka katika makundi tofautitofauti kulingana na umri wao. Kutokana na hali hii, waandishi wa bunilizi za watoto hutumia sana kipengele cha nyimbo katika kazi zao ili kuwasilisha ujumbe utakaomfikia mtoto katika njia mwafaka.

Hali kadhalika tanzu mbalimbali zilizojitokeza katika bunilizi za watoto zilimfaa mtoto Mwafrika katika mazingira yake. Hekaya, kwa mfano zilitumika katika kupitisha ujumbe fulani kwa mtoto. Mara nyingi, hekaya hizi zilitumika katika kuwaonya watoto kuhusiana na jambo fulani na hali kadhalika kuleta funzo la uadilifu

katika jamii. Katika bunilizi ya Syokau, (2018) katika *Kade na Katana,* Zambarau Kajaza bibiye Kibibi aliwasimulia wajukuu wake hekaya katika uk. 5, kwa lengo la kutoa funzo la uadilifu, kuhimiza ushirikiano na heshima kwa wazee.

Tunapozungumzia maamkizi katika mazungumzo, mtoto Mwafrika hana budi kujifundisha. Hii ni kwa sababu katika jamii nyingi za Kiafrika, watoto walipaswa kuelewa jinsi ya kuhusiana na kutangamana na wakuu wao. Mtoto mdogo hapaswi kuamkua mtu mzima. Mtoto angefanya hivyo, angeonekana mtovu wa nidhamu na angeadhibiwa vikali katika jamii hiyo. Hali hii inajitokeza katika bunilizi ya Syokau, (Keshatajwa) uk.13. Zambarau Kajaza alitaka wajukuu wake watambue jinsi ya kuamkuana na kuheshimu wazee wao.

Katika utendaji wa baadhi ya vipengele hivi, dhana ya Uafrika unajitokeza kwamba, vipengele vinavyozungumziwa na mwandishi inafahamika katika mazingira ya mtoto mfano matumizi ya ala za muziki, usimulizi wa hadithi miongoni mwa mengine.

### 7.2.3 Uamilifu wa Maudhui na vipengele vya Mwingilianotanzu

Hatimaye, utafiti huu ulitimiza lengo la tatu la utafiti huu kwa kudhihirisha uamilifu/utendakazi wa maudhui na vipengele vinavyowasilishwa kupitia tanzu husika kwa mtoto Mwafrika katika mazingira yake. Maudhui kama vile dini, magonjwa, utamaduni, umaskini, maadili, uwajibikaji, malezi yanaeleweka katika mazingira ya mtoto Mwafrika. Hivyo basi, uchimuzi wa maudhui haya yanafaa maana mtoto ana uwezo wa kuelewa kinachozungumziwa na mwandishi katika usomi wake.

Imebainika kwamba, maudhui yanayochimuzwa katika bunilizi teule ni muafaka kwa mtoto Mwafrika. Maudhui kama vile utamaduni, ushujaa, ushirikiano na utangamano, malezi, dini, umaskini, magonjwa na ujirani mwema ni masuala ambayo yanaishughulisha jamii za Kiafrika na kwa hivyo yanamhusu mtoto Mwafrika.

Bunilizi hizi basi zinakuwa nyenzo za kuelimisha mtoto wa Kiafrika na kumhami na maarifa ya jinsi ya kukabiliana na changamoto za jamii yake.

Vipengele vya mwingilianotanzu, vinavyojitokeza katika bunilizi teule vinaeleweka katika mazingira ya mtoto Mwafrika. Vipengele kama nyimbo, mashairi, maigizo, ndoto, picha na michoro vinaeleweka hasa katika mazingira anamokulia mtoto wa Kiafrika anayelengwa na bunilizi teule za Kiswahili.

### 7.3 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu una mchango mkubwa katika uwanja wa uandishi. Utawazindua waandishi wa bunilizi za watoto katika kuangazia masuala anayoyaelewa mtoto wa Kiafrika katika kazi zao. Mbali na kukuza stadi ya kusoma, bunilizi za watoto lazima ziangazie masuala ibuka yanayoweza kuwakumba watoto katika jamii. Aidha, utafiti huu unachangia katika kuimarisha nadharia zilizotumika za kuhakiki bunilizi teule. Nadharia hizi zinajitokeza kama msingi wa kukuza na kuendeleza uandishi wa bunilizi za watoto, fasihi ya Kiswahili na fasihi nyingine za Kiafrika.

### 7.4 Mahitimisho

Mijadala na uhakiki iliyoendelezwa katika tasnifu hii imebainisha kwamba bunilizi za watoto ni mojawapo ya tanzu za fasihi andishi ya Kiswahili. Imebainika kuwa mwingilianotanzu ni mojawapo ya mbinu ambazo zimetumika kuchimuza maudhui katika bunilizi teule za watoto. Maudhui yanayochimuzwa na vipengele vya kimwingilianotanzu yanaeleweka na mtoto Mwafrika katika mazingira yake halisi.

Tanzu zinazoingiliana na maudhui yanayochimuzwa katika bunilizi yanamsaidia mtoto Mwafrika katika kukuza lugha na kupata hamu ya kutaka kusoma zaidi fasihi ya watoto kwa ujumla. Usomaji wa bunilizi hizi utamsaidia mtoto kujifunza mengi

hasa kuhusiana na changamoto zinazokumba jamii yake na jinsi ya kukabiliana na changamoto.

Utafiti huu ulibainisha matumizi ya mihimili ya nadharia ya mwingilianomatini kwamba hakuna kazi ya kifasihi inayoweza kujitegemea pasipo na kutegemea kazi zingine tangulizi zinazofanya zikamilike. Kupitia kwa nadharia hii, imebainika kwamba, vipengele vya kimwingilianotanzu hutegemeana na kuingiliana kwa lengo la kuchimuza maudhui maalum katika bunilizi kuu.

**7.5 Mapendekezo**

Utafiti huu ni muhimu sana katika kitaaluma. Hii ni kwa sababu unawahamasisha waandishi wa bunilizi za watoto kwamba, vipengele vinavyotumika katika uandishi husaidia kuchimuza maudhui yanayofahamika na mtoto Mwafrika katika mazingira yake asilia. La muhimu ni kwamba, usomaji wowote wa bunilizi za watoto unapaswa kujali mtoto Mwafrika katika mazingira yake. Utambuzi kuwa kuna mwingilianotanzu katika bunilizi za watoto, utafiti huu unapendekeza kuwa utafiti mwingine unaweza kufanywa kwa kutumia nadharia hii ya mwingilianomatini katika vipengele vingine vya fasihi ili kuona matokeo yake yatakavyokuwa.

Pili, baada ya kuhusisha nadharia ya Uoniafrika katika utafiti huu, utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu Uoniafrika kwa kuelekezwa na nadharia nyingine za fasihi za Kiswahili. Hii ni kwa sababu Mwafrika anapaswa kuhusishwa na mambo yanayomhusu katika mazingira yake asilia.

Data zilizotumika katika utafiti huu ni bunilizi teule za watoto katika maktaba. Hivyo basi, tafiti zaidi zinaweza kufanywa kwa kuhusisha data pana zaidi au hata data zingine. Kwa mfano kuna haja ya kuendeleza utafiti huu katika maeneo mengine

ambayo hayakuangaziwa. Kwa mfano, tamathali za usemi na mbinu za kimuundo na nyinginezo ambazo zinapatikana katika bunilizi za watoto.

Kuhusu tafiti za baadaye, waandishi wa bunilizi za watoto wanafaa kuhusisha mtoto Mwafrika katika kazi zao kwamba, katika kazi zozote za kifasihi lazima wamtambue mtoto katika mazingira yake asilia.

.

**MAREJELEO**


Abedi, A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: East Africa Literature Bureau.

Abdalla, A. O. (2014). *Kuchunguza dhamira za kijamii na Kiutamaduni katika Riwaya za Shafi Adam Shafi: Mfano wa Kuli na Vuta N'kuvute.* Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa)

Abby, A. (1989). The role of play songs in the moral, social, and emotional development of African children. *Research in African Literatures*, *20*(2), 202-216.

Achebe, C. (1976). *Morning not yet on Creation Day*. New York: Anchor Books.

Achebe, C. (1990). *Hopes and Impendiments: Selected Essays*. New York: Anchor Books.

Achieng, O. B. (2012). *Sifa za mashujaa na umuhimu wao Kwa jamii zao: ulinganifu wa Fumo Liyongo na Lwanda Magere*:Tasnifu ya uzamifu; Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Adwar, S. (2009). *Managing Transition into adolescent through performing arts for active learning: A case of elocution*. A research paper presented at the fifth PPMC symposium on African Music held at Moi Girls School, Eldoret. Kenya.

Agalo, J. (2012). *Emerging role of media as the language art in children's literature in Kenya.* Journal in Humanities and Social Sciences, Vol.4, No 1

Akoleit, J. (1990). *Response and Criticism in Children's Literature in Kenya: The Case Study of Barbara Kimenye.* MA Thesis Kenyatta University (Unpublished).

Akuno, E. A. (1999). *A conceptual Frame work for Research in Music Education within a Cultural Context*. Paper presented at cultural week seminer, Kenyatta University, Nairobi.

Ali, J. A. E. (2017). *Kuchunguza Dhamira katika Riwaya ya Kiu ya Mohamed Suleiman Mohamed* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).

Alison, D. (2019). *How to Start a Letter with Professional Greeting Examples*. Tovuti

Allen, G. (2000). *Intertextuality*. London: Routledge.

Abedi, K. A. (1954). *Sheria za kutunga mashairi*. East African Literature Bureau.

Asante, M. K. (2003). *Afrocentricity: The Theory of Social Change* (Revised and Expanded Edition). Chicago Illinois: African Images.

Asante, M. K. (1980). International/intercultural relations. *Contemporary black thought*, 43-58.

Asante, M. K. (1998). *The Afrocentric Idea* (Revised and Expanded Edition). Philadelphia: Temple University Press.

Asante, M. K. (2000). *The Western Journal of Black Studies*

Awolalu, J. O. (1976). What is African traditional religion. *Studies in comparative religion*, *10*(2), 1-10.

BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Bakize, L. H. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es salaam: TUKI

Bakize, L. H. (2015). Gender Balance Struggles in Tanzanian Kiswahili Children's Literature. *Kiswahili,* 78

Bakize, L.H., na Senkoro, F. E. M. K. (2019). Shujaa wa Kike katika Bunilizi za Kihistoria za Watoto katika Kiswahili. *Kiswahili*, 82

Baktin, M. M. (1986). *Speech Genres and Other Late Essays*. Austin: University of Texas Press.

Balisidya, M.L. (1982). The Image of the Woman in Tanzanian Oral Literature: A Survey. *Kiswahili,* 49

Bauman, R. (2004). *Cross-Cultural perspectives on Intertextuality.* Oxford: Blackwell publishing Ltd.

Best, W. R., & Gall, M. (1996). *Educational Research an Introduction.* New York. Longman.

Bogdan, R., & Biklen, S. K. (1992). *Qualitative Research of Education: An Introduction to Theory and Methods*, Boston: Allyn and Bacon.

Bower, V., & Barrett, S. (2014). Rhythm, rhyme and repetition. *Developing Early Literacy 0–8: From Theory to Practice. London: SAGE*, 118-134.

Gall, M. D., Borg, W. R., & Gall, J. P. (1996). *Educational research: An introduction*. Longman Publishing.

Brandel, R. (1959). *The Music of Central Africa An Ethnomusicological study*. London: Methuen

Bwire, T. O. (2004). *Uhakiki wa tamthilia ya watoto kama zao la michezo ya utotoni* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).

Chawane, M. (1954). *The Development of Afrocentricity: A Historical Survey*. Mides Chawana. University of Johanesburg ..midasc@uj.ac.com.

Chike, F. M. (2015). *The Critical Concept of Afrocentrism in Nigerian Literature.* Tasnifu.Chuo Kikuu cha Exeter

Chinwenizu. (1987). *Decolonizing the African mind*. Lagos: Pero Press.

Chukwolo, J.C. (2009). Afrocentrism or Eurocentrism: The Dilemma of African Development. *The New Journal of African Studies*.

Clayton, J., & Rothstein, E. (1991). *The Influence of Intertextuality in Literary History*. Wisconsin: The University of Wisconsin Press.

Disasa, J. (1988). African Children's Attitude toward Learning. *Journal of multicultural counseling and development*, *16* (1), 16-24.

Eagleton, M. (1996). *Feminist Literary Theory: A reader.* Basil and Blackwell. New York.

Ehlers, L., & Frank, C. (2008). Child participation in Africa. *Children's Rights in Africa: A Legal Perspective*, 111-128.

Ekiru, S. (2018). *Uadilishaji wa Mtoto katika Ujenzi wa Jamii Adili: Tathmini ya Hadithi za Watoto. Katika Fasihi ya Kiswahili: Utafiti na Maendeleo Yake.* CHAKAMA. Dar es Salaam.

El-Kaiim, M. F. S. (1985). *Ufasaha wa ushairi*. Kenya Literature Bureau.

Erastus, D. (2017). *Tunajifunza Nini Vita Dhidi ya Kiswahili*. www.mwanachitoday.co.tz.

Fox, G. (Ed.). (1976). *Writers, Critics, and Children: Articles from Children's Literature in Education*. New York: Agathon Press.

Fox, G. na wengine (1977). *Writers, Critics and Children.* New York, Agatho

Gataka, G. (2012). '*Uhakiki wa Maudhui Teule katika Utenzi wa Mikidadi na Mayasa'*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Nairobi. (Haijachapishwa).

Gitonga, (2017). Uchambuzi Linganishi wa Fani na Maudhui ya Nyimbo za Harusi za Kimeru na za Kiswahili: Chuo Kikuu cha Nairobi: Tasnifu ya Uzamili. (Haijachapishwa).

Herman, L. (2011). Dhima ya mwingilianomatini katika Hadithi za watoto katika Kiswahili. Katika *Kioo Cha Lugha*, juz. 9. kur. 73-83

Hodgson, D. L. (1999). Women as children: Culture, political economy, and gender inequality among Kisongo Maasai. *Nomadic peoples*, 115-130.

Ibala, H. (2018). *Jukumu la Vyombo vya Kielektroniki katika Ukuzaji wa Fasihi ya Watoto" katika Fasihi ya Kiswahili: Utafiti na Maendeleo yake*. Tuki: Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Ismael, Z. S. (2015). *Historia ya Fasihi ya Watoto Tanzania: Maendeleo na mafanikio.* Wasilisho katika kongamano la CHAWAKAMA-AFRIKA MASHARIKI lililofanyika katika chuo kikuu cha Kyambogo Uganda, bewa la Shimoni PTC

Jones, K. (2008). *How to Write Effective poetry for Kids.* Katika http://www.helium.com./items/1176034-childrens-poetry-childrens-Humour-writing-for-children.

Kahigi, K.K. (1995). " Lugha katika Vitabu vya Watoto," katika, Kioo cha Lugha, Juz.10 uk 122-134.

Kenguru, P. M. (2013). *Athari za Fasihi Simulizi katika Riwaya ya Utubora Mkulima.* Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Nairobi: Nairobi

Khamis, S. A. M. (2007). Utandawazi au Utandawizi? Jinsi lugha ya Riwaya mpya ya Kiswahili inavyodai." Katika *Kiswahili*, Juzuu namba 70, Dar es Salaam

Kijumwa, M. (1913). *Utenzi wa Fumo Liyongo katika Tenzi Tatu za Kale* (mh M. M Mulokozi). Dar es Salaam: Tuki.

King'ei, K. (2000). *Miale ya Uzalendo*. Nairobi: Phoenix Publisher

Kinoti, T. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

KLB (2013). History and Government. Nairobi: KLB

Kinara, G. (2012). *Maudhui ya UKIMWI katika Ua la Faraja na Kala Tufaha*. Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Kobia, J. M. (2008). *Utendaji katika Nyiso za WaIgembe*. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi New Age International, Ltd.

Kubo, M. (2011). *Mwangaza wa Fasihi*. Nairobi: The National Educational Service.

Kristeva, J. (1980). *Desire in Language: A Semiotic Approach to Literature and Art*. New York: Columbia Press.

Lemanster, T. (2012). *What is intertextuality, Great World Text: A programme of the centre for Humanities,* University of Wisconsin- Madson, Wisconsin.

Macha, N. (2013). *Matumizi ya mtindo wa Mwingilianomatini kwenye Tendi*. Makala katika www.chomboz.blogspot.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: nadharia, historia na misingi ya uchambuzi*. Dar es salaam: Mture Educational Publ..

Maitaria, J. N. (2010). Methali kama Fomula ya Uwasilishaji wa Ushairi wa Kiswahili: mfano wa Mashairi ya Abdilatif Abdalla, katika P. S. Malangwa na Bakize, L. H. (Wah). (2010). *Kioo Cha Lugha*. (Juz 8): Uk 33-49. Dar es Salaam: TATAKI.

Maria, N. (1995). *Aspects and issues in the History of childrens Literature.* Greenwood

Masebo, J. A., & Nyangwine, N. (2000). Nadharia ya Fasihi. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Mazrui, M. (1998). *Maamkizi na Utamaduni wake Uganda*. Jinja Books Printing Press.

Mbithi, J. S. (1992). Introduction to African Religion.Nairobi: EAEP publishers.

Method, S. (2015). *Umahiri Katika Fasihi ya Kiswahili. Mwongozo kwa mwanafunzi na mwalimu wa Fasihi Simulizi na Andishi.*

Ministry of Education. (2002). Ministry of Education and Technology: Primary School Education Syllabus. *Juzuu* 1. Nairobi: Ministry of Education.

Mnenuka, A. (2010). Fomula ya Tamthilia ya ndani ya Tamthilia ( PTT) katika *"Tamthilia Teule za Kiswahili*," katika Kioo cha Lugha . Juz. 8., kur.93-106.

Mohochi, S. (2000). Kiswahili na Vyombo vya Habari nchini: Matatizo katika Matumizi ya Lugha. Katika: *Kiswahili katika Karne ya ishirini na moja.*

Momanyi, C. (2009). *Mchezo wa Kobole.* Nairobi: Oxford University Press

Moses, W. na wenzake (2019). *Matumizi ya Nyimbo za Kizazi Kipya kama Mbinu ya Kufundishia Masuala Ibuka katika Shule za Upili Nchini Kenya.* Katika Isimu na Fasihi ya lugha za Kiafrika. Eldoret: Moi University press.

Mrikaria, S.E. (2015). Nyimbo za watoto na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Katika jarida la *Kiswahili na maendeleo ya jamii. Uk. 123-137* Wahariri: Mwenda Mukuthuria, James Ontieri, Mosol Kandagor na Leonard Sanja.

Muge, T. (2018). Nafasi ya Fasihi ya Watoto katika Ukuzaji wa Mshikamano wa Kitaifa: Katika Mwanga wa Lugha. *Jarida la Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika*, Chuo Kikuu cha Moi.

Murimi, (2016). Mwingilianotanzu katika Modern Taarabu-Mipasho: Chuo Kikuu cha Moi. Tasnifu. ( Haijachapishwa).

Murimi, J, Obuchi, S na Kandagor, M (2016). Mwingilianotanzu katika Uainishaji wa Tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiswahili. Journal of Education Research, Vol. 2.

Mulokozi, M. M (1989). Tanzu za fasihi Simulizi. Katika, *Mulika. Na.21*. Dar es Salaam: Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili.

Mulokozi, M. M., & Kahigi, K. K. (1995). *Malenga wa bara*. University Press.

Mutembei, A.K. (2009). *UKIMWI katika Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TATAKI

Mnyampala, (1965). *Diwani ya Mnyampala*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Ndalu, A. (1997). *Mwangaza wa Kiswahili.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Ndumbaro, E. (2013). *Taathira katika Fasihi: Msingi wa kuwepo motifu za aina moja katika Tanzu anuai za Fasihi za mataifa /makabila tofautitofauti ulimwenguni.* Makala katika www.chombez.Blogspot.

Nduye, G. (2015). *Dhima ya Mwingilianomatini katika Hadithi za Watoto za Kabila la Wabena.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Njeri, G. (2019). *Usawiri wa Familia ya Kisasa katika Fasihi ya Watoto Nchini Kenya.*Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Njogu, K., & Chimera, R. (1999). Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu. Nairobi: JKF

Ngugi, E. (2018). *Maudhui na Mtindo katika Ushairi wa Watoto: Uchanganuzi wa Utenzi wa Haki za Watoto na Mashairi BulBul.* Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Kenyatta.Haijachapishwa.

Ngugi, M. B. (2014). *Umilisi wa Stadi za Maamkizi katika Ujifunzaji wa Kiswahili. Chuo kikuu cha Kenyatta.* Tasnifu (Haijachapishwa.)

Ngugi, P. Y. (2012). Children’s Literature Research in Kenyan Universities: Where are we now?. *International Journal of Arts and Commerce*, *1*(2), 60-77.

Ngugi, P. (2012) “Tafsiri katika Fasihi ya Watoto: Mbinu na Mikakati.” Katika: Omari na Mrikaria . Mulika. Tataki. TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ngugi, P. (2011). *Language and Literacy Education: The State of Children’s Literature in Kenya.* Berlin: Lambert Academic Publishing.

Ngugi, P. (2000). Nafasi ya Muziki Uliopendwa katika fasihi ya Kiswahili: *Swahili Forum* VII. 145-152

Niane, D. T. (1965). *Sundiata: An epic of Old Mali* (Tr. G.D. Pickett) London. Longman.

Nikolojeva, M. (1996). *Intertextuality in childrens literature.* New York: Gorland Publishers.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. (Mhr.) (2007). “Ufundishaji wa Masuala-ibuka katika shule nchini Kenya,” Katika *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya*. Nairobi: Twaweza Communications. 11-23.

Nyoni, T., & Nyoni, M. (2013). The Form and Content of Children's Poetry and Games on a Kaleidoscopic Cultural Terrain. *Theory & Practice in Language Studies*, *3*(2).

Longhorn. (2014). Kamusi ya Karne ya 21. Nairobi: Longhorn Publishers.

Ojiambo, B. T. (2004). *Uhakiki wa Tamthilia ya Watoto kama zao la Michezo ya Utotoni.* Chuo Kikuu cha Nairobi. Tanifu. (Haijachapishwa).

Okofor, V. O. (2010). Understanding the Afrocentric conceptual Paradigm, katika Robertson, C. C. (mh). *Africa Rising: Multidisciplinary Discussion on African Studies and History.* Asmara: Africa World Prss, inc.

Olagunju, O. (2013). Globalization and inter-religious dialogue in African cultural context. *Journal of Studies in Social Sciences*, *2*(1).

Omar, A. (1981). *How Learners Greet in Kiswahili. Across sectional Survey: Apaper presented at An International Conference on Pragmatics and Language Learning.* Indiana University.

Ouma, O. K. (2013). *Uhakiki wa Maudhui Teule katika Utenzi wa Nabii Isa*. Tasnifu ya Uzamili iliyotolewa katika chuo kikuu cha Nairobi: Haijachapishwa

Osore, M. (2020). Kiswahili kama Nyenzo ya Umoja na Mshikamano Nchini Kenya Ikilinganishwa na Nchini China. *Mulika Journal*, *38*(1).

Osazee, Fayose, P. (1991). Children’s Literature Research in Africa: Problems and Prospects. In Saur K.G (ed.) Children’s literature Research. Munchen. International Resources and Exchange.

Ramadhan, T.S. (2018). *Utendaji katika Nyimbo za Ngoma ya Wassamba: Mifano kutoka Mdumange Nchini Tanzania.* Tasnifu katika Chuo Kikuu cha Moi. Haijachapishwa.

Reichard, S. (1998). *Poetry for Children*. Retrieved from; http://www.Suite101.com/article.cfm/childrens-writing.

Republic of Kenya. (2010a). *The Kenya Constitution*. Nairobi: Government Printer.

Republic of Kenya. (2010b). *Children Act 2001: Chapter 141*. Nairobi: National Council for Law Reporting.

Robert, S. (1958). *Maisha ya Siti binti Saad:'mwimbaji wa Unguja*.

Robert, T. C. (1994). *Afrocentricity:* The Sceptic dictionary.sceptic.com

Sanders, J. (1967). Psychological Significance of Children's Literature Katika *The Library Quartely*. The University of Chicago Press. 15- 22. 27-2-2014.

Scott, W. V., & Deirdre, D. J. (2009). *Research Methods for Everyday Life Blending: Qualitative and Quantitative Approaches.* Jossey-Bass Publishers. United States of America.

Senkoro, F. E. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi*, KAUTTU, Dar es Salaam.

Senkoro, F. E. (1982*). Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Siks, G. B. (1978). *Drama with Children.* New York, Harper and Row

Silverstein, N. (1969). Godard and Revolution. *Salmagundi*, (9), 44-60. Silverstein, N. (1969). Godard and Revolution. *Salmagundi*, (9), 44-60.

Simala, I, (2006). *Fasihi Simulizi katika enzi ya utandawazi. Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Nairobi: Twaweza Communications.

Slade, P. (1973). *An Introduction to Children's Drama.* London, University of London Press.

Scott, D. (2017). A mixed methods study of North Carolina principals' perceptions of the roles of school social workers.

Stebbing, B. (1999). Learning Through Play: A Manual for Early Childhood Educators. Harare: UNICEF.

TUKI, (2004). Kamusi ya Kiswahili sanifu. Dar es salaam: TUKI

TATAKI, (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Dae es salaam: TUKI

Taylor, C. (2009). *A secular age*. Harvard university press.

Taylor, S. J., & Bodgan, R. (1984). *Introduction to Qualitative Research Methods: The Search for Meaning.* New York: John Wiley and Sons.

Tucker, N. (1981). *The child and the book: A psychological and literary explorations.* London: CUP.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la pili). Nairobi: Oxford University Press.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Tatu). Dar es Salaam/ Nairobi: TUKI/ Oxford University Press.

Ussi, U. J. (2015). *Suala la utendaji katika michezo ya jadi ya watoto: mfano kutoka Bumbwini-Zanzibar* (Doctoral dissertation, Chuo Kikuu cha Dodoma).

Ventriglia, L. (1992). Stages of Second Language Acquisition. ESOLD – Instructional Leadership, Retrieved 16 November, 2017, from http://file://nfs5.ucn.muni.cz/profiles/447388/Desktop/Stages2ndAcqRev2.pdf ]. p.1-2.

Wafula, M. N. (2011). 'Tradition'versus 'modernity': generational conflict in Vuta n'Kuvute, Kufa Kuzikana, Msimu wa Vipepeo and Tumaini.

Walliman, N. (2005). *Your research project: a step-by-step guide for the first-time researcher*. Sage.

Wamalwa, M. K. (2018). *Language Choice, Performance Aesthetics and Quality in selected Kenyan Films* (Doctoral dissertation, Moi University).

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi*.Nairobi: Focus Books

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Focus Books

Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Wanjala, W. F. (2015). *Mwingilianotanzu katika fasihi simulizi ya Kiafrika: Mfano wa embalu na mwaka kongwa*. Tasnifu ya uzamifu: Chuo Kikuu cha Kenyatta Nairobi. (haijachapishwa)

Wasambo, W. (2014). *A Traditional Ritual Ceremony as Edurama: A Case Study of Imbalu Ritual among the Bukusu of Western Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

White, L., & Couzens, T. (Eds.). (1984). *Literature and Society in South Africa.* Johannesburg: Maskew Miller Longman.

**Bunilizi Teule**

Nandwa, R. (2013). *Kito Apepeta*. Nairobi: Queenex Publishers Ltd.

Nandwa, R. (2016). *Mchezo wa Mtelezo.* Nairobi: Queenex Publishers Ltd.

Kea, (2013). *Msiba wa Kujitakia*. Nairobi. Phoenix Publishers.

Matundura, (2008). *Sitaki Iwe Siri*. Nairobi. Longhorn Publishers.

Momanyi, (2009). *Mchezo wa Kobole*. Nairobi. Vude-Muwa Publishers.

Namlola, (2019). *Hidaya*. Nairobi. East African Publishers.

Syokau, (2018). *Kade na Katana*. Queenex Publishers Ltd.